

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 21 Aprili, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Kikao cha Kumi na Nne katika Mkutano wetu huu wa Tatu. Natumaini Waheshimiwa Wabunge mmeshazoea namna ya kuvihesabu hivi vikao. Mkutano wote huu wa Bajeti ni Mkutano wa Tatu tangu tuanze. Kwa hiyo wote ni Mkutano wa Tatu, kila siku ni Kikao kimoja, kwa hiyo Mkutano ni mmoja ni wa Tatu, lakini vikao kila siku ni kikao tofauti. Kwa hiyo leo ni Kikao cha 14 cha Mkutano wetu wa Tatu.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Mchengerwa.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Tunaanza na TAMISEMI ambayo ina maswali matatu siku ya leo. Swali la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini. Mheshimiwa Mbunda, tafadhali.

Na. 114

**Kuanza Kujenga na Kukarabati Hospitali ya  
Mji wa Mbinga**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga na kukarabati majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Mbinga kutokana na kukosa baadhi ya majengo na yaliyopo kuchakaa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA  
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Mbinga ina majengo saba ambayo ni jengo la akinamama, jengo la huduma za Bima, jengo la upasuaji, jengo la

maabara, jengo la kuhifadhia maiti, jengo la mionzi na jengo la wagonjwa wa nje. Baadhi ya majengo hayo yana uchakavu wa wastani na mengine yana uchakavu wa hali ya juu. Jengo muhimu linalokosekana katika hospitali hiyo ni jengo la wodi ya watoto. Serikali imefanya tathmini ya hali ya uchakavu wa miundombinu ya hospitali hiyo ili kuona namna bora ya kufanya ukarabati au ujenzi wa hospitali mpya ya halmashauri. Kuanzia Mwaka wa Fedha 2017/2018 hadi 2019/2020, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri imefanya ukarabati wa jengo la wodi maalum na jengo la wagonjwa wa nje kwa gharama ya shilingi milioni 45.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma za afya katika Halmashauri ya Mji wa Mbanga na katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imeipatia Halmashauri ya Mji wa Mbanga shillingi milioni 500 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Kituo cha Afya, Kalembo ambacho ukarabati wake umekamilika na huduma zinatolewa ikiwemo huduma za upasuaji. Aidha, mwaka 2021 Serikali imeipatia shillingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma matatu ya Zahanati za Kagugu, Iringa na Ruwaita. Vile vile katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali imeomba kuidhinishiwa shillingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma matatu ya zahanati katika Halmashauri ya Mji wa Mbanga.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa awamu itaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya kutolea huduma za afya nchini kote ikiwemo katika Halmashauri ya Mji wa Mbanga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Mbanga Mjini nimekuona, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Naibu Waziri wa TAMISEMI kwa majibu mazuri, lakini vile vile niipongeze Serikali kwa kutoa huduma nzuri katika maeneo mbalimbali kwenye fani ya afya. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa hospitali hiyo ilijengwa mwaka 1970, jengo la *OPD* na jengo

la upasuaji ni majengo ambayo yamepitwa na wakati na hayaendani na hadhi ya hospitali ya wilaya pamoja na jengo la wodi ya watoto ambao limekosekana kabisa.

Je, Serikali itaanza lini kushughulikia ujenzi wa majengo ya *OPD*, upasuaji na wodi ya Watoto?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; katika hospitali hiyo kuna uhaba wa watendaji, wafanyakazi, Madaktari na watendaji wasaidizi. Je, ni lini Serikali itachukua hatua ya kuhakikisha kwamba changamoto hiyo inatatuliwa? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jonas William, Mbunge wa Mbanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nipokee pongezi za Mheshimiwa Mbunda na kwamba Serikali imeendelea kuboresha sana huduma za afya kwa kujenga miundombinu, lakini pia kuhakikisha vifaatiba na dawa zinapatikana. Kuhusiana na hospitali hii kuwa kongwe ni kweli. Hospitali hii imejengwa miaka ya 70 na ni hospitali ambayo kimsingi ni chakavu, inahitaji kuboreshewa miundombinu ili iweze kuendana na majengo ambayo yanaweza kutoa huduma bora za afya kwa ngazi ya hospitali ya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hayo, ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba Serikali imeanza kufanya tathmini ya uchakavu wa majengo yale na upungufu wa majengo ambayo yanahitajika katika hospitali ile ili sasa tuweze kuona namna ya kutenga fedha kwa ajili ya kuanza *either*, kukarabati majengo yale na kuongeza yale majengo yanayopungua au kuanza ujenzi wa hospitali mpya. Kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba

tathmini hiyo itakapokamilika tutakuja na jawabu la njia sahihi ya kwenda kutekeleza ili kuondokana na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kweli kuna changamoto ya upungufu wa watumishi katika kada mbalimbali katika hospitali hiyo na nchini kote kwa ujumla. Katika bajeti yetu tumeeleza mipango kwamba baada ya kukamilisha miundombinu ya majengo, tutakwenda kuhakikisha tunaboresha upatikanaji wa vifaatiba, lakini suala linalofuata muhimu na linapewa kipaumbele cha hali ya juu ni kuhakikisha sasa tunakwenda kuomba vibali vyta kuajiri watumishi wa afya katika ngazi zote za vituo vyta afya, zahanati na hospitali ili tuweze kutoa huduma bora zaidi. Kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunda kwamba, katika Hospitali hii ya Mji wa Mbinga pia tutaweka kipaumbele katika kuajiri watumishi ili kuendelea kuboresha huduma za afya.

**SPIKA:** Bado tuko TAMISEMI, Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata.

Na. 115

**Barabara ya Kilando – Katete – Kazovu - Korongwe**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya kutoka Kilando – Katete – Kazovu – Korongwe katika Wilaya ya Nkasi itakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa Rukwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabaraya Kirando – Korongwe ina urefu wa kilomita 35. Matengenezo ya barabara hii yalianza mwaka wa fedha 2017/2018 kwa kuanza na usanifu wa barabara yote ya kilomita 35 na usanifu wa daraja moja la mita 40 la Mto Kavunja; Usanifu wa madaraja mawili yenye urefu wa mita 12.6 kila moja.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017, *TARURA* ilifungua Barabara ya Kirando – Kazovu yenye urefu wa kilomita 22 iliyotengenezwa kwa gharama ya shilingi milioni 108.37. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, kiasi cha shilingi milioni 11.4 zitatengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara yenye urefu wa kilomita 11.4.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali ilianza ujenzi wa daraja la Mto Kavunja lenye urefu wa mita 40 kwa gharama ya Shillingi billioni 1.76 na shillingi milioni 954.70 zimeshapokelewa na ujenzi unaendelea ambapo daraja hili linatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2021. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2021/2022, daraja hili litatengewa kiasi cha shilingi milioni 500.

Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara na madaraja yaliyobaki kwenye Barabara ya Kirando – Korongwe kulingana na upatikanaji wa fedha ili kuondoa changamoto ya usafiri kwa wananchi wa Kazovu, Kitete na Korongwe katika Wilaya ya Nkasi.

**SPIKA:** Kwa majibu hayo Mheshimiwa Bupe ameridhika. Kumbe una swali la nyongeza, karibu.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa naipongeza Serikali kwa kutenga kiasi cha shilingi billioni 1.7 kwa ajili ya barabara hiyo, lakini barabara hiyo imechukua muda mrefu sana, zaidi ya miaka mitano haijatengenezwa kabisa na madaraja yote yamekatika kabisa. Wananchi wa Kata ya Isaba, Kazovu, Bumanda, Korongwe, Katete wanapata tabu sana wakati wanapotaka kwenda kupata huduma za afya katika Kata

ya Kirando. Swali la kwanza; nataka kujua, ni sababu zipi zimesababisha kusimama kwa ujenzi wa barabara hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuongozana nami mguu kwa mguu kwenda kuona tatizo lillipo katika wilaya hiyo? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa David Silinde, Naibu Waziri TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tunakiri kabisa kwamba sababu kubwa ya kuchelewa ama kutokukamilika kwa wakati kwa barabara hii kwa muda mrefu ni kutokana na kuwa na bajeti finyu. Hivyo tumeendelea kufanya matengenezo ya kawaida kwa kipindi hiki cha miaka hii ambayo Mheshimiwa Mbunge alikuwa anaieleza. Hata hivyo, tunaahidi mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba Serikali bado itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya barabara hii kwa ajili ya kuwasaidia wananchi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwa sababu ya kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Mbunge ya kuwapigania wananchi wa maeneo ya Nkasi pamoja na Mkoa mzima wa Rukwa na najua kila siku amekuwa akitukumbushia katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwenye barabara hizi, nimuhidi kabisa mara baada ya Bunge hili nitaongozana naye tukawasikilize wananchi na kupatia ufumbuzi barabara hizo. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, nimekuona.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Changamoto ya barabara ambayo imetoka kutajwa ya Kirando – Katete ni sawasawa na changamoto ya kutoka

Wanging'ombe kwenye Jimbo la Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, kutoka Wanging'ombe kuelekea Kipengele, Lupira, Kijombo hadi Lumbira ile barabara ambayo iko chini ya TARURA. Naomba kuuliza, je, ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa sababu hadi dakika hii ninavyozungumza wakazi wamekuwa wakilala njiani wakati wanaposafiri kutokana na changamoto ya barabara hiyo? Kwa hiyo, naomba majibu ya swali hili. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Festo Sanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anafahamu na bahati nzuri ameainisha katika eneo ambalo Naibu Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, jimboni kwake ndiko barabara ilikoanzia, lakini kwa sababu mimi na Mheshimiwa Mbunge pamoja na yeye mwenyewe anafahamu katika bajeti fedha ambazo tumekuwa tukitenga na tunaahidi mbele yako kwamba tutaendelea kutenga fedha kwa kadri zinavyopatikana kuhakikisha hii barabara inapitika wakati wote. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata, la mwisho kwa TAMISEMI, linaulizwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, Mheshimiwa Mtaturu.

Na. 116

### **Kujenga Barabara kwa Kiwango Cha Lami – Ikungi**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya ujenzi wa barabara ya urefu wa kilomita tano kwa kiwango cha lami Wilayani Ikungi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali kuitia Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (*TARURA*) imepanga kufanya usanifu na tathmini ya gharama za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika Mji wa Ikungi. Utambuzi wa barabara hizi umekuwa shirikishi ili kutoa kipaumbele kwenye barabara zenyе umuhimu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2021, *TARURA* imetoea shilingi milioni 598.22, kati ya shilingi milioni 890.89 zilizotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenyе urefu wa kilomita 97.92 katika ya Wilaya ya Ikungi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali itaomba kuidhinishiwa shilingi milioni 925.08 kwa ajili ya matengenezo yenye urefu wa kilomita 92.6. Vilevile Shilingi bilioni 1.4 zitatengwa kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Mihuye Wilayani Ikungi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufanya usanifu na kujenga barabara kwa kiwango cha lami kwenye maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Ikungi kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa majibu ambayo yanaeleza zaidi barabara za kawaida kwa sababu milioni 900 haina uwezo wa kujenga kilometa ya lami hata moja. Kwa hiyo naomba sasa kujua kwa sababu Mji wa Ikungi ni mpya kwa maana ya wilaya ni mpya na kwa sababu Makao Makuu ya Wilaya tunategemea

yawe na lami. Sasa naomba njue kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu alituhakikishia tangu 2019 na leo ni 2021; je, ni lini hasa Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga hizo kilometa tano ya lami ili wananchi wa Ikungi nao waweze kupata lami na kufaidi matunda ya uhuru? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ametaka kufahamu ni lini sasa Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga kilometra tano za lami katika Makao Makuu ya Wilaya yake katika eneo la Ikungi. Ni kwamba, kama katika jibu letu la msingi tumeainisha hapa kwamba katika mwaka huu wa fedha 2021/2022, tumeponga kuititia Wakala wa Barabara Vijiji na Mijini kwa maana ya TARURA kutenga fedha kwa ajili ya kufanya usanifu na tathmini za gharama ya ujenzi kwa kiwango cha lami katika eneo hilo. Kwa hiyo mara baada ya usanifu na tathmini ya kina ambayo itakwenda kufanyika katika mwaka huu wa fedha maana yake katika mwaka wa fedha unaofuatia tutaanza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa lami katika eneo la Ikungi. Nimehakikishie, Serikali ya Rais wa Sita, mama Samia Suluhu Hassan iko tayari kukamilisha ahadi hiyo kwa vitendo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nimekuona Mheshimiwa Juliana Shonza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kufahamu kwamba, ni lini barabara ya kutoka Mlowo kwenda Kamsamba ujenzi wake utaanza, ikizingatiwa kwamba, suala zima la upembuzi pamoja na usanifu limeshakamilika, lakini pia ni barabara ambayo ipo kwenye llani ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na ni ahadi

ya Mheshimiwa Rais ya Awamu ya Tano pamoja na Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alipokuja kwenye kampeni. Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, barabara za nyumbani hizo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA – MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, barabara hii naifahamu vizuri ni barabara ambayo inasimamiwa na *TANROADS*. Ni kutoka Mloo mpaka Kamsamba ambapo ni nyumbani kwetu kabisa ni kilometra 166.6 na miaka yote imekuwa ikihudumiwa na *TANROADS*. Bahati nzuri kwasababu Serikali ni moja na ndio maana iko katika llani ya Chama cha Mapinduzi ninaamini mimi na yeze tukishirikiana kwa pamoja ile barabara itajengwa kwa kiwango cha lami na ninajua Serikali imeipangia fedha kwa ajili ya ujenzi utakaoanza hivi karibuni. Ahsante sana.

**SPIKA:** Asante. Waheshimiwa tukubaliane tuhamie Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano. Swali la Mheshimiwa Abdalla Rashid Rashid, Mbunge wa Kiwani.

Na. 117

**Serikali Kujenga Tuta Kuzuia Maji ya Bahari ya Hindi  
Kutoathiri Mashamba – Kiwani**

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga tuta kuzuia maji ya Bahari ya Hindi yasiathiri mashamba na mazao ya Wakulima wa Vijiji vya Nanguji, Jundamiti, Mwambe na Kiwani?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
MUUNGANO NA MAZINGIRA** aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kabla ya kujibu swalil la Mheshimiwa Abdalla Rashid, Mbunge wa Jimbo la Kiwani, kutoa maelezo mafupi yafuatayo kuhusu ongezeko la kina cha maji bahari (*Sea Level Rise*):-

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya athari ya mabadiliko ya tabianchi katika dunia yetu ni kuongezeka kwa ujazo wa maji ya bahari (*Sea Level Rise*). Kwa mujibu wa takwimu za kisayansi zilizopo, kina cha maji ya bahari kimeongezeka kwa wastani wa sentimeta 21. Ili kutimiza lengo la kupambana na mabadiliko ya tabianchi, nchi wanachama wa mkataba zilianzisha mifuko ya fedha kama vile *Least Developed Countries Fund, Adaptation Fund, Green Climate Funds* na *Global Environment Facility*. Nchi zillizoendelea ziliyahidi kuchanga fedha na kuziweka kwenye mifuko hiyo. Hata hivyo, kuna changamoto ya urasimu ndani ya sekretarieti ya mifuko ambayo husababisha uidhinishaji wa miradi kuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swalil la Mheshimiwa Abdalla Rashid, Mbunge wa Jimbo la Kiwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ujenzi wa kuta za bahari hugharimu fedha nyingi, ambazo ni vigumu kuzipata kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali itaendelea kuandaa miradi ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuendelea kufanya ufuutilaji wa karibu ili kupata fedha kuititia mifuko hiyo na kuwezesha Serikali kujenga kuta hizo mara fedha zitakapopatikana. Aidha, wakazi wa maeneo ya Nanguji, Jundamiti, Mwambe na Kiwani kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge wanahimizwa kuibua miradi ya ujenzi wa matuta wakati wa *TASAF* ya III Awamu ya Pili ambayo utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2021.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdalla Rashid, Mbunge wa Kiwani, swalil la nyongeza.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali na pia niishukuru Serikali kwa kupeleka fedha katika maeneo hayo ya ujenzi wat uta hilo. Na nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa, miradi hii inagharimu fedha nyingi katika utekelezaji wake, lakini katika utekelezaji huo Serikali haikutumia mafundi wazuri na hatukupata matokeo mazuri katika ujenzi wa tuta hilo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia mafundi bobezi ili wananchi waweze kunufaika na ujenzi huo wa tuta?

Mheshimiwa Spika, lakini swalii la pili, Naibu Waziri atakuwa yuko tayari kufuatana nami ili kwa macho yake aende kushuhudia ujenzi wat uta uliofanyika katika *phase II* ya *TASAF* Awamu ya Pili?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Hamad Hassan Chande tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali haifanyi shughuli zake kwa kubahatisha upo utaratibu maalum ambao umeandaliwa wa kutumia wataalamu bobezi. Wataalam ambao wana uwezo mkubwa wa kujenga miradi hiyo, ili ufanisi uweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, lakini swalii lake la pili, niko tayari kwa sababu ya juhudii zake ambazo nimeziona katika jimbo lake kufuatananaye bega kwa bega, hatua kwa hatua mpaka katika jimbo hilo kuona sehemu husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maida, nimekuona, uliza swalii la nyongeza.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo linalowaathiri wananchi wa Nanguji na Kiwani linafanana kabisa na tatizo linalowaathiri wakazi wa Kijiji cha Kojani. Na kwa kuwa, wananchi wa Kijiji cha Kojani wamekuwa wakilalamika muda mrefu kuhusiana na suala la maji ya bahari kuwaathiri katika makazi yao ya kudumu. Je, Serikali ina mpango gani au inaweza kuweka mkakati gani ili kuweka ukuta, pamoja na alama, lakini ili kunusuru makazi ya wananchi wa Kijiji cha Kojani? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano. Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, majibu kwa Wakojani huko.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kojani ni ndani ya jimbo lang na Kojani ni sehemu yangu nitashawishi Serikali na kuandika miradi tofauti kwa ajili ya kuhami kisiwa hicho cha Kojani. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kumbe wewe mvuvi bwana. Wakojani ni wavuvi maarufu sana. (*Kicheko*)

Tuhamie Wizara ya Fedha na Mipango. Swalii la Mheshimiwa Halima James Mdee.

Na. 118

### **Tozo ya Asilimia Moja kwa Mkopaji wa Benki ya Kilimo**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

(a) Je, ni nini sababu ya kuweka tozo ya ada ya tathmini ya asilimia moja kwa mkopaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo ambapo asilimia 50 inalipwa kabla ya kuanza kufanya tathmini na asilimia 50 inalipwa baada ya mkopo kuidhinishwa?

(b) Je, ni kigezo gani kilisababisha tozo kuwa asilimia 1 na si vinginevyo?

(c) Je, mkopo usipoidhinishwa hiyo asilimia 50 ya asilimia moja iliyolipwa inarudishwa ama la?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Mchomba, majibu ya swali hilo tafdhali.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ada ya tathmini ya mikopo inayotozwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo ya Tanzania ni kwa ajili ya kulipia gharama za uchambuzi wa maombi ya mkopo ambayo ni pamoja na shajara, uhakiki wa mradi pamoja na dhamana ya mkopo.

(b) Mheshimiwa Spika, kigezo kinachotumika kutoza ada ya uchambuzi wa maombi ya mikopo ni gharama halisi za uchambuzi wa maombi ya mkopo zinazotokana na nguvu ya soko kwa wakati husika. Aidha, utaratibu huu ni wa kawaida kwa taasisi za fedha kutoza ada ya uchambuzi wa maombi ya mikopo.

(c) Mheshimiwa Spika, endapo mkopo hautaidhinishwa, asilimia 50 ya asilimia moja iliyolipwa huwa hairejeshwi kwa mwombaji wa mkopo kwa kuwa kiasi hicho kinakuwa kimetumika kulipia gharama za uchambuzi wa mkopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Sekta ta kilimo ni sekta ambayo inaa jiri kati ya asilimia 65 hadi 70 ya Watanzania, hii ni robo tatu ya Watanzania wanategemea hii sekta moja kwa moja, *directly* ama *indirectly*. Lakini sasa

ukiangalia mikopo iliyotolewa kwa sekta binafsi kwa mwaka huu uliopita eneo la kilimo ambalo linatengemewa na asilimia 65 mpaka 70 ya Watanzania limepeata asilimia 8.7 tu ya mikopo yote iliyotolewa kwa sekta binafsi. Sasa na hii inajumuisha Benki ya Kilimo yenyewe pamoja na hizi benki nyingine. Sasa hiki ni kiashiria kwamba, mazingira ya kibenki sio rafiki kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu, kwa kuzingatia haya, Serikali ina mikakati gani, mosi kuiongezea mtaji benki ya kilimo, lakini pili kuzungumza sasa na mabenki haya mengine ya biashara ili kuwe kuna riba rafiki ili wakulima waweze kukopa mikopo? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, Benki ya Kilimo ni mionganoni mwa benki ambayo ina mikopo chechefu sana, na taarifa ya CAG iliyopita imeonesha kwamba, kati ya mikopo chechefu ya shilingi bilioni 129 iliyorekodiwa ni mikopo chechefu ya shilingi bilioni 2.1 tu iliyoweza kukusanywa. Sasa Serikali ina mkakati gani basi, kuhakikisha kwamba, hii mikopo inakusanywa ili kutoa nafasi kwa wakulima wengine kuweza kukopa na benki kuendelea kama kwaida? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Mcemba, tafadhalii.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali maswali aliyoyasema. Na kipengele cha pili cha swali lake ndio kinatoa majibu ya kipengele cha kwanza kwamba, ni kwa nini inaonekana mikopo inayokwenda kwenye sekta hiyo ni kidogo:-

Mheshimiwa Spika, sababu yake ni hiyo ambayo umeweza kuona kwamba, hata Mdhibiti, CAG, aliweza kuonesha kwamba, sekta hiyo inaongoza kwa mikopo chechefu.

Mheshimiwa Spika, na sababu kubwa na ameuliza mkakati ni nini wa Serikali:-

Mheshimiwa Spika, utasikiliza mara kwa mara Waziri wa Kilimo amelisemea ni kuibadilisha sekta nzima, ili itoke kwenye ubahatinasibu kwenda kwenye uhakika. Na sehemu ya kwanza ambayo Mheshimiwa Waziri wa kilimo ameweke mkazo, kama ambavyo Mheshimiwa Rais ameelekeza nguvu ieletekezwe, ni kuanzia na mbegu bora zenyewe. Kwamba, mtu anapokopa halafu akaenda kuwekeza kwenye kilimo, halafu akatumia mbegu bora ana uhakika wa kupata kutokana na kile kilichowekezwa. Kwa maana hiyo sekta nzima ikibadilishwa ikawa sekta ya uhakika, mbegu bora, kilimo cha umwagiliaji, matumizi bora ya zana za kilimo pamoja na uhifadhi pamoja na masoko, ukiukamilisha ule mnyumburisho wote maana yake unamfanya yule aliyekopa akawekeza kwenye kilimo awe na uhakika wa kurejesha.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo utaratibu ule utakapokuwa umekamilika kwa kuanzia na hilo la mbegu bora pamoja na vingine ambavyo viko kwenye mpango wa sekta ya kilimo vitawezesha sekta hiyo iwe ya kutabirika na ya uhakika na hivyo, itawezesha mtu aweze kukopa. Na ikishakuwa ya uhakika hata benki zitakuwa na uhakika wa kukusanya kutokana na hiyo kwa hiyo, riba zitakuwa rafiki.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali kuiwezesha, kuiwekea nguvu; tutaendelea kuliangalia kwa sababu ni moja ya kipaumbele ambacho tunalenga ili kuweza kuwezesha uchumi wa viwanda, lakini pia kukuza kipato cha kila Mtanzania, ili tuweze kusonga mbele kiuchumi.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Catherine Magige, swalii la nyongeza, tafadhali.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, iliyokuwa benki ya *FDME*, sasa ni zaidi ya miaka minne tangu *BOT* waifunge. Wananchi wa Arusha na sehemu mbalimbali waliokuwa na akaunti katika benki hiyo hadi leo hawajui hatima ya pesa zao. Nini kauli ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri. Na mara zote amekuwa kinara wa kuwatetea wananchi wa Tanzania, hasa wa Arusha, nadhani ndio maana huwa wanamchagua mara kwa mara:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuwepo na zoezi hilo la kuichukua iliyokuwa benki ya *FDME* na kilichochelewesha ni ule utaratibu ambao ni wa kawaida unapoikabiodhi kwa mufilisi kwa hatua zile. Kwamba, unatoa kile cha kwanza ambacho kiko kisheria kwa wale ambao walikuwa na akiba zisizozidi kiwango kilichowekwa kisheria, lakini kwa wale ambao viwango vyao vilikuwa zaidi ya kiwango kinachogawanya kwa awamu ya kwanza huwa ni lazima zoezi la mufilisi likamilike kwanza.

Mheshimiwa Spika, na zoezi hilo linahusu uhakiki wa mali zote zilizopo zikusanywe, ziuzwe, halafu zikishauzwa zikageuzwa kuwa fedha ndio watu wale waweze kugawanya, wale ambao akiba zao zilikuwa zinazidi kiwango cha kwanza ambacho kilikuwa kimegawanya. Sasa kwa kuwa zoezi hilo kukamilika linachukua muda, kuhakiki mali uzipate zote, lakini pia uzibadilishe ziwe fedha linachukua muda, hicho ndicho ambacho kimechelewesha.

Mheshimiwa Spika, sasa ni lini itakamilika?

Mheshimiwa Spika, nakumbuka utaratibu huu ulikuwa bado unaendelea na ulikuwa hatuia nzuri. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge tutakapokuwa tumemaliza zoezi lako la hapa Bungeni nitapata taarifa ambapo imeshafikia hatua gani ili niweze kujua ni lini watakuwa wameshakamilisha kwasababu, zoezi lilikuwa linaendelea.

**SPIKA:** Tuendelee na Wizara ya Elimu, sayansi na Teknolojia. Swali la Mheshimiwa Mbunge wa Ludewa.

Na. 119

**Kukamilisha Ujenzi wa Chuo Cha VETA  
Shaurimoyo – Ludewa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha Ujenzi wa Chuo cha VETA Shaurimoyo – Ludewa ili kuzalisha Wataalam watakaosaidia kutekeleza mradi wa Liganga na Mchuchuma utakapoanza?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Omar Kipanga, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Njombe kinachojengwa katika Wilaya ya Ludewa ni mionganini mwa vyuo viliwyokuwa vinajengwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuititia mradi wa kuimarisha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu (*STVET – TE*). Mradi huu ulikuwa unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) ambapo mkataba kati ya Serikali na Benki hiyo uliisha muda wake tarehe 31 Desemba, 2019, kabla mradi haujakamiliaka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kukamilika kwa mradi huu, utekelezaji wa mradi huu utaendelea kuititia Mradi wa Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi (*ESPJ*) kwa utaratibu wa “*Force account*”. Tathmini ya gharama imeshafanyika ambapo jumla ya shilingi 4,342,678,784.32 zitatumika katika kukamilisha ujenzi huu.

Ujenzi wa Chuo hiki unatarajiwa kuanza tena katika Mwaka wa Fedha 2020/2021. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga, swalii la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ina uhaba mkubwa wa walimu kwenye shule zake za msingi, jambo linalosababisha wazazi kuchangishwa kati ya 15,000 mpaka 20,000 kwa ajili ya kuajiri walimu wa kujitolea kwenye Kata ya Mlangali, Mavanga na Lugarawa. Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa kutosha kwenye shule za msingi za Wilaya ya Ludewa ikiwa ni pamoja na kuwaajiri wale walimu waliojitlea kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, shule 23 za sekondari zilizopo Jimboni Ludewa hazijafanyiwa ukaguzi muda mrefu. Je, ni lini Wizara itatoa maelekezo kwa wadhibiti ubora wa elimu walioko pale Ludewa waweze kufanya ukaguzi huo kuliko kuendelea kusubiri wakaguzi kutoka kanda? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Juma Omar Kipanga tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna changamoto ya uhaba wa walimu katika maeneo mbalimbali nchini. Na kama mnavyofahamu hivi punde tu Mheshimiwa Rais aliagiza kwamba, wale walimu 6,000 ambaao wa kuziba nafasi utaratibu wake uweze kufanyakia mapema. Lakini kama mnavyofahamu mwaka jana mwezi wa Novemba Serikali ilitoa kibali cha kuajiri walimu zaidi ya 13,000. Tunaamini kati ya wale 13,000 walimu karibu elfu nane walikuwa tayari wameshasambazwa shulenii na walimu 5,000 walikuwa wanaendelea na mchakato.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika magawanyo huu sasa na hawa 6,000 watakaopatikana hivi punde watakwenda kutatua tatizo lille la upungufu wa walimu katika Halmashauri zetu ikiwemo na Halmashauri au Wilaya ya Ludewa.

Mheshimiwa Spika, hili la wazazi kuchangishwa, naomba tulibebe. Tutashirikana na wenzetu wa TAMISEMI tuweze kuangalia namna gani jambo hii linaweza likachukuliwa hatua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili amezungumzia suala la ukaguzi wa shule, Wizara inaendelea na kuimarisha Kitengo hiki cha Wadhibiti Ubora, ambapo hatua tofauti zimeweza kuchukuliwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2018/2019 mpaka hii 2020/2021. Wizara imeweza kufanya mambo yafuatayo; kwanza, tumeweza kusambaza Wadhibiti Ubora 400 katika Halmashauri zote nchini.

Pia katika kipindi cha mwaka 2018/2019 hadi 2020/2021 jumla ya ofisi za Wadhibiti Ubora 100 katika Halmashauri zetu zimeweza kujengwa na mpaka hivi navyozungumza tunaendelea na ujenzi wa ofisi 55 na ukarabati wa ofisi 31. Sambamba na hilo, Wizara yangu tumeweza kununua na kusambaza magari 83 kwenye Halmashauri tofauti tofauti.

Mheshimiwa Spika, lengo la kufanya hayo yote ni ili kuimarisha Kitengo chetu hiki cha Udhibiti Ubora hasa katika Halmashauri zetu. Kwa kufanya hivyo, tunaamini kutokana na ongezeko la shule nydingi ambazo zinahitaji kukaguliwa za msingi na sekondari tutaweza sasa kuzifikia shule hizo kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sasa Wadhibiti wetu wa Ubora hawa wa Wilaya watakwenda kufanya ukaguzi katika shule hizi za msingi na sekondari katika maeneo waliopo badala ya kutumia wale Wadhibiti Ubora wa Kanda ambao walikuwa wanakagua hizi shule katika kipindi kilichopita. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Dkt. Chaya nilikuona, uliza swali la nyongeza, tafadhalii.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Hitaji ya chuo cha *VETA* katika Jimbo la Ludewa linafanana sana na hitaji ya chuo cha *VETA* katika Jimbo la Manyoni Mashariki.

Je, ni lini sasa Serikali itakuja na mpango wa kuhakikisha kwamba Jimbo la Manyoni Mashariki hususan Wilaya ya Manyoni inakwenda kujengewa chuo cha *VETA*? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu wa swali hilo Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, lini *VETA* Manyoni.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mbunge wa Manyoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimeeleza mara kadhaa katika Bunge lako hili Tukufu kwamba hivi sasa Serikali inaendelea na ujenzi wa vyuo 29 katika Halmashauri mbalimbali nchini, ambapo jumla ya shilingi bilioni 48.6 zimeweza kutengwa na zinaendelea kutumika kwa ajili ya ujenzi huo. Serikali inaendelea na utaratibu wa kutafuta fedha kwa sababu lengo kuu ni kuhakikisha kwamba katika kila Wilaya na Mkoa tunakuwa na *VETA*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge mara tu fedha zitakapopatikana tutahakikisha kwamba tunakwenda kujenga *VETA* katika Halmashauri ya Manyoni lakini na Halmashauri zote ambazo bado hazijafikiwa na *VETA* nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sillo Daniel Baran uliza swali lako kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Na. 120

**Ujenzi wa Barabara ya Dareda – Bashnet – Dongobesh**

**MHE. SILLO D. BARAN** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Dareda – Bashnet – Dongobesh kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Majibu wa swali hilo Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe*, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dareda – Bashnet hadi Dongobesh yenyeye urefu wa kilometra 54 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania-*TANROADS* ambapo kilometra 10 zimejengwa kwa kiwango cha lami na kilometra 44 ni za changarawe. Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) imekamilisha kazi ya upembuzi yakini na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Dareda – Bashnet hadi Dongobeshi kwa kiwango cha lami. Kazi hii ilifanywa na Mhandisi Mshauri *Luptan Consults Ltd* kwa kushirikiana na Mhandisi *Consultancy Ltd* kwa gharama ya shilingi milioni 398. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, wakati ujenzi kwa kiwango cha lami ukisubiri upatikanaji wa fedha, Wizara yangu kupitia *TANROADS* inaendelea kuifanya matengenezo mbalimbali barabara hii ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi milioni 513.594

zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti uliza swali lako.

**MHE. SILLO D. BARAN** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini pamoja na majibu hayo nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umeshakamilika, je, ujenzi wa barabara hii unaweza ukaanza kwenye bajeti ijayo ya mwaka 2021/2022? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pilli, kwa kuwa barabara hii inafanana na barabara ya Magugu kwenda Mbuyu wa Ujerumani kuititia Daraja la Magara ambalo limejengwa na Serikali kwa thamani ya shilingi bilioni 13 hadi Mbulu; je, Serikali ipo tayari kuanza ujenzi wa barabara hii pia ili kuchochea maendeleo katika eneo hilo? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, *Engineer Msongwe* majibu tafadhalii ya maswali hayo ya Mheshimiwa Baran.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sillo Baran, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dareda hadi Dongobesh yenyeye urefu wa kilometra 54 kwenye maeneo ya *escarpment* ambayo tulijua yana changamoto yameshajengwa kilometra 10. Pia tumekamilisha usanifu wa kina mwaka huu, kwa hiyo, tusubiri bajeti; siwezi nikasema sasa hivi lakini nadhani litajitokeza kwenye bajeti lakini kwa maana ya kukamilisha usanifu wa kina maana yake tuna mpango wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami na hiyo tu ni hatua za kuelekea huko.

Mheshimiwa Spika, ameuliza barabara inayoanza Mbuyu wa Mjerumani hadi Daraja la Magara. Barabara hii pia ipo kwenye mpango na itakamilika kufanyiwa usanifu wa kina Septemba mwaka huu. Kwa hiyo, tayari pia ipo kwenye mpango kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kuanzia Mombo - Soni - Lushoto ni nyembamba mno na husababisha usumbufu mkubwa sana kwa watumiaji wa barabara hiyo hasa katika kipindi hiki cha mvua.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua barabara hiyo ya Mombo - Soni - Lushoto? (*Makof*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Shekilidi, Mbunge maarufu kabisa ndani ya mjengo huu, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali. (*Makof/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara ya Mombo - Lushoto ni nyembamba. Nimhakikishie Mheshimiwa Shekilindi barabara hii itakapoingia kwenye mpango wa kuikarabati upya na ujenzi mpya tutaiangalia; ndio maana kunakuwa na usanifu mpya. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii itakapoingizwa kwenye mpango wa kujenga upya itafanyiwa *Design* upya na itapanuliwa ili kuweza kuingia kwenye viwango vya sasa vya barabara za mita saba na nusu kama zilivyo barabara nyingine. Ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kama unavyojuu changamoto ya barabara mikoani ni kubwa na kwa Mkoa wa Mara katika miaka zaidi ya mitatu, minne *TANROADS* Mkoa wa Mara imekuwa haipewi fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa barabara. Sasa tunauliza ni lini Serikali itapeleka fedha za kutosha *TANROADS* Mkoa wa Mara ili iweze kukarabati barabara zote za Majimbo 10 ya Mkoa wa Mara ikiwepo Bunda Mjini; barabara ya kutokea Sazira – Nyamswa; barabara ya kutoka Kinyambwiga kuja Rwagu kutokea Ng'ombe mpaka Manyamanyama? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mgao wa fedha za *TANROADS*, fedha zinagawiwa sawa na hakuna upendeleo unaofanyika na Serikali kwenye barabara zake zote za Mikoa mbalimbali. Nataka tu nimjulishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna miradi kadhaa kwa kiwango cha lami ambayo mpaka sasa hivi inatekelezwa katika Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mbunge kwamba tunatoa fedha kwa usawa na hasa kwa miradi ambayo inatekelezwa na yeye ni shahidi zipo barabara za Nyamuswa, Bunda zinajengwa. Kwa hiyo, hatuwezi tukakamilisha miradi yote kwa wakati mmoja, lakini ni mpango wa Serikali kwamba barabara zote ambazo zimeainishwa kwenye llani na zimeahidiwa na viongozi zitajengwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa tuhamie Wizara ya Viwanda na Biashara, swali litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

Na. 121

**Wahitimu wa Shahada ya *Science, Industrial Engineering Management***

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali inawatumia vipi wanafunzi wanaohitimu Shahada ya *Science in Industrial Engineering Management* katika Uchumi huu wa kati wa Viwanda?

(b) Je, ni wanafunzi wangapi waliohitimu katika fani hiyo wameajiriwa Serikalini tangu mwaka 2019 hadi 2020?

**SPIKA:** Majibu wa swali hilo Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Shahada ya Sayansi katika Menejimenti ya Uhandisi wa Viwanda (*Bachelor of Science in Industrial Engineering Management*), ilianzishwa mwaka 2015/2016 katika Chuo Kikuu cha Mzumbe. Shahada hiyo ilianzishwa ikilenga kuzalisha wataalam wa kusimamia shughuli za uzalishaji katika viwanda ambavyo vinamilikiwa na Serikali na vile vya mashirika na makampuni binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2017/2018 mpaka 2019/2020, wahitimu wengi katika fani hiyo wameajiriwa katika sekta binafsi hususan katika viwanda vya kuzalisha bidhaa kama vile viwanda vya saruji, vinywaji, nguo,

sukari, vyakula, mbao, vifungashio, mafuta na kadhalika na katika uchimbaji wa madini. Pia, wahitimu hao wameajiriwa katika taasisi za Serikali zinazoshughulikia masuala ya ubora kwa mfano Shirika la Viwango Tanzania - *TBS*, Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda-*TIRDO*, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Taasisi ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo -*TEMDO*, huduma za viwanda vidogo Vidogo-*SIDO* na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali yetu inatekeleza azma ya ujenzi wa viwanda, yaani uchumi unaoongozwa na viwanda, wahitimu katika fani hiyo walioajiriwa wanatumika katika usimamizi wa shughuli mbalimbali za viwanda vilivyopo katika sekta ya umma na sekta binafsi na hivyo kuleta tija katika uzalishaji na uendeshaji wa taasisi za umma na za binafsi.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2017/2018 mpaka 2019/2020 jumla ya wahitimu wa shahada hiyo walikuwa 228. Kati ya hao, wahitimu 55 walipata ajira. Aidha, kati ya hao 55 waliopata ajira, katika mashirika na taasisi za Serikali ni wahitimu saba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Viwanda. Tunazungumzia uchumi wa kati ikiwemo kuondeleza viwanda vyetu, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, ni nini mpango wa Serikali katika kuongeza viwanda vingi ili hawa vijana wanaohitimu mafunzo haya waweze kupata ajira kwa sababu naona ni vijana saba tu ambao wameajiriwa na Serikali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, ni nini mpango mkakati wa Serikali kufufua viwanda vyote ambavyo vilijengwa enzi za Mwalimu ili hawa vijana wetu akribani 228

waliohitimu mafunzo haya ambao hawajapata ajira waweze kuajiriwa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu wa maswali hayo Naibu Waziri Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Silaoneka, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Tanzania tupo katika mkakati wa kuwa na uchumi unaoendeshwa na viwanda na hasa tukiwa sasa tumefika katika uchumi wa katii. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha tunaongeza viwanda vingi kwa kuhamasisha sekta binafsi kuititia kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya wadau wa viwanda kuwekeza katika viwanda vingi ambavyo hatimaye vinatumia vijana wetu wanaohitimu katika vyuo vingi ambavyo vinatoa elimu hususan inayolenga katika kuongeza ubora wa bidhaa zetu zinazozalishwa katika viwanda lakini pia lengo ni kuona sasa tunakuwa na viwanda ambavyo vitakuwa vinapata wataalam walio na utaalam mahsusii katika mahitaji wa viwanda hivyo.

Kwa hiyo, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi lakini pia mashirika na watu mbalimbali na wawekezaji kutoka nje ambao wanaweza kuwekeza katika viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili ni kweli viwanda vingi vilivyokuwa vimejengwa wakati wa enzi za Nyerere lakini pia viwanda vingi ambavyo vilikuwa vimebinafishwa havifanyi kazi. Serikali ina mkakati maalum kwanza kuititia viwanda vyote ambavyo havifanyi kazi, lakini hasa vile ambavyo vilikuwa vimebinafishwa kwa watu ambao hawaviendeze ili tuweze kuvifufua. Lengo ni kuona sekta ya viwanda inaendelea lakini wa kutumia miundombinu ya viwanda iliyokuwepo hapo kabla ili viweze sasa kuchukua wataalam wengi ambao wanasona katika vyuo vyetu vingi ili waweze kuajiriwa katika viwanda hivyo.

**SPIKA:** Tunaendelea na Katiba na Sheria, Mheshimiwa Taska Mbogo uliza swali lako.

Na. 122

**Hitaji la Court Reporter na Stenographer Mahakamani**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itasomesha wataalam wa *Court Reporter* na *Stenographer* ili Mahakama zetu ziwe na wataalam hao?

**SPIKA:** Majibu wa swali hilo, Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Katavi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa haina mpango wa kusomesha wataalamu waandishi wa *Stenographer* (*Stenographer na Court Reporters*) ambao hufanya kazi za uandishi wa maelezo ya mijadala ya wakati wa uendeshaji wa kesi Mahakamani. Kazi hizo kwa sasa zinafanywa na Waheshimiwa Majaji na Waheshimiwa Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuangalia utaratibu mzuri wa kuwatumia wataalamu hawa ambao kwa sasa hawapo katika Muundo wa Utumishi wa Mahakama. Baada ya kukamilika kwa utaratibu unaoangaliwa na kuingizwa kwenye Muundo wa Utumishi wa Mahakama, Wizara itaandaa mpango wa mafunzo kwa wataalamu hao kuanza kuwasomesha rasmi tayari kwa kuanza kuwatumia kwenye Mahakama zetu hapa nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Taska Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali haina mpango wa kusomesha *Stenographer* nchini Tanzania; na kwa kuwa kazi hizi zimekuwa zikifanywa na Majaji na Mahakimu wenye; swali langu kwa Serikali: Je, Serikali haioni kwamba inawaongeza mzigo Majaji na Mahakimu wasome, watoe hukumu na pia wanachukua jukumu la kuandika? (*Makofii*)

Swali la pili, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi sana nchini Tanzania kwamba baada ya hukumu unakuta mwananchi inamchukua muda, hata mwezi mmoja kupata ile hukumu yake; hii yote ni kwa sababu hatuna *stenographer* mle Mahakamani: Je, Serikali haioni kwamba inawakosesha wananchi haki yao ya kupata hukumu zao mara tu kesi inapohukumiwa? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza Mheshimiwa anasema Waheshimiwa Mahakimu na Majaji wanakuwa na mzigo mkubwa sana wakati wanasiliza kesi na wakati huo huo wanachukua uandishi, ni kweli lakini katika mazingira ya kawaida Serikali kama nilivyoeleza mwanzo kwenye jibu langu la msingi, ni kwamba hawa watu hawajaingizwa kwenye mfumo wa utumishi wa Mahakama. Kwa maana hiyo, Serikali inapitia utaratibu mzuri utakaowezesha hawa watu, kwa sababu itakuja kama idara mpya kama zilivyo idara nydingine za kiutendaji kwenye Serikali hii. Utaratibu wa kuanzisha idara mpya una milolongo yake katika kuangalia masuala mbalimbali. Tunajua wazi kwamba ni mzigo, ni kweli, ndio maana Serikali imeendelea kuupitia mchakato wa kuanzisha section hii Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kwa hukumu siyo kwa sababu tu hatuna hawa watu, hili ni jambo ambalo lina mambo mbalimbali ambayo yanajitokeza pale

Mahakamani. Nikuhakikishie tu kwamba sasa hukumu hazichelewi zaidi ya mwezi mmoja. Tumeendelea kukaa na Mahakimu na kuona uharakishaji wa utoaji wa hukumu zao.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa hivi tunaelekea kwenye Mahakama ya Kiswahili, kwa hiyo, vitu vingi vitarahisishwa baada ya muda siyo mrefu na mambo yote yatacaa sawa. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo kwa linalekezwa kwa Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Mohamed Juma Soud, Mbunge wa Donge, tafadhalii.

Na. 123

**Kuiwezesha Mifuko ya Kuendeleza Utalii na  
Wanyamapori Nchini**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuiwezesha Mifuko ya Kuendeleza Utalii na Wanyamapori na kufikia lengo la watalii milioni tano ifikapo 2025?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mary Francis Masanja.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Tozo ya Maendeleo ya Utalii (*TDL*) ulianzishwa kwa Sheria ya Utalii Na. 29 ya Mwaka 2008, Kifungu cha 59(2). Lengo la Tozo hiyo ni kuendeleza mazao ya utalii; kudhibiti ubora wa huduma za biashara za utalii; kukuza na kutangaza vivutio vya utalii; kujenga uwezo katika sekta ya utalii; na kuwezesha tafiti na shughuli nyingine yoyote kwa ajili ya maendeleo na kuboresha sekta ya utalii.

Kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020, vyanzo vya tozo hii kwa sasa vinakusanywa na Wizara kwa kushirikiana na *TRA* na makusanyo hayo huingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wanyamapori, upo Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania ambao ulianzishwa kwa Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Sura 283, Kifungu cha 91(2). Mfuko huo unawezesha shughuli za kuhifadhi wanyamapori ndani na nje ya maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wanyamapori wanaendelea kulindwa na kusimamiwa kwa ajili ya kuendeleza utalii nchini, mifuko ya utalii na wanyamapori imekuwa ikiwezeshwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Pamoja na vyanzo vya mapato vya mifuko hii kukusanywa na kupelekwa kwenye Mfuko Mkuu (Hazina), Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imetenga fedha kupitia bajeti kuu ya Serikali kwa ajili ya kutekeleza kazi za mifuko husika. Hivyo, kazi zilizokuwa zinafanywa na mifuko hii sasa zitatekelezwa kupitia bajeti kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma, Mbunge wa Donge, swalilisha la nyongeza.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Kama unavyokumbuka kwamba mifuko hii imeweza kuchangia maendeleo makubwa katika masuala ya uhifadhi, hususan kupunguza wimbi la ujangili nchini pamoja na kuongeza wigo wa masuala mazima ya miradi ya wanajamii, halikadhalika kuingiza vivutio ambavyo vimetu pelekea kufikia lengo la watalii 1,300,000: Je, kutokana na mabadiliko ya sheria hii, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba mabadiliko haya hayaendi kudumaza maendeleo ambayo yamefikiwa katika matumizi ya mifuko inayoathirika kutokana na sheria hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kama tunavyofahamu, mwezi wa Pili mwaka huu Mheshimiwa Waziri Mkuu alifungua maonyesho ya mifuko pale Arusha na alitoa wito wa kwamba mifuko hii iweze kuendelezwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Je, tuna mpango gani mbadala wa kusaidia mifuko hii ili pamoa na mabadiliko haya ya sheria ambayo yamefanyika kuhakikisha kwamba yanakwenda kusaidia mafanikio ambayo yamepatikana hasa tukilinganisha kwamba hivi sasa wenzenzu wa *CMA* wameanza kulalamika kutokana na matatizo ya...?

**SPIKA:** Ahsante sana. Umeshaeleweka Mheshimiwa.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. kwanza nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Soud, lakini nimtoe wasiwasi kwamba Serikali iliona suala hili baada ya mifuko hii fedha zake zilizokuwa zinakusanywa kupelekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, Serikali ilianza kutekeleza majukumu yake yaliyokuwa yanatekelezwa kwenye mfuko huu kupitia bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimtoe wasiwasi kwamba shughuli sasa ambazo zilikuwa zinatekelezwa na mfuko huu ikiwemo uhifadhi, kudhibiti ujangili na shughuli nyingine za kuendeleza utalii, kukuza na kutangaza utalii, Shughuli zote hizi sasa zinatekelezwa na bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 shughuli zote zilizokuwa zinatekelezwa kwenye mifuko hii, sasa zimeingizwa kwenye bajeti kuu ya Serikali. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape Nnauye, nimekuona.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na kumwalika Naibu Waziri aje kutembelea msitu wa hifadhi wa Rondo, maeneo ya Tarafa ya Rondo, Rutamba, Milola na Kiawa yamekuwa yakiathiriwa sana na Wanyamapori hasa tembo; na kwa kuwa idadi ya askari wanaohusika na ulinzi wa eneo hili ni kidogo.

Je, Serikali iko tayari kutoa mafunzo na kuwawezesha vijana wa maeneo haya washirikiane na wale askari katika kusaidia kulinda mali na Maisha ya wananchi wa eneo hili?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kwa kifupi Naibu Waziri Mheshimiwa Mary Francis Masanja.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kweli kumekuwa na matukio mbalimbali ya uvamizi wa tembo. Hii tukumbuke tu kwamba tunaishi maeneo mengi ambayo kihistoria ilikuwa ni mapito ya Wanyamapori wakiwemo tembo. Wizara kwa mara nyingi imekuwa ikipata hizi taarifa na kutoa ushirikiano kwa wananchi ikiwemo kupeleka maaskari kuwaondoa hao tembo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kushirikiana na vijana wakiwemo kwenye maeneo husika hasa kuanzisha WMA ambazo huwa zinashirikiana na Wizara katika kuhakikisha kwamba zinatunza maeneo husika lakini pia tunashirikiana kudhibiti hawa Wanyama wakali. Hivyo niko tayari kuongozana na Mheshiniwa Nape Nauye kwenye Jimbo lake kuhakikisha kwamba suala hili tunali-solve kwa Pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la mwisho kabisa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Miaka 20 iliopita ndani ya Jimbo la

Momba Ivuna, kuna kimondo kidogo kilidondoka (*Ivuna Meteorite*) na kikachukuliwa na watu wa NASA. Je, Serikali ina mpango gani wa kufuatilia kimondo hiki kwa ajili ya kukirudisha na kuendelea kuongeza idadi ya watalii nchini? (*Makofi*)

**SPIKA:** Sina hakika kama Naibu Waziri ana taarifa hizo. Waziri mwenyewe, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro tafadhali.

**WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nampongeza kwanza Mheshimiwa Condester kwa kazi nzuri anayowafanya wananchi wa Mombasa na ndiyo maana walikuchagua kwa kura nydingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imeshaanza kufanya mawasiliano na Balozi wetu aliyeo nchini Marekani kuanza kufuatilia jambo hili. Tutakapopata majibu, tutamjulisha Mheshimiwa Condester na Bunge lako Tukufu. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Tukubaliane maswali yaishie hapo.

Wageni waliopo jukwaa la Spika ninaanza na wageni 30 ambao ni wageni wa Spika mwenyewe, nao ni viongozi wakuu pamoja na wachezaji wa *Azam Sports Club* kutoka Jijini Dar es Salaam. *Azam Sports Club!* Makofi hayatoshi hayo jamani. Ahsante sana. (*Makofi*)

Ahsanteni sana Azam na karibuni sana hapa Bungeni Dodoma. Mnacheza mpira mzuri, mwendelee kuboresha kabisa, tunawategemea. Hata Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake ya Namungo inawatambua. Kwa hiyo, karibuni sana Dodoma, watakuwa na mechis hapa, hebu tuifuatilie na tuhudhurie Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Wako wageni wanne wa Naibu Spika, Mheshimiwa Tulia Ackson na Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo ambao ni kutoka Chama cha Waigizaji Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na

Mwenyekiti wao Ndugu Leornard Mwinuka. Ahsanteni sana. Hawa ni waigizaji, sikupata majina yao vizuri, lakini wanatoka Chama cha Waigizaji. Ni wasanii hao. (*Makof*)

Kwa upande wa wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri wa Maliasili na Utalii na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja ambao ni wadau wa utalii, yaani wawakilishi wa vyombo vya Habari kutoka Kanda ya Ziwa Jijini Mwanza wakiongozwa na Ndugu Charles Mseti. Wale wa Mwanza, karibuni sana. (*Makof*)

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Pauline Gekul, Naibu Waziri wa Habari Utamaduni Sanaa na Michezo ambao ni watumishi wa *United Bank of Africa (UBA)* kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Joseph Mnembuka. Karibuni sana *UBA*.

Wageni 28 wa Wabunge wa Mkoa wa Mbeya ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Mbeya wakiongozwa na mlezi wao, ndugu Bahati Mapasa. Karibuni sana kutoka Mbeya. (*Makof*)

Wageni 13 wa Mheshimiwa Shally Raymond, ambao ni kikundi cha sala kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Charles Kidiru. Karibuni sana. (*Makof*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Hamisi Taletale, nimeambiwa ni Madiwani 16 wa kutoka Morogoro. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Hamisi Taletale wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri, Mheshimiwa Lucas Lemomo. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. Leo ni bajeti ya TAMISEMI, kwa hiyo, msiondoke hapo leo, msikilize mpaka jioni. Ahsante sana.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Maida Abdallah ambao ni Watendaji Wakuu wa Kampuni ya *Wonderland Africa Tour Agency* kutoka Jijini Dar es Salaam akiwemo Mkurugenzi Mtendaji, Ndugu Saidi Rukemo na Mbunifu Ndugu Mustapha Rukemo. Karibuni sana, wale pale. (*Makof*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Luhaga Mpina ambaao ni wapiga kura wake kutoka Kisesa Wilayani Meatu Mkoani Simiyu wakiongozwa na Ndugu Donald Masunga. Karibu sana Masunga. (*Makof*)

Matangazo mengine; Ndugu Hussein Nassor Amar, Mwenyekiti wa Waislamu Bungeni ananiomba niwatangazieni Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Umoja wa Wabunge Waislamu, mkutane katika kikao kitakachofanyika leo mchana saa 7.00 ukumbi 229. Kamati ya Uongozi wa Wabunge Waislamu, ukumbi 229 saa 7.00 mchana.

Mheshimiwa Humphrey Polepole, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, anaomba niwatangazieni Wajumbe wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, mkutane mara baada ya kipindi cha maswali katika ukumbi wa Msekwa D. Mkutane mara baada ya matangazo haya.

Mheshimiwa Shally Raymond, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wakatoliki, anawatangazieni Waheshimiwa Wabunge wote, wanajumuia na wageni wote kuwa leo kutakuwepo na ibada ya Misa Takatifu itakayoanza saa 7.00 mchana katika Kanisa la Bunge *Chapel* mara tu baada ya kusitisha shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anaomba niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge kuwa uongozi wa *Bunge Sports Club* umeandaa fomu maalum za kuwaomba wanamichezo wote kujiorodhesha na kuainisha aina ya michezo mnayopendelea kushiriki ili waweze kuandaa utaratibu mzuri zaidi wa mazoezi pamoa na vifaa husika.

Kwa hiyo, mjiandae ili muweze kupata vifaa husika na hasa wale wa Kuvuta Kamba, maana yake wale wana vifaa vyao maalum. Wana buti zao fulani, wanahitaji *gloves* na lishe maalum. Kwa hiyo, mjiandikishe Waheshimiwa. (*Makof*)

Ninao mwaliko kwenu Waheshimiwa Wabunge kutoka Kanisa la Mlima wa Moto *Assemblies of God* Dar es Salaam kutoka kwa *Bishop* Rose Joseph Mgeta, anasema Jumapili ijayo tarehe 25, itakuwa ni kumbukumbu ya mwaka mmoja toka, Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatare kufariki mwaka jana nyakati kama hizi. Kwa hiyo, tarehe 25, kutakuwa na misa ya kumbukumbu kwa Waheshimiwa Wabunge ambao mtakuwa Dar es Salaam, basi mnaombwa kushirikiana pamoja na waumini wa Kanisa hilo la Mlima wa Moto katika ibada ya kumwombea Mheshimiwa Getrude Rwakatare. (*Makofisi*)

Baada ya hayo, moja kwa moja tuingie kwenye uchangiaji Waheshimiwa Wabunge, lakini jinsi mlivyo wengi tutajaribu dakika tano tano, kama nilivyowaambia *day one* ilikuwa ni hivyo hivyo, hata katika bajeti zinazofuata jiandikishe siku ile ambayo bajeti inaanza, usisubiri wenzako wasemee ndiyo na wewe upate wazo la kusema unachelewa. Ukiijandikisha mapema unapata dakika za kutosha, ukija na wazo mwishoni basi hivyo hivyo maana orodha ni ndefu na siyo wote mtapata nafasi. Kwa hiyo, tuvumiliane dakika tano nenda moja kwa moja kwenye suala zima ili Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aweze kukupata na kuelewa unaongelea kitu gani. Katibu

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, Mheshimiwa Thea Medard Ntara, dakika tano. Kama nilivyosema, anza moja kwa moja, acha shukurani, acha nini, unafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Msingi wa kujenga uchumi wa viwanda ni kuwa na *technical schools* au *colleges*, niipongeze Serikali kwa kuboresha baadhi ya vyuo hivyo, yaani sekondari za ufundi chache katika nchi hii, angalau wameboresha majengo. Sasa niombe licha ya kuboresha majengo hayo, waboreshe na vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji, kwa sababu, majengo tu hayatasaidia.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanajua kwamba zile shule zilikuwa zinasikika sana; Ifunda, Iyunga, Mtwara, Moshi *Technical*, hizi sekondari sasa hivi hazisikiki kwa sababu ubora umepungua. Kwa hiyo, niwaombe sana Serikali waziangalie, majengo pamoja na vifaa vya ufundishaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia katika ufundishaji waboreshe kwa kutumia Taasisi ya Elimu ili waweze kuwapa mafunzo wale Walimu ya ufundishaji mahiri, tunaita *competent base*, tumeizungumza sana hiyo toka 2005, lakini ni *practice bado* Walimu wanafundisha kwa kuwajaza wanafunzi maarifa, wanawajaza, wanawajaza, lakini *practical skills* zimebekwe pembeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nirudi kwa watendaji. Ni kweli kuna baadhi ya watendaji wetu wanatuangusha, lakini kuna baadhi ya Wakurugenzi wanafanya kazi vizuri, wakati wote tunaangalia wale wanaofanya vibaya, lakini wapo wazuri. Hivyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, wapewe pongezi zao, wapewe *recognition*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna Mkurugenzi alikuwa anafanya kazi pale Jiji, nitoe mfano, wakati anakuja pale, maegesho tu walikuwa wanapata milioni 84 kwa mwezi, lakini alipoingia yeye akakusanya bilioni 1.6 kwa mwezi. Wakurugenzi kama hao naomba wapewe *recognition*, *Maslow's hierarchy* inasema binadamu siyo fedha tu, binadamu siyo mapenzi tu, binadamu siyo shughuli nyingine,

binadamu hata kule kutambuliwa anaweza akafurahi zaidi.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa stendi ya Mbezi huyo Mkurugenzi aliweza kuokoa bilioni zaidi ya 12. Hizo zinge pigwa, kwa hiyo, hapa nimesimama kuzungumzia kwamba Wakurugenzi wengine ni kweli siyo mahiri, lakini kuna wale wazuri tuwatambue na wapewe *recognition*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumze kwa watumishi; tunapozungumza ni watumishi na wengi zao ni Walimu, tunasema Walimu ndiyo wengi katika watumishi, kwa hiyo, tunapotetetea Walimu na mimi ni mwalimu, tunapotetetea siyo kwamba watumishi wengine tumewaa cha pembeni.

Mheshimiwa Spika, Walimu wanafanya kazi nydingi mno na sisi ni mashahidi, tukija uchaguzi Walimu, tukija kwenye sensa tunategemea Walimu, watoto wetu tumewaa cha mashulenii huko Walimu. Jana nilikuwa na Mheshimiwa mmoja akawa anasema jamani hawa Walimu wana kazi, sisi tuko huku watoto wako mashulenii huko. Kwa hiyo, tunapotetetea wapandishwe mishahara, ni kwa sababu ndiyo kundi kubwa na limeshasemwa siku nydingi, lakini bado walimu mishahara yao hairidhishi, licha ya matatizo yao mengi ambayo wanakuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Thea Medard Ntara, umetumia vizuri sana dakika zako tano na huo ni mfano kwa wengine wote watakaofuata.

Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, utafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kamonga.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na kwa sababu ya ufinyu wa

muda naomba niende moja kwa moja nizungumzie matatizo yaliyoko kwenye jumbo langu.

Mheshimiwa Spika, barabara ya King'ori inaanzia Malula kwenda King'ori kwenda Malulango, kwenda Leguluthi hadi Ngarenanyuki, sasa hivi iko kwenye hali mbaya sana sana na hivi karibuni nilipata picha kutoka jimboni ya hiyo barabara, nilikwenda kwa Waziri wa Ujenzi akaitizama, akaniambia ni kweli hii siyo barabara tena imekuwa shamba. Hii barabara nimeiongelea mara nyingi sana, lakini kwa bahati mbaya sana hata kwenye ilani haipo, hata kwenye mpango haipo.

Nilikwenda kumwona Waziri Mkuu tukazungumzia hilo jambo akaniambia niandike barua kwa Waziri wa Ujenzi nilianidika. Kwa hiyo, naomba sana TAMISEMI waikumbuke barabara hil, iingie kwenye mpango na itengenezwe haraka sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nilipata jibu la swalilangu namba 42 ambalo niliuliza TAMISEMI kwamba zilitengwa shilingi bilioni 1.259 kwa ajili ya kukarabati kwa kiwango cha changarawe ili ipitike mwaka mzima, lakini hizo fedha hazijapelekwa. Matokeo yake barabara ile imeharibika na haipitiki, wananchi wanateseka, wanashindwa kufuata mahitaji yao ya muhimu, wanashindwa kwenda kutafuta huduma zao za afya. Naomba sana, sana, hatua zichukuliwe. Hilo moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia napongeza Serikali imefanikiwa sana kuwafikia wananchi Mkoa wa Kilimanjaro. Mkoa wa Kilimanjaro ukitizama barabara zinatoka barabara kuu kwenda mlimani, barabara inayotoka Boma Ng'ombe kwenda Sanya Juu ni lami, barabara ya Kwa Sadala kwenda Masama ni lami. Ukienda barabara ya Machame kutoka Bashinituzi kwenda Machame ni lami, barabara ya Kibosho ni lami, *KCMC*kwenda Huru lami, *KCMC*kwenda Mweka lami, barabara ya Kawawa lami, barabara ya kwenda Marangu lami, barabara kwenda Mwika lami, hayo mafanikio, tunaomba wahamishe wapeleke Mlima Meru, Mlima Meru

Terei inafanana na Mlima Kilimanjaro wananchi wengi wako kwenye mteremko, kwa hiyo, barabara zile huwa zinaharibika sana kila mvua zikinyesha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hali ya hospitali ya wilaya ni mbaya, yale majengo yalijengwa miaka 60, tunaomba sana TAMISEMI watupie jicho pale, wakarabati yale majengo na watusaidie kumalizia *mortuary* ambayo tuliianza kwa nguvu za wananchi kufikia mahali na imebaki kidogo tu, kama tukipata fedha kidogo tutamalizia ile *mortuary*, tuweze kuwa na *mortuary* pale Arumeru Mashariki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tuna upungufu wa Vituo vya Afya; tuna upungufu wa vituo 19, tuna vituo saba tu wilaya nzima, tunaomba TAMISEMI iliangalie hilo na kutujengea vituo vya afya, najua wananchi wanaangaika kujenga vituo vya afya, lakini wanahitaji msaada. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuna Kituo cha Afya Momela, kilikuwa kinafanya kazi vizuri. Kwa bahati mbaya kwa sababu iliokea sintofahamu mwaka 2019, wale wa hisani *Africa Amini Alama* ikabidi waondolewe kukiendesha kile kituo. Baada ya hapo huduma zimedorora sana, hakuna mashine *X-Ray* na ile iliyopo hakuna wataalam wa kusoma. Tunaomba Serikali ifanye juhudhi iboreshe huduma za afya pale na kama ikiona ni shida sana, wale wahisani wako pale pale wanaendesha huduma za tiba mbadala, waitwe kile kituo kiendeshwe kwa mpango wa *PPP*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niyaseme hayo machache. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Dkt. Pallangyo. Nimeshakutaja Mheshimiwa Joseph Kamonga na Mheshimiwa Rweikiza atafuata.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na nianze kwa kumpongeza sana

Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho zuri na mpango mzuri.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo wananchi wa Jimbo la Ludewa wamenituma niombe mambo machache yaweze kufanyiwa kazi kwenye sekta ya barabara za vijiji na sekta ya afya. Kwa kuanzia na barabara za vijiji, mara zote tafiti zimekuwa zikiituonyesha kwamba wananchi wengi wa Tanzania wanaishi maeneo ya vijiji na tatizo kubwa ni umaskini ambao unawasumbua. Kwa hiyo, ningependa kumwomba Waziri wa mwenye dhamana Ofisi ya Rais, TAMISEMI aweze kuwaongeza fedha watu wa TARURA ili zile barabara za vijiji ziweze kuboreshwa. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, nina changamoto kubwa sana kule Jimboni kwangu Ludewa, kuna barabara inaanzia Lusitu inakwenda Madilu, Ilininda mpaka Mundindi; msimu huu wananchi wanatumia gharama kubwa sana kuweza kukodi bodaboda, barabara hazipitiki kabisa. Barabara hii hasa inayoanza Madilu mpaka Ilininda halijapata matengenezo kwa miaka zaidi ya nane. Wananchi wa Ludewa wamekuwa wakijitolea sana kuchimba hizi barabara kwa majembe ya mkono, lakini wanakatishwa tamaa baada ya kuona Serikali haiwaungi mkono kwa kutenga fedha na kufanya ukarabati wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, kuna eneo la Kigasi – Milo - Ludende mpaka Amani; barabara hii nayo ni muhimu sana, wananchi wa maeneo hayo ni wakulima, wana mazao mengi yanapaswa kupita kwenye barabara hii, lakini ina changamoto kubwa sana msimu wa mvua haiwezi kabisa kupitika. Mwaka huu nimelazimika mara kadhaa kwenda kushirikiana na wananchi kwa ajili ya kwenda kufanya matengenezo.

Kwa hiyo, wananchi wanajihisi kama Serikali imewaaacha, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri, naomba eneo hili liweze kuangaliwa na barabara hii ipewe fedha na kuweza kutengenezwa kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika wakati wote. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna ile Kijiji cha Masimavalafu, kuna Mto Ruhuhu ambapo panahitajika kivuko, ambako inakuwa ni rahisi sana wananchi kwenda Hospitali ya Peramiho kuweza kupata matibabu. Kwa hiyo katika eneo hili tungeomba hata kama kuna kivuko kimeachwa sehemu, tupewe sisi kitusaidie pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia na sekta ya afya; naomba sana hawa wananchi tunaowahamasisha waweze kuwa na hizi bima za afya, wanavyokwenda hospitali waweze kupata dawa na matibabu stahili yanayohitajika. Maana imekuwa ni changamoto kubwa sana, wataalam wanajitahidi kuwahamasisha wananchi wanakuwa na bima za afya lakini hawapati huduma kwa kiwango kile ambacho kinakubalika.

Kwa hiyo, naamini sana Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wote wawili wanaweza wakasimamia eneo hili tukaboresha ili wananchi waweze kuona kwamba Serikali inawathamini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, napenda kushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kamonga. Waheshimiwa Wabunge ratiba yetu ya kesho iko kama tulivyokwishatangaza, kwamba tuna ugeni mkubwa sana wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kesho Alhamisi, jioni na tutawatangazia vizuri zaidi huko mbele tunakoendelea, naomba sana kama jirani yako hayupo, hebu mpigie simu harudi haraka sana, yako mambo ambayo ni lazima Mbunge awepo yeye mwenyewe na tuna *take record* na *record* hizi huwezi kujua kesho wala kesho kutwa, si vizuri kutokuwepo katika *landmark speech* ya Rais wa Awamu ya Sita anapokuja kuhutubia Bunge hili. (*Makofii*)

Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, ambao hawapo sijui wako wapi, warudi wote, wawepo kesho, Wabunge wote mrudi muwepo kesho, ukumbi utakuwa umejaa kote, *gallery* zote *everywhere*, halafu ndani ya

ukumbi wa Bunge haiku hivyo, haitaeleweka. Kwa hiyo, kama jirani yako hayupo mpigie simu mwambie asafiri leo usiku kesho *everybody should be here*.

Mheshimiwa Jasson Rweikiza atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimba Abbas.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii. Kwanza napenda kuwapongeza sana Waziri, Mheshimiwa Ummey Mwalimu na Manaibu wake Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Festo kwa kazi nzuri ambayo wamekwisha kuifanya hadi sasa ambayo inaonekana.

Mheshimiwa Spika, nipende pia kuipongeza Serikali ya CCM kwa kazi kubwa inayofanyika kwenye maeneo yetu. Kazi zinaonekana, shule zinaonekana hata kama zina matatizo madogo madogo, vituo vya afya kwa maana ya hospitali, zahanati, hospitali za wilaya na vituo vya afya, barabara zinatunzwa, zinarekebishwa, tunasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo niseme kwamba tunahitaji kuongeza jitihada na kuboresha miundombinu tuliyonayo. Sasa niongelee jimbo langu, pale kwenye jimbo langu, kuna Kata moja inaitwa Lukoma, haina shule ya sekondari kwa hiyo, wanafunzi kutoka pale Lukoma wanatembea kilomita 19 kwenda shule jirani kutafuta elimu. Nasema jirani kwa sababu ndiyo inayofuata lakini siyo jirani kilomita 19 kwenda tu, kurudi 19, jumla 38 kwa siku moja mtoto mdogo wa *form one*, wa *form three* au kidato chochote, anatembea kilomita 19 kwenda, hivyo hivyo kurudi, kwa hiyo kwa siku anatembea kilomita 38 karibu 40, ambayo ni adha kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hii kata na yenye we iipatiwe shule, shule tulishajenga tayari pale, tumefika katikati hapo kwenye ukuta, lakini hatuna uwezo wa kumalizia, wananchi wamechanga wameishiwa nguvu, tunaomba Serikali itoe msaada unaotakiwa pale iki shule hii

ikamilike na hawa wananchi wapate shule ya kata, kama ilivyo sera ya CCM kila kata iwe na shule ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo zima la Bukoba Vijijini, hatuna shule ya *A level*, ya *form five* na *form six*, sasa hii nayo ingawa ngazi hii ni ya kitaifa, lakini ni vizuri tukawa na shule ya namna hiyo kusudi tuweze kupata huduma inayotokana na shule hiyo. Tuna shule za sekondari za *form one* hadi *form four* nyingi zaidi ya 30, lakini hatuna shule ngazi ya *form five* na *form six*. Kwa hiyo, wanafunzi wanapomaliza darasa la kumi na mbili hawawezi kusoma pale pale mpaka watafutiwe sehemu nyingine, nje ya mkoa au nje ya jimbo ambayo nayo inakuwa ni adha kubwa kwenda mballi.

Mheshimiwa Spika, nikiwa bado kwenye eneo la shule la elimu, tumejenga shule nyingi kwenye nchi hii, za kata za sekondari na zingine zillkuwepo, nyingi zimekuwa na matatizo kidogo kidogo ambayo yanababishwa huduma isiwe nzuri. Niongele sasa kwenye vyoo, shule nyingi hazina vyoo vizuri au havina vyoo kabisa, wanafunzi wanakwenda maporini hata Walimu na watumishi wengine wanakwenda kwenye maeneo ambayo siyo salama. Pale nina Shule moja inaitwa Kaishozi Sekondari, shule hii ni kubwa ni ya siku nyingi siyo ya kata, iko siku nyingi, lakini haina choo, choo kimeharibika siku nyingi na wanafunzi wanapata tabu sana inapofika kuwa na haja ya kwenda chooni.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na suala la *TARURA*; Wabunge wengi wamezungumzia suala la *TARURA*, *TARURA* imekuwa ni mkombozi mkubwa wa barabara za vijijini na mijini zile ambazo siyo za *TANROAD*, lakini *TARURA* haina fedha kama walivyosema Wabunge wenzangu, ina fedha kidogo, nafikiri mpaka leo wanapewa asilimia 30 ya *Road Fund* (Mfuko wa Barabara), *TANROADS* wanapewa asilimia 70 na *TARURA* asilimia 30.

Sasa fedha hizi ni ndogo sana, *TARURA* wana kilomita zaidi ya laki moja na kumi ambazo wanazihudumia ambazo kila mwaka zinaongezeka na ni barabara mpya, ndogondogo lakini za muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, hizi barabara ni muhimu kwa sababu ndizo zinawapeleka watu mbalimbali mashambani, zinapeleka pembejeo zinazoenda mashambani huko, zinawasaidia wanafunzi kwenda mashulenii, zinawasaidia wananchi kwenda katika vituo vya afya kupata huduma za afya, bila barabara inakuwa ngumu sana. Kwa hiyo, *TARURA* fedha hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, hasahaha niongee Jimbo langu la Bukoba vijiji pale kama ilivyo majimbo mengine ya Kagera tuna mvua nydingi kwa hiyo ikija mvua moja au mbili barabara nydingi zinashindwa kupiditika zinakuwa hazipitiki hazifai kabisa. Kwa hiyo, tunaomba kwamba tunapopangia hela ya *TARURA* iwe ndogo iliyopo tunatafuta namna ya kuiongeza hiyo ndogo iliyopo Kagera iangaliwe kwa jicho la pekee kwamba ipewe fedha za kutosha kusudi barabara ziweze kupanuliwa kutengenezwa na madaraja yaweze kufunguliwa nakupitika muda mwingu wa mwaka.

**SPIKA:** Ahsante sana!

**MHE. JASSON S. RWEKIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tarimba Abbas atafuatiwa na Mheshimiwa Maida Abdallah.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kipee wewe mwenyewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii lakini nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wanamichezo kwa heshima kubwa walonipa ya kunichagua kuwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* tena katika uchaguzi ambao kwa bahati mbaya sana sikuwepo, hivyo nilichaguliwa nikiwa sipo nataka niwaambie kwamba nitarudishia hisani hiyo kwa kuwatumikia kwa nguvu zangu zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu naupeleka kwenye masuala ya barabara, nimekuwa nikiangalia kila Mheshimiwa Mbunge anayesimama karibu asilimia zaidi ya

80 ya sisi tuliomo humu ndani tumekuwa tukizungumzia suala la *TARURA*. *TARURA* ni chombo kipyä chombo ambacho tumekipa majukumu makubwa sana zaidi ya mzigo wanaoweza kuubeba. Wenyeewe hawana chanzo cha fedha zaidi ya *allocation* ambayo Serikali inawapa kuitia *road fund*.

Mheshimiwa Spika, wanamtandao wa zaidi ya kilomita laki 100 na katika hizo kilomita zaidi ya 78,000 zote ni mbaya, unategemea nini katika utaratibu tunaotaka kwenda nao wa kuinua tija na kuinua mapato kwa wananchi wetu kuinua uchumi katika nchi ambayo barabara nyingi kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni barabara mbaya unapata wapi tija na uchumi ukakuwa kwa kasi tunayoitaka si rahisi.

Mheshimiwa Spika, na ubaya utakuta kwamba *TARURA* yenye kwa kuwa ipoipo natumia neno ipoipo kwasababu haijakuwa *intergrated* na mifumo ya kisheria iliyopo katika nchi hii. Nawapa mfano mmoja ukiangalia sheria ya *Urban Planning Actile* ya mwaka 2007, hasa *section seven* ambayo inatoa mamlaka ya upangaji wa miji, kwa mamlaka za *city, municipal*, ama za mjini. Lakini *TARURA* inakuja inafanya maamuzi yake ya kujenga barabara vile wanavyotaka wao hakuna *consultation* kati ya *TARURA* na *urban authorities* ama *planning authorities* na hiyo inatupa matatizo makubwa kwasababu *user* ni wananchi wa maeneo husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano pale Kinondoni, utakuta kwamba Kinondoni tuko mjini lakini ukienda kwenye kata zote hali ni mbaya sana katika sana katika barabara. Ukienda Kigogo hali mbaya, ukienda Mwananyamala angalau kidogo ukienda Makumbusho ukienda wapi unamleta *Managerwa TARURA* kwa mfano anatoka Kigoma kwa wakwe zangu kule unamleta Kinondoni hajui mahitaji ya Kinondoni na hafanyi *consultations* na *urban authorities* unatarajia nini.

Mheshimiwa Spika, na hii ndio unaikuta katika maeneo mengine kwamba kwa kuwa hakuna *consultations* na wao ndio wanaojenga barabara tunapata matatizo na matatizo hayo yanapeleka kwa mfano kule Kinondoni sisi si wakulima hatuna bahari hatuvui pale katika Jimbo la Kinondoni kazi yetu sisi ni biashara na uchuuzi na shughuli nyingine ndogondogo tunahitaji kutembea sana, tunahitaji barabara ambazo ziko nzuri ambazo zinapitika. Sasa ukiangalia pale kwetu utakuta tunahitaji moja kubwa la barabara ambayo ni kilomita tatu tu iko kuanzia pale Mtaa wa Mlandizi kule na inakuja inapita sehemu za makumbusho inakwenda kuhudumia, kata karibu nne.

Mheshimiwa Spika, sasa ningemuomba Mheshimiwa Waziri kwamba apate muda yeye ama wasaidizi wake twende nao Kinondoni wakaangalie pamoja na kwamba Kinondoni ndio Dar es Salaam, lakini hali ni mbaya sana za barabara na hasa mvua zinaponyesha tunakuwa na adha kubwa sana na ukiangalia Wananchi wa Kinondoni ni moja kati ya watu ambao wanachangia sana katika kodi za Serikali ikiwemo mapato ya pale Kinondoni kwenyewe ambako tunakusanya zaidi ya bilioni 40 kwa mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na hili ningeiomba Serikali sasa iweze ohh! *my God!* naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tarimba, Mheshimiwa Zungu Mheshimiwa Tarimba anasema Kinondoni ndio Dar es Salaam sasa sijui hilo linakubalika kwamba sio llala, Mheshimiwa Hamida Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Pathani ajiandae. Mheshimiwa Hamida Abdallah.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa kwa kunipa nafasi nichangie hoja ambayo hiko mbele yetu. Katika halmashauri ambayo inakusanya mapato mapato madogo ni Halmashauri ya Manispaa ya Lindi. Jana nilikuwa nasikia Mheshimiwa Zungu kwake anakusanya bilioni 60 lakini ukiangalia kwenye halmashauri yetu tunakusanya bilioni moja

na milioni mia tatu tu Lindi Manispaa ina majimbo mawili na majimbo hayo yana changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali kutusaidia kwasababu tayari tumeshaandika andiko mradi kwa ajili ya miradi ya kimkakati ya ujenzi wa soko kuu lakini ujenzi wa stendi kuu ya mabasi.

Mheshimiwa Spika, soko ambalo linatumika sasa lilijengwa tangia mwaka 1950 ni muda mrefu sana soko limekuwa chakavu mno, hata mapato yanayoingia kutoka katika soko lile ni mapato madogo sana tunakila namna ya kuona Serikali ni kwa namna gani mnaweza mkatusaidia halmashauri ya Manispaa ya Lindi kuhakikisha kwamba tunapata fedha za kuwekeza katika miradi hii ya kimkakati ili kuongeza mapato yetu ya halmashuri ili tuweze kuhudumia wananchi wa halmashauri.

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa barabara Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea suala zima la TARURA ninajua kwamba Serikali inaendelea kuboresha majiji miji pamoja na manispaa. Bahati mbaya sana miaka miwili mfululizo katika Manispaa ya Lindi hatujabahatika kupata fedha za kujenga barabara zetu.

Kwa hiyo, ninaiyomba Serikali itusaidie kuhakikisha kwamba kipindi hiki cha fedha tunapata fedha kwa ajili ya kuboresha Manispaa yetu ya Lindi na ukizingatia kwamba tuna changamoto kubwa za barabara na mvua zilizonyesha miaka miwili mfululizo ni mvua kubwa sana uharibifu mkubwa sana wa barabara upo katika maeneo yetu na barabara hizi kushindwa kutumika. kwa hiyo ninaiyomba Serikali iangalie katika hoja hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niongelee swala la Watendaji wetu wa Kata, watendaji hawa ndio wasimamizi wa shughuli za maendeleo katika kata zetu lakini ndio wanaosimamia kukusanya mapato yetu katika kata zetu. Kuna changamoto kubwa sana katika eneo hili, ninaiomba Serikali kuhakikisha kwamba tunaboresha ofisi zao za kata na ofisi hizi zilizokuwepo ambazo wanadandiadandia tu hata vifaa vyaa kufanyia kazi hawana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba sana Serikali kuhakikisha kwamba tunaboresha ofisi za Watendaji wa Kata lakini kuboresha vifaa nya kufanya kazi ikiwemo pikipiki na vifaa vingine nya ofisi ili iwe rahisi wao kupita katika maeneo mbalimbali na kuhakikisha kwamba wanaendelea kukusanya mapato na Serikali tuendelee kupata mapato yetu ili tuweze kumudu kuwashudumia wananchi wetu katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninajua muda mdogo naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi/Vigelegele*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamida Abdallah nishakutaja Maimuna Pathani atafuatiwa na Mheshimiwa Mwamtumu Dau.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi kuchangia hoja katika Serikali za Mitaa, sehemu ya kwanza napenda kuchangia ni uhamisho wa watumishi wa Serikali za Mitaa kumekuwa na matatizo sana la watumishi wa Serikali za Mitaa kuhama kwa suala kubwa hili la kubadilishana hilo suala limekuwa kizungumkuti.

Mheshimiwa Spika, kuna mtu ambaye nilikuwa namshughulikia kabisa mwenyewe aliniomba *document* zake nizishughulikie nimeangaika nazo muda mrefu karibu miaka miwili bila mafanikio na huyo mtu alishapata mtu wa kubadilishana naye na kulikuwa na nyaraka zote ambazo zilikuwa zinatakiwa kwa ajili yakubadilishana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa kila siku naenda Mtumba kila baada ya siku mbili tatu lakini nikifika kule naambiya *document* hizipo natoa kopi zingine naacha, nikika siku mbili nikienda tena naambiya hizo *document* hizipo natoa copy nyingine naziacha pale, nimefuatilia hiyo *issue* karibu miaka miwili mpaka ilipofika kipindi cha kwenda kwenye kampeni nikaacha nikamwambia yule binti aje mwenyewe kibaya zaidi alivyokuja mwenyewe ndio yalitokea mambo ya ajabu sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufuatilia pale aliandikiwa barua feki ya uhamisho yule binti yangu alitaka kufukuzwa kazi alipokwenda kuripoti sehemu ambayo anatakiwa kwenda kuripoti walipofuatilia ile barua ilionekana ni feki. Kwa kweli matatizo yalikuwa makubwa sana, ikabidi niingilie kati yale mambo yakaisha akarudi kwenye kituo chake kilekile cha kwanza. Kwa hiyo, tunaomba TAMISEMI iangalie kitengo hicho cha uhamisho mambo yanayofanyika ni mabaya naya aibu sana tunaomba kuwaomba m jitahidi kurekebisha hapo Serikali yetu Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni eneo la watumishi wa afya na walimu kuna maeneo mengi katika mkoa wetu ya Lindi ni sehemu ambazo sio rafiki sana kwa kuishi, ni sehemu zenyе mazingira magumu. Watumishi wanakwenda pale kwenda kuchukuwa cheki namba baada ya muda wanatafuta uhamisho kuhamza kwenda sehemu nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba kuna watumishi vijana ambaao wamemaliza chuo wako kwenye maeneo yale wameomba nafasi za kazi naomba wapewe kipaumbele wale vijana kuliko mkiwachukuwa watu ambaao wanatoka maeneo ya mbali wanafika pale kuchukuwa cheki namba wanaondoka mfano halisi ni Wilaya ya Liwale, Nachingwea huko Kilimarondo kuna shida sana za watumishi na sehemu nyngi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya tunacho kikubwa kizuri cha Kilimarondo lakini inakatisha tamaa watumishi wako 12 pale wanafanya *operation* zote wana huduma nyngi zote afya lakini hali ni ngumu. Kwanza hata jokofu lile la *theatre* hawana, hawana vifaa tiba, watumishi ni wachache. Na pia kuna hospitali zetu za wilaya kuna Hospitali ya Wilaya Nachingwea, ina hali mbaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hospitali ile ya Nachingwea haina vifaa tiba muhimu kwa mfano kuna wodi ya wazazi iliyopo pale haina kifaa hata kimoja ni jengo tu lipo pale mapambo lakini hakuna kifaa tiba kwenye ile *theatre* na *theatre* kubwa

iliyopo katika Wilaya ile ya Nachingwea haina hata zile taa hakuna hata *washing machine* vitanda ni vya kizamani vimechakaa sana, tunaomba Waziri husika atupie macho hospitali za Mkoa wa Lindi zaidi zile zilizopo pembezoni na Vituo vya Afya ili waweze kusaidia wananchi wa kule wapate huduma stahiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo tunaliomba kwako kwa hawa watumishi ambao wanakwenda kwenye sehemu mazingira magumu tunaomba iweke posho kwa watu wale ahsante naomba kuchangia hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maimuna Pathani. Mheshimiwa Mwamtumu Dau atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest na Mheshimiwa Deo Sanga ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana niugane na wenzangu ambao waliosimama katika Bunge lako hili Tukufu kuichangia TAMISEMI na Serikali za Mitaa. Kwa kuzungumzia moja kwa moja, nazungumzia kwenye hoja maana nisemi Mheshimiwa Ummy Mwalimu nimpongeze na nimshukuru sana kwa kuletwa kwenye kamati hii na kwa kweli umeonekana mtu mahiri wa kuja kwenye kamati hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naanza kutangulia kusema kwamba kuna watumishi wengi katika halmashauri ambao hao watumishi wa umma hawajapata stahiki zao kwa kipindi kirefu. Suala hili la watumishi wa umma ambao waliokuwa awajapa stahiki zao toka kipindi cha miaka ile mitano tuliyopita tulikuwa tunazungumzia wastahiki hawa wa umma katika Serikali yetu. Kwa hiyo, napenda kuishauri Serikali yangu ili hawa watumishi waliokuwa wameacha kazi zao wapewe stahiki zao kwa uhakika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa kuzungumzia suala la kuunganisha vikundi vya watu wenye ulemavu au watu wa mahitaji maalum, tumetembelea katika halmashauri katika kamati yangu hii tumewaona vikundi mbalimbali ambavyo vilivyokuwa havijaunganisha kwenye halmashauri zile watu

wenye ulemavu ili wakaweza kufanya kazi zao katika vikundi vyao na ile asilimia yao mbili wanayoipata, bado awajakaa kabisa wakaweza kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, vilevie napenda kuishauri Serikali waweze kuwapatia mafunzo watu wenye ulemavu ili waweze kujisaidia nakujkwamua kiuchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho nazungumzia kuhusu *TASAF*, *TASAF* kusaidia wananchi wanaonufaika ruzuku za Kaya Maskini, hii *TASAF* tulikuja tukaitia baraka hapa katika Bunge lako Tukufu na kwa bahati hii *TASAF* ipo katika halmashauri lakini napenda kusema kwamba ninaishauri Serikali *TASAF* izidi kufanya kazi zao kwa urefu zaidi ili waweze wale watu wa Kaya Maskini wapate na wao kunufaika, na vilevile wawapatie vikundi mbalimbali katika ndani ya hii *TASAF* ili na wao waweze kufanya kazi zao vizuri na waweze kujkwamua kiumaskini.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kuunga hoja mkono asilimia mia moja ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Dau kwa kutumia muda vizuri Mheshimiwa Anatropia dakika tano pia Mheshimiwa Deo Sanga jiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru dakika tano ni chache sana niliambiwa nitakuwa na saba nianze kwa kueleza changamoto ya walimu wa wilaya ya Kyerwa, na hii nimepigiwa simu mpaka jana usiku saa tisa walimu walioajiriwa mwaka 2012 hawajawahi kupandishwa madaraja naomba muwafikirie sana na hilo suala lao mlifanyie kazi wanahisi kama wamesahauliwa tafadhalii.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nongelee changamoto ya stendi kuna shangamoto ya stendi ya mabasi Nkweda, Nkwenda ni mji mdogo na kumekuwa na ajali nyingi kutegejemea kwamba mabasiyanageuzia eneo lile dogo, kwa

hiyo, kuna changamoto ya ajali nyingi sana naomba hiyo muifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwa tathmini fupi naona muda ni mfupi nimepitia miaka tofauti kuangalia bajeti hii ya Wizara ya TAMISEMI na kwa kifupi naweza nikaeleza fedha imekuwa itatengwa lakini haiperekwi.

Mheshimiwa Spika, mwaka mmoja tu ambao ni mwaka jana ndio fedha imeenda kwa asilimia 62 lakini miaka mingine yote inaenda kwa asilimia 54, 52, 50 na hiyo inakuwa *reflected* kwenye hoja za Wabunge nikulalamikalalamika kwasababu mambo hayafanyiki fedha haiende.

Mheshimiwa Spika, nirudi tena kwenye Wilaya ya Kyerwa tunachangamoto ya huduma za afya tuna hospitali moja ambayo ni hospitali ya Wilaya lakini pia na hospitali ambayo ni ya *mission*. Lakini tunaambiwa kutakuwa zahanati kwa kila Kijiji tutakuwa na Kituo cha Afya, Kyerwa ina zahanati tatu, kata 24 zina Zahanati 3 ikiwa ni upungufu wa zaidi ya asilimia 80 kwa hiyo, watu wa kerwa hawana huduma za afya kwa asilimia 80.

Mheshimiwa Spika, tunaangalia huduma za afya kwa asilimia 80 tunaangalia zahanati, zahanati zipo 24 tuna vijiji 667 tukiwa na zahanati 23 ambayo ni upungufu wa asilimia 97 kwa hiyo watu asilimia 97 kwenye vijiji hawana huduma za zahanati au za kuweza kupata matibabu wanayostahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia watumishi wa umma kwa kada ya afya kuna upungufu wa asilimia 67, tuna watumishi asilimia 24 tu. Kwa hiyo, tunategemea watu wa Kyerwa waishiishi tu, wakiumwa wao wenyewe wanajua itakuwaje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naongea kwa uchungu mkubwa sana, fedha za bajeti zinavyoshindwa kupelekwa kuna maeneo mengine yanafaidika, mengine yanazidi kuwa *disadvantaged*, moja wapo ni Kyerwa na wilaya zake nyingi

za Mkoa wa Kagera; fedha ikiwa haiwezi kwenda haipielekwi kwenye hayao maeneo.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye habari ya barabara, sitaki kuongelea, muda hautoshi lakini kule hakupitiki. Mimi narudia kusema kilio chao, wale ni Watanzania wanalipa kodi, wanastahili huduma. Kwa mfano, Kituo cha Afya cha Nkwenda nimezaliwa mimi, yaani mimi mama yangu alijifungulia pale Anatropia lakini hakijawahi kufanyiwa ukarabati mpaka leo. Pale kwenye wodi alikolazwa hajjawahi kufanyiwa ukarabati mpaka leo mimi nakwenda mama mtu mzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kituo hicho nachokisema kinahudumia *out patients* zaidi ya 1,000 kwa mwezi; wanawake wanaojifungua ni 300 mpaka 400 kwa mwezi; operesheni zinazofanyika pale ni zaldi ya 60 mpaka 70 kwa mwezi lakini hicho kituo cha afya kina upungufu wa majengo, hakina hata mashine ya kufulia. Wanawake zaidi ya 400 wanajifungua pale watu wanafua kwa mkono, *it is totally unfair.* (*Makofii*)

## TAARIFA

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia ukae chini upewe taarifa. Ndiyo Mchungaji, Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimpe taarifa. Pamoja na changamoto anazosisema kwenye upande wa afya, zipo, lakini Kituo cha Afya Nkwenda wamejenga maabara kubwa, wameweka jengo la upasuaji, wamepeleka vifaa vyaa kufulia na vyaa upasuaji na upasuaji unaendelea. Leo hii kuna jengo kubwa pale la mama na mtoto lina zaidi ya vyumba 24, Serikali inaendelea kuvikamilisha. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, hiyo taarifa waipokee watu wa Kyerwa waone Mbunge wao anavyowatelekeza kwa sababu changamoto anazijua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze, hii siyo siasa, wanaoumia ni wananchi wa Kyerwa, wanaokosa huduma za afya ni watu wa Kyerwa, tusilete *drama* hapo. Asitafute *legitimacy* kwa kuumiza watu, tuseme ukweli, pelekeni fedha Kyerwa watu waweze kupata huduma za afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nimeeleza habari ya changamoto ya watumishi wa afya na wale wachache ambaao tuko nao, asilimia 24, wamekuwa wanabaki kwenye maeneo yaleyale madogo. Nitakwenda kutoa suluhisho; Kyerwa bado tuna nafasi ya kuongeza mapato, nimesoma ripoti ya CAG, inaonesha Mkoa wa Kagera ni moja kati ya mikoa ambayo haijafanya vizuri kwenye kupeleka ile asilimia 10 ambayo wanapaswa kurudisha kwa wazee, akina mama na watu wenye ulemavu. Hawapeleki fedha hizo kwa sababu hatuja-*exhaust* vyanzo vya mapato. Tuna uwezo wa kujenga stendi, tulikuwa na masoko ya kimkakati, yametelekezwa.

Mheshimiwa Spika, tuna uwezo wa kufanya biashara na Waganda, tuna uwezo wa kuwa na masoko tukafanya kazi na halmashauri ikawa na fedha. Tunaomba Kyerwa mtukumbuke kwenye masuala ya miundombinu tuweze kuzalisha vya kutosha, tutaweza kufanya maendeleo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Muda hauko upande wako Mheshimiwa.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga nilishakutaja na utafuatiwa na Mheshimiwa Stella Ikupa.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Ummy na Manaibu wake, amepata watu wa kazi naye anafanya kazi nzuri. Nawapongeza Katibu Mkuu na timu yake, Bunge linawaamini watafanya kazi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuna miradi ambayo imekuwa ikizungumzwa hapa na Waheshimiwa Wabunge juu ya miundombinu katika miji 45 na Makambako Mji umo. Wamekuwa wakijibu kwamba mikakati na michakato inaendelea. Tunaomba michakato inayoendelea waimalize haraka ili Makambako tuweze kupata soko kubwa na zuri; tupate barabara ambazo zitaletwa na huu mkopo ambapo fedha zitatolewa na Benki ya Dunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wamezungumza hapa wenzangu juu ya afya. Mimi naunga mkono kwamba kwenye afya kuna changamoto, hasa upande wa bima. Watu wanashindwa kujinga na bima za afya kwa sababu wakienda kwenye matibabu hawapati dawa. Kwa hiyo, tunaomba sana ili tupate watu wengi wa kujinga na bima ya afya tupeleke dawa, hususan katika Jimbo langu la Makambako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuna zahanati tatu pale Makambako ambazo zilitengewa shilingi milioni 150, Mheshimiwa Ummy na wasaidizi wake wanajua. Tunaomba fedha hizi ziende ili wananchi wale kwa zahanati ambazo tumeshawaambia shughuli hizi ziweze kukamilika na kuwashudumia wananchi wa Makambako.

Mheshimiwa Spika, katika elimu bajeti hapa inaonesha mtaongeza sekondari za kata katika nchi hii. Niombe na mimi kwenye Jimbo la Makambako kata mbili hazina sekondari. Kata hizo ni Kitisii na Mwembetogwa, tunaomba tupate fedha ili tuweze kujenga sekondari katika kata hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumzia sana suala la *TARURA* na mimi nawaunga mkono. Nina barabara pale ya kutoka Makambako – Mulowa – Kifumbe – Mutanga hadi Lupembe. Tunaona kwamba fedha ambazo *TARURA* wanatengewa ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, amezungumza jana Mbunge mwenzangu mmoja hapa; ili kuongeza mfuko huu tufanye kama tulivyofanya kwenye Mfuko wa Maji na Mfuko wa *TANROADS*, tuongeze angalau shilingi 100 kwenye simu kama walivyochangia Waheshimiwa Wabunge jana. Pia tuongeze hata kwenye mafuta shilingi 50, itaongeza mfuko huu kuwa mkubwa ambapo barabara zetu zitatengenezwa vizuri. Mjini Makambako tuna barabara moja ya mjini pale inayopitia Golgota, ilitengenezwa lami kilometra moja, imebaki kilometra moja na kitu, niombe Mheshimiwa Ummy kupitia *TARURA* barabara hili iishe.

Mheshimiwa Spika, sasa nina suala maalum. Tangu kitokee kifo cha mpendwa wetu, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kweli mambo ambayo sasa yameanza kuwekwa kwenye mtandao yanahatarisha amani. Ni hatari kwa nchi yetu, ni hatari kwa Taifa letu na vyombo vya usalama vimebaki kimya.

Mheshimiwa Spika, mfano, ukifungua mule unakuta sasa wamemuweka Mheshimiwa Rais wetu Mstaafu Kikwete, Mheshimiwa Katibu Mkuu Mstaafu Kinana, Mheshimiwa Nape na wewe umo, sasa nani atafuata, hii ni hatari! Ni lazima tukemee jambo hili ambalo ni la kutugombanisha Watanzania kwamba watu hawa ni hatari ndiyo waliofanya vitu ambavyo wameandika mule. Hili ni hatari tukiliacha likaendelea, kesho hatujui atawekwa nani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kikwete apumzike Msoga kule amefanya kazi yake vizuri na Mzee Kinana naye akapumzike. Huyu Mheshimiwa Nape wewe ni shahidi, 2013, 2014 mpaka 2015 wakati wa uchaguzi akiwa na Mzee Kinana walizunguka miaka mitatu kutafuta kura za CCM. Mheshimiwa Nape huyu alikatwa mpaka kiganja na Kinana

alipata maumivu ya bega mpaka alikwenda kutibiwa, tuache! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wewe sasa wameanza kukuweka kwenye mtandao. Jamani Spika wetu anafanya kazi nzuri, tumuache Spika afanye kazi yake. Suala la Bagamoyo Spika alichosema kibaya ni nini? Amesema mikataba ile ijadiliwe, ninyi ndio mna uwezo wa kusema hiki hakifai, hiki kinafaa; Bunge hili. Tunaelewana ndugu zangu, Spika alichosema kibaya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo kwenye mitandao, aah Spika sijui nini...

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ndugu zangu, niombe tumuache Spika na Nailbu Spika waendeshe Bunge hili vizuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Sanga. Nilimvumilia maana yake ni Seneta, ndiyo wazee wa mji huu.

Tunaendelea na Mheshimiwa Stella Ikupa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Makoa, Mbunge wa Kondoa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya uzima na uhai ambao anaendelea kunipatia kila siku.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumtakia heri Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mpendwa wetu mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, niendelee kumuombea kwa Mwenyezi Mungu siha njema, hekima na maarifa ya kuendelea kuliongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali kwenye maeneo mengi, kwenye eneo la watu wenyе ulemavu kwa yale ambayo yamekwisha kufanyika na yale ambayo yanaendelea kufayika. Kwanza, naomba nianze na eneo la kamati za watu wenyе ulemavu. Serikali imekimbizana na kuhakikisha kwamba kamati za watu wenyе ulemavu zinaundwa kwenye maeneo mengi ya nchi yetu lakini bado kuna maeneo ambayo kamati hizi hazijaundwa. Niishauri Serikali ihakikishe kwamba zoezi hili la uundwaji wa kamati za watu wenyе ulemavu linakamilika nchi nzima. Pia kwa yale maeneo ambayo tayari kamati hizi zimekwisha kuundwa basi Serikali iziwezeshe ili ziweze kufanya kazi kwa mujibu wa sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kamati hizi ni muhimu sana. Mambo mengi ambayo yanaendelea huko chini ambayo hayagunduliki kwenye eneo la watu wenyе ulemavu yatakuwa solved kama hizi kamati zitaanza kufanya kazi kama ambavyo zilikuwa zimetarajiwа na sheria. Kwa hiyo, Serikali kuititia TAMISEMI iweze kuliona hili na kutenga fedha ili kamati hizi ziweze kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali na kuishukuru sana na watu wenyе ulemavu wamenituma niliseme hilo kwa kuweza kusikia kilio chao na hatimaye kuweza kufanya marekebishо ya kanuni za mikopo ya halmashauri zetu. Itakumbukwa kwamba katika Bunge la Kumi na Moja, Waheshimiwa Wabunge pia waliweza kuishauri sana Serikali kwamba ione namna ya kufanya marekebishо ili basi mtu mwenye ulemavu mmoja mmoja aweze kupata mkopo. Suala hili Serikali yetu sikivu imekwisha kulifanyia kazi. Kuna swali ambalo nililetа lakini sasa sioni hata umuhimu tena wa swali hili kuweza kujibiwa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali kwamba iendelee kuzihimiza halmashauri zetu kutenga fedha lakini pia kununua mafuta ya watu wenyе ualbino na hatimaye kuyasambaza kama ambavyo maelekezo yamekuwa yakitolewa mara kwa mara. Zipo halmashauri ambazo zinatenga fedha lakini kutenga tu haitoshi. Mtu anaishia

kutenga, ukifuatilia kweli fedha imetengwa, lakini mwisho wa siku fedha zile hazikuwahi kufanya kazi ambayo ilikusudiwa. Pia kuna maeneo mengine unakuta mafuta yananunuliwa lakini hayawafikii walengwa. Kwa hiyo, niombe Serikali iweke mkazo mkubwa kwenye eneo hili la mafuta kwa watu wenyewe ualbino.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikisema na naomba nirudie tena; vifaa hivi visaidizi kwa sisi watu wenyewe ulemavu ni kama chakula. Kama vile ambavyo binadamu wa kawaida anahitaji kula, vivyo hivyo mtu mwenye ulemavu hivi vifaa kwake inakuwa ni kama chakula ambacho akikikosa kwa kweli inakuwa inamhatarishia maisha yake. Nimeshuhudia mimi mwenyewe kwa macho yangu kwa sababu nimekuwa kwenye eneo hili kwa muda mrefu; watu wenyewe ualbino wanateseka na kansa za ngozi. Hata kama itatokea mtu ukaona picha yenye kwa kweli sijui unaweza ukafanyaje lakini ni muhimu sana haya mafuta yakawafikia wenzetu.

Mheshimiwa Spika, pia elimu kubwa iendelee kutolewa kwa watu wenyewe ualbino ili iwasaide na/ama iwawezeshe ni jinsi gani pia wanawenza wakajikinga na hizi kansa za ngozi. Kwa sababu unakuta mtu mwingine mafuta amepaka ndio lakini nguo aliyovaa inamhatarishia maisha kwa sababu anakuwa anajiachilia kwenye mionzi ya juu.

Mheshimiwa Spika, naomba niiombe Serikali kwenye eneo la ajira na hasa TAMISEMI, zile ajira zikiwa zinatangazwa basi itolewe angalau hata idadi fulani maalum kwa watu wenyewe ulemavu. Kwa mfano, sasa hivi kuna ajira 6,000, hata zikatengwa nafasi 300 ama 200 kwamba hizi ni kwa ajili ya watu wenyewe ulemavu, kama hawatapatikana basi zitaendelea kuchukuliwa na watu wengine.

Mheshimiwa Spika, kwa harakaharaka naomba nizungumzie suala la miundombinu kwenye shule zetu na hasa vyoo. Vyoo vimeduwa ni tatizo kubwa sana, watoto wenyewe ulemavu wanapata shida, kwa hiyo, Serikali iendelee kuweka nguvu kubwa na kutenga fedha kuhakikisha kwamba angalau basi katika kila shule kunakuwa na tundu moja

ambalo litamuwezesha mwanafunzi mwenye ulemavu kuweza kulitumia.

Mheshimiwa Spika, pongezi zangu zienda kwa Serikali, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika aya ya 73, 74 mpaka 75 imeonesha ufaulu wa watoto wenye ulemavu. Pia kuna ongezeko la uandikishwaji na fedha ambazo zimeweza kununua vifaa visaidizi ambazo ni takribani shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa kutumia muda vizuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Ali Makoa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Salum.

**MHE. ALI J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara lakini pia mimi nichangie katika eneo la elimu. Niikumbushe Wizara ya TAMISEMI kwamba Serikali ilichukua Shule ya Wasichana ya Kondoa na kuifanya shule ya *Advanced Level*/na hivyo ikawa ni shule ya kidato cha tano na cha sita, lakini shule ile ilikuwa ni ya *O-Level*. Baada ya Serikali kuibadilisha hatukupata tena sekondari ya bweni ya wasichana ya Kondoa. Kwa hiyo, naomba katika mpango wa Wizara wa ujenzi wa sekondari kumi za bweni za wasichana, basi waende wakaifidie ile sekondari katika Jimbo la Kondoa Mjini ili mabinti zetu wa kidato cha kwanza hadi cha nne waweze kuendelea kupata masomo katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa elimu, tuna shule yetu shikizi ambayo sasa hivi imekwisha *mature*. Shule ile wananchi walijenga, sasa tuna madarasa manne, wako wanafunzi 300 ina mwalimu mmoja. Kwa hiyo, naiomba Wizara watusaidie kujenga majengo matatu ikamilishe majengo saba ili wanafunzi wale waendelee kusoma na isajiliwe iwe shule kamili ya msingi. Tukisema kuwarudisha katika shule mama itakuwa ni vigumu kutokana na mazingira

magumu na umbali wa kutoka Chang'ombe hadi shule mama ilipo eneo la Tumbelo.

Mheshimiwa Spika, naishauri na kuiiomba Serikali kwamba walimu waliojitelea ni wengi, basi walimu wale katika ajira hizi wapewe kipaumbele kwa sababu wametumia muda wao mwingu kujitolea kufundisha katika sekondari hizo. Pia nishauri, wapo vijana wengi waliomaliza masomo ya ualimu, hawana kazi wako mitaani wakati Serikali inafanya mpango wa kuwaajiri basi watoe tamko la wale vijana waendelee kwenda kuzaidia shule zetu kwa kujitolea angalau wawekewe fungu hata la kupata fedha ya nauli na sabuni kwa ajili ya kujikimu.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa afya, tunafahamu Hospitali yetu ya Wilaya ya Kondoa ilijengwa miaka mingi sana. Leo vituo vya afya vinavyojengwa kwenye kata ni bora kuliko Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kondoa, ni hospitali kongwe sana. Naomba sasa katika ule mpango wa Wizara wa kujenga hospitali mpya, wafikirie namna gani sasa ya kupeleka fedha pia Kondoa kwa ajili ya kujenga hospitali mpya ukizingatia sasa Kondoa ni Halmashauri ya Mji. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Serikali imejenga barabara nzuri sana Kondoa, kwa hiyo, mazingira ya barabara ile yanavutia ajali nyangi. Mara nyangi zinatokea ajali, majeruhi wanapopelekwa kwenye hospitali ile wanakosa huduma na hivyo wanapewa *transfer* kuja Dodoma. Wakati huohuo, hospitali ya mji haina hata *ambulance*, kwa hiyo, wanaanza kuhangai ka kutafuta *ambulance* kuwaleta watu Dodoma. Kwa hiyo, naomba mambo mawili hayo kwamba katika mpango wao waweze kusaidia kujenga Hospitali ya Halmashauri ya Mji lakini pia basi wapeleke *ambulance* kwa ajili ya kusaidia watu wanapotakiwa kupewa *transfer*. (Makof)

Mheshimiwa Spika, jambo linguine kwenye hospitali hii tunayo *X-ray* ya kisasa kabisa lakini watu wanakwenda kupimwa pale wanapewa *CD* wanakuja kusomewa majibu

Dodoma. Tunaomba basi papelekwe mtaalam kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, cha ajabu zaidi ni kwamba hospitali kongwe haina chumba cha maiti. Juzi imetokea ajali watu karibu nane wamefariki lakini hatuna *mortuary*. Kwa hiyo, tunaomba watusaidie kujenga *mortuary* kwa ajili ya kuhifadhi maiti wetu.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa miundombinu, matatizo ni kama yalivyo katika Halmashauri nyengine; barabara zetu ni mbovu. Tulikuwa tunaomba, Halmashauri ya Mji na Halmashauri ya Kondoa itenganishwe wapatikane Mameneja wawili wa *TANROADS* ili mmoja afanyie upande wa *Kondoa DC* na mwingine Kondoa Mjini ili kuwapunguzia mzigo maana eneo ni kubwa sana. Izingatiwe Kondoa ni kubwa imetoa wilaya mbili na majimbo matatu. Kwa hiyo, ni wilaya kubwa sana, tunaomba tupate Meneja wa tofauti kati ya Wilaya ya Kondoa na Kondoa Mjini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa wakati huu. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Bahati mbaya ameshamaliza. Unasema!

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo, haya.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kwa kuzingatia kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako, Toleo 2020, kuomba mwongozo wako juu ya jambo lilitokea hivi karibuni katika majadiliano hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mmoja wa Wabunge wenzetu, amesimama hapa na kuzungumzia mambo ambayo yanajitokeza katika mitandao ya kijamii. Nilitaka mwongozo wako kama mitandao ya kijamii na habari zinazotoka katika mitandao ya kijamii zinaweza zikawa *reference* za kutumia katika majadiliano yetu hapa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu kimsingi kumekuwa na upotoshaji mwinci. Mimi mwenyewe nimeshauawa mara mbili kwenye mitandao ya kijamii; mara nime-*paralyze*, mara nimekufa, naandikwa kwenye mitandao ya kijamii na viongozi wetu wamekuwa wakichafuliwa; sasa inawezekana tukaendelea na shughuli za Bunge, tukawa tunapoteza muda wakati mwincine *ku-refer* mambo katika mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kama ni *reference* sahihi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Kanuni zinasema mwongozo ukiombwa, Spika anaweza kutoa ufanuzi hapo hapo au wakati mwincine. Kwa hiyo, nachagua kufanya wakati mwincine. Tunaendelea na Mheshimiwa Ahmed Salum na atafuatiwa na Mheshimiwa Aysharose Matembe.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Kwanza naiunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri makini sana katika Wizara nydingi na ninaamini kabisa katika Wizara hii ya TAMISEMI, pamoja na wasaidizi wake tunakwenda kufanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka nianze na *TARURA* moja kwa moja. *TARURA* ni mamlaka iliyotengenezwa kwa ajili ya kutengeza barabara vijijini. Inafanya vizuri. Katika Jimbo la Solwa kule kwangu wanafanya vizuri sana, lakini shida kubwa kabisa katika *TARURA* ni upungufu wa fedha watu wanazoiomba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nina kilometa 743, lakini fedha ambazo tunahitaji ni shilingi bilioni saba na fedha ambazo tumepata mwaka huu ni shilingi bilioni 1,100 na *something*. Utaona kwamba tatizo kubwa kwenye *TARURA* ni upatikanaji wa fedha tu. Sasa Wabunge wengi katika Bunge hili wamechangia sana na ukienda katika michango mikubwa, hasa katika Wizara hii ya TAMISEMI ni suala zima la *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai, tumekuwa na Mfuko wa Maji, tumekuwa na Mfuko wa *REA* wa usambazaji wa umeme vijijini, tumekuwa na Mfuko wa *Road Fund*; sasa mifuko hii inaonekana kama kwa namna fulani wanafanya vizuri. Kwa hiyo, tuendelee na mifuko hiyo hiyo. Sasa tuwe na Mfuko wa *TARURA*, tuwe na Mfuko wa Ukamilishaji Maboma ya Halmashauri zetu. Tufanye hivyo tu, na fedha zipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama alivyongea Mheshimiwa Zungu jana, nimemsikia hapa na Waheshimiwa Wabunge, fedha zipo kwenye mitandao, kwenye simu na kwenye mafuta na wananchi hawashindwi kulipa. Kwa maana ukichaji shilingi kumi kwa kila dakika, kwa kila mtu anayepiga simu au kwa kila lita shilingi 50, tutakuwa na mfuko wenye fedha wa kutosha kabisa kwenda kukamilisha miradi yetu katika Halmashauri zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye Hospitali ya Wilaya, nashukuru sana, nimepata shilingi milioni 800 kwenda kukamilisha majengo yaliyobaki. Naomba tu Wizara hii ifanyi kila itakavyofanya; na kipaumbele cha Wizara hii kwa mwaka huu, nilifurahi sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu alivyosema wanakwenda kwenye tiba; vifaa tiba na afya yenye. Sasa kwenye hospitali yangu ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Jimbo la Solwa, tunahitaji vifaa tiba ili tuendelee na kazi kwenye Hospitali ya Wilaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye maboma, nataka sasa niongee juu ya maboma haya. Katika Jimbo la Solwa tuna zahanati 42. Naishukuru sana Serikali imetupa shilingi milioni 150 kwa zahanati tatu ambapo sasa hivi tunakwenda

kukamilisha zahanati hizo; Zahanati ya Kilimawe, Zahanati ya Mwamedilana, tunakwenda kukamilisha zahanati tatu. Vile vile katika *ceiling* tulioipata mwaka huu ni kwa ajili ya zahanati tisa tu. Maana yake katika 42 ukitoa tisa unabaki na 33. Tukienda kwa bajeti tatu bado tutakuwa na upungufu wa ukamilishaji wa zahanati kwa miaka mitatu mpaka 2024.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Wizara ione namna ya ukamilishaji wa maboma haya, siyo tu Jimbo la Solwa, hata nchi nzima tuwe na mipango mikakati. Wizara ikinipa shilingi milioni 500 ya ukamilishaji wa majengo ya zahanati, ikanipa shilingi milioni 500 ya ukamilishaji wa majengo ya sekondari, wakanipa shilingi milioni 500 ya ukamilishaji wa majengo ya shule ya msingi, kila mwaka tutakuwa tumekamilisha kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano elimu ya sekondari, nina majengo 63. Nikija kwenye shule za msingi majengo 80, kwenye zahanati majengo 42 yanataka ukamilishaji wa katika Jimbo la Solwa, ambapo tunakwenda kuwa na zahanati zaidi ya 80 *out of vijiji* 126. Naomba sana, sana tu, Wizara kama Wizara, tunapokuwa na miradi mikubwa, *well and good*, mradi wa reli safi kabisa; mradi wa umeme kule, safi kabisa; sasa twende kwenye huduma za jamii moja kwa moja. Hizo huduma za jamii ndiyo zinakwenda kusaidia wananchi wenye hali ya chini kule (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukitengeneza maboma haya ya zahanati, shule za msingi na nyumba za walimu tukaenda kwenye sekondari, kama ulivyo sema wewe wiki iliyopita, unapowapelekea madawati, mtoto wa masikini anapokaa, ni fadhila kubwa mno kwa Mungu. Sasa ndiyo twende huko. Tujikite sana kwenye maboma na ukamilishaji wa maboma katika Jimbo la Solwa pamoja na nchi nzima kwa ujumla wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni upungufu wa watumishi kwenye zahanati zetu. Nina upungufu mkubwa mno katika zahanati mno. Serikali izingatie hili kupitia TAMISEMI,

Mheshimiwa Ummy namwaminia sana, upungufu wa watumishi ni mkubwa sana... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ahmed Salum.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, dakika ni chache, unaweza kuniongeza mbili!

**SPIKA:** Dakika tano ni chache sana. (*Kicheko*)

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, Mungu akubariki sana. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aysharose Mattembe atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na kutuwezesha kuuona mfungo huu wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana dada yangu Mheshimiwa Ummy kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii ya TAMISEMI, lakini pia niwapongeza sana Manaibu, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange pamoja na Mheshimiwa Silinde kwa kazi nzuri ambayo wameanza kuifanya. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kujikita katika ujenzi wa miundombinu ya shule za sekondari. Hata hivyo, nikiri kwamba shule hizi zina upungufu mkubwa sana wa walimu. Naiomba Serikali itazame Mkoa wangu wa Singida kwa jicho la kipekee, kwani Wilaya zangu za Mkalama, *Singida DC*, Iramba, Manyoni zina upungufu mkubwa sana wa walimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile nangependa kujikita katika suala zima la afya katika Mkoa wangu wa Singida. Tunayo hospitali yetu nzuri ya Wilaya ya Manyoni, lakini hospitali hii ina changamoto kubwa sana ya majengo, majengo mengi ni finyu na pia ni chakavu kwasababu hospitali hii imejengwa muda mrefu sana, miaka ya 1950.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri yetu ya Wilaya ya Manyoni imetenga eneo, naiomba sana Serikali katika bajeti hii iweze kutujengea hospitali mpya ya wilaya na vilevile kukarabati hospitali hii ambayo sasa ni chakavu na majengo yake ni finyu na hospitali hii ibaki kama Kituo cha Afya kwa kuwa kata yetu ya Manyoni haina Kituo cha Afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichangie kuhusu hospitali yetu ya Wilaya ya *Singida DC*. Hospitali hii imekamilika lakini changamoto kubwa, jengo la wazazi halijakamilika. Naiomba sana Serikali ituwezeshe kutupa fedha ili jengo hili nalo liweze kukamilika na sasa wanawake na akina mama waweze kupata huduma bora za afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia tunacho kituo chetu kizuri kabisa cha Mgori kimeshakamilika. Nakushukuru na wewe uliweza kukitembelea kituo hiki wakati wa kampeni, lakini kituo hiki hakina vifaa tiba. Naiomba sana Serikali pia itutazame kwa jicho la kipekee iweze kutupatia fedha kwa ajili ya vifaa tiba. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la uvezeshaji wa vikundi vya wanawake na vijana. Tunazo asilimia 10 zinatolewa katika halmashauri zetu, lakini nikiri kwamba asilimia hizi hazitoshi kukidhi mahitaji ya wananchi wetu. Ipo Mifuko ya Maendeleo ya Wanawake na Maendeleo ya Vijana. Naomba sasa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na TAMISEMI washirikiane ili sasa wananchi waweze kuitambua mifuko hii na waweze kupata mikopo mingi zaidi kwani mahitaji ni makubwa sana. Naiomba Serikali itazame upya utoaji wa asilimia hizi 10 kwani wanatoa fedha, itakuwa ni

jambo jema sana iwapo watatoa vifaa ili mikopo hii sasa iweze kuleta tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzagu kabisa ambao wamesimama hapa na kuzungumiza suala la barabara za *TARURA*. Naiomba sana Serikali iweze kutenga fedha za kutosha ili sasa tuweze kuwa na miundombinu mizuri katika vijiji vyetu na katika kata zetu. Natambua kwamba Serikali imefanya kazi kubwa kwa kuunganisha wilaya na wilaya na mikoa na mikoa, lakini upande wa vijijini bado hali ni tete *especially* katika wilaya zangu zote za Mkoa wa Singida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie suala la mwisho la kuomba tuongezewe watumishi katika vituo vyetu vya afya pamoja na hospitali zetu za wilaya. Katika Mkoa wangu wa Singida kuna uhaba mkubwa sana wa watumishi wa Kada ya Afya. Namwomba sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu atuongezee watumishi wa kutosha ili wananchi wa Mkoa wa Singida wawefeze kupata matibabu kwa ufanisi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja na ninakushukuru kwa nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Aysharose Mattembe. Mheshimiwa Luhaga Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa. Kwa sababu ya changamoto ya muda, niende moja kwa moja kwamba kuna baadhi ya Halmashauri zetu ambazo zina wazabuni na wakandarasi ambao walishatoa huduma muda mrefu, mpaka leo hii hawajalipwa fedha zao. Hii ni kutohana na zile Halmashauri kuelemewa na changamoto za kimapato. Kwa hiyo, wameshindwa kuwalipa wakandarasi na wazabuni ambao walishatoa huduma. Matokeo yake wananchi hawa wanateseka sana, wanauza nyumba zao, wanakimbia miji yao, wamefilisika na wana mateso makubwa. Watu

walishatujengea shule tayari zinafanya kazi, barabara zinafanya kazi, miradi ya maji inafanya kazi lakini hawajalipwa na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ombi langu, Waziri aratibu madeni yote ya Halmashauri zilizoelemewa kulipa madeni ya wananchi hawa ili wazabuni na wakandarasi wapate haki yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la pili, tunao Waheshimiwa Madiwani, Waheshimiwa Wenyeviti wa Vijiji na Waheshimiwa Wenyeviti wa Vitongoji. Tunakubaliana sote hapa umuhimu wa hawa viongozi. Hata hivyo, viongozi hawa ambaa ni Madiwani wetu ambapo leo tunaidhinisha shilingi triliioni 7.68 waende kuzisimamia, hawalipwi. Malipo ya Waheshimiwa Madiwani ni madogo mno kiasi kwamba hawawezi kuhimili na usimamizi huo wala kukidhi mahitaji ya shughuli zao wanazozifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wetu wa Vitongoji na Vijiji hawalipwi kabisa. Tatizo ni nini? Viongozi hawa wame-sacrifice muda wao wote kwa ajili ya kuitumikia Serikali, wanachangisha michango; tukitaka madarasa, wao ndio wanaochangisha, tukitaka zahanati wao ndio wanaofanya; tukitaka mukutano wa hadhara, wao ndio wanaofanya; kwa nini hawalipwi viongozi hawa? Sababu za kutokulipwa ni nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mtendaji wa Kijiji analipwa, Watendaji wengine wote kwenye Kijiji hata 30 wanalipwa, lakini Mwenyeekiti wa Kijiji mshahara wake unakosekana. Ni nani huko Serikalini ambaye alishakataa hawa viongozi wasilipwe mishahara yao inayostahili kulingana na kazi wanazozifanya? Nashauri Serikali ifanye maamuzi ya kuwalipa hawa viongozi ili nao waweze kutoa huduma sawasawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, tumezungumzia kuhusu kupeleka shilingi triliioni 7.68 kwenye Halmashauri zetu. Kwanza nikubaliane kwamba hizi fedha ni ndogo kulingana na

mahitaji tuliyonayo; mahitaji ya barabara, maji, zahanati na huduma mbalimbali kwenye maeneo yetu ya Serikali za Mitaa na kwamba hili ndiyo eneo muhimu sana ambalo wananchi wetu wanapata huduma moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tunapeleka fedha katika eneo ambalo tayari lina changamoto nyingi. Kama tulivyoona taarifa ya CAG kwamba, hati safi zinazidi kuporomoka, hati zenye mashaka zinazidi kuporomoka na kwenda kwenye hati mbaya. Maana yake tunapeleka fedha eneo ambalo lina changamoto kubwa sana ya usimamizi.

Mheshimiwa Spika, sasa hizi changamoto kwa nini zimekuwa za kudumu? Nadhani hapa kuna kazi ambayo hajafanyika sawasawa. Hii kazi tukitaka tuifanye sawasawa lazima tuzifanye kikamilifu zile *activities* zote ambazo zinazohusika ili tuweze kukomesha. Haiwezekani Bunge hili kila likikutana linazungumzia watu kutosimamia fedha vizuri na watu kupata hati chafu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, leo tunaweza tukazungumza Halmashauri zilizopata hati mbaya na chafu, lakini unakuta watumishi wanaohusika hata na kuandaa hizi hawapo. Unakuta hakuna wahasibu, hakuna wakaguzi, unapataje hati safi katika mazingira haya? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mkaguzi hapa anasema, nafasi 510 zinakaimiwa. Kwa nini nafasi 510 zikaimiwe? Kwa nini tuwe na upungufu mpaka wa watumishi Wakuu wa Idara, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo; tunakuwaje na upungufu na watu hawa? Kwa nini hizi nafasi zisizibwe mara moja? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, hivi kwa nini tuendelee na utaratibu wa *vetting* na mambo ya *seniority* katika kuajiri? Hivi kuna shida gani Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Wakuu wa Vitengo wakapatikana kwa njia ya ushindani tu? Tunavijana wengi *competent* sasa hivi. Sasa unafanya *vetting*, miaka mitatu unampata mtu uliyemfanyia *vetting* miaka mitatu, halafu miezi sita unamtumbua kwa

kutokuwa na uwezo. Kwa nini tusifanye ushindani? Wakafanya *oral*, wakafanya *written*, tukapata *competent*? Vijana tunao wa sekta zote, *competent* kabisa. Kwa nini twende na mambo haya?

Mheshimiwa Spika, nafasi hizi zijazwe na tusikubali kuwa na upungufu mpaka wa watalaaamu? Mtu wa kusoma *X-Ray* ni mmoja, halafu unakuwa upungufu wa huyo huyo, kweli! Meatu pale leo miaka mitatu *X-Ray* haifanyi kazi. Ipo pale, haifanyi kazi, hakuna mtaalam wa kusoma.

Mheshimiwa Spika, la pili, tunao hawa wakaguzi wetu, hivi tunapate hati chafu? TAMISEMI mnapataje hati chafu wakati una Kitengo cha Ulaguzi ambacho kinatoa taarifa kila robo mwaka? Mnazisimamiaje hiso taarifa? Mnazi-*coordinate* vipi zile taarifa za ukaguzi mpaka mwingie kwenye hati chafu? Hapa kuna tatizo kubwa la usimamizi.

Mheshimiwa Spika,...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Luhaga.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Malleko.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya TAMISEMI.

Kwanza nianze kwa kutoa pole kwa familia mojawapo katika Kata ninayoishi, Kata Qurus Karatu kwa kuondokewa na mtoto mdogo wa Darasa la Kwanza aliyefariki leo asubuhi wakati anaenda shulenii akavamiwa na fisi, akafiriki, nawapa pole sana.

Mheshimiwa Spika, hii ni ujumbe kwa Serikali kwamba ipo haja ya kuangalia hizi shule zetu za msingi, zijengwe katika mazingira karibu na jamii ya maeneo yale. Vile vile muda wa kwenda shuleni asubuhi kwa hawa watoto wadogo wa Darasa la Kwanza na la Pili kwa sababu ya umri wao kwa kweli sidhani kama ile asubuhi mapema lazima wawe wanafika shuleni ili kuwaweka katika mazingira salama zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inaweza ikafikiriwa kuwa *reviewed* hawa watoto wadogo wa Darasa la Kwanza wanaoenda shuleni asubuhi wakawa wanaingia hata mchana ili kuwaweka katika mazingira salama zaidi wanapoenda shuleni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nichangie katika mambo matatu yafuatayo: kwanza, ni kuhusiana na uhaba wa nyumba za walimu katika shule zetu za msingi na sekondari. Ili tuweze kutoa elimu katika ubora na viwango vinavyotakiwa, pamoja na uwepo wa walimu, pia ni kuhakikisha tunakuwao na miundombinu rafiki yenye kutosheleza ili tuweze kutoa elimu inayotakiwa kwa watoto wetu na kupata ubora ambao tunaoutarajia kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kitabu cha takwimu cha elimu Tanzania, uhaba wa nyumba za Walimu katika shule zetu za msingi, tuna upungufu wa nyumba za Walimu 204,141na kwa shule za sekondari tuna upungufu wa nyumba za Walimu 67,699; jumla ya upungufu nyumba za Walimu katika shule zetu za msingi na sekondari kama nchi tuna upungufu wa nyumba 271,874. Sasa ukiangalia takwimu hizi na ukiangalia kilichotengwa kwa mwaka huu fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu maana yake Serikali inatarajia kujenga nyumba za Walimu 300 tu katika upungufu wa nyumba 271,000. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa ukifanya mahesabu, maana yake kila mwaka kama tutakuwa tunajenga 300, wakati tuna upungufu wa 200,000 *plus*, maana yake tunahitaji miaka 906 ili kukamilisha ujenzi wa nyumba hizi za Walimu hapa nchini. Sasa ni vyema Serikali ikalitazama hili, kama kweli tunataka

elimu iliyo bora na kama tuna upungufu wa kiwango hiki, basi waje na mikakati thabiti ya kuona namna gani tunaondokana na upungufu wa nyumba za Walimu hapa nchini katika shule zetu zote za msingi na za sekondari. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia pia uhaba wa madarasa; uhaba wa madarasa unapelekea wanafunzi wengi kutokupata nafasi za kwenda kuendelea, mfano wakimaliza darasa la saba wanataka kwend *form one* mara nyingi tumeshuhudia ikifika ule wakati ufaulu ukiongezeka Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya wanakimbizana, yaani tunafanya zimamoto kujenga madarasa ili wanafunzi waliofaulu wote waweze kwenda shulenii. Sasa takwimu zipo zinaonesha kabisa wazi, mfano, mwaka 2018 wanafunzi waliokosa nafasi ya kwenda kidato cha kwanza kwa sababu ya uhaba wa madarasa ni 134,000; mwaka 2019 imepungua kidogo imekwenda 21,000; mwaka 2020 waliokosa nafasi ni wanafunzi 59,700.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu, kuna Sera ya Elimu bure, hii sera ndio inakuja kuleta matokeo haya ambayo tunayaona, kwamba ufaulu ukiongezeka maana yakje wanapokwenda huko *form one* wanakosa madarasa, hili linajulikana. Sasa kwa nini Serikali isiweke pia mkakati wa kuhakikisha upungufu wa madarasa unakwisha, wanafunzi wote waliofaulu wanakwenda shule. Takwimu zinaonesha shule ya msingi, upungufu ni madarasa 82,200; shule za sekondari upungufu ni madarasa 4,647. Huu upungufu ni mkubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa tunapojadili suala la elimu na tukitaka kweli tutoe elimu iliyo bora kwa wanafunzi wetu, tukitaka nchi yetu itoe *product* nzuri kwenye sekta ya elimu hatuna budi kuwekeza kuhakikisha nyumba za Walimu na madarasa yanakuwepo na kuhakikisha kwamba wanafunzi waliofaulu wanakwenda shule na isije ikatokea sababu hawaendi shule eti kwa sababu tu hakuna madarasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie hoja ya mwisho ambayo nimejikita kuzungumzia leo, ni suala la udhibiti ubora katika Idara ya Udhibiti Ubora...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Parezzo. Hii takwimu ya nyumba za Walimu inabidi kuangaliwa vizuri. Kwa sababu shule za mijini, Majiji, Miji, Manispaa, Miji Midogo Walimu wengi hawapendi kukaa shulen na kuna nyumba nyingi tu nzuri. Kwa hiyo, sio lazima Mwalimu aishi shulen, lakini kuna vijiji vipo *remote* na maeneo ambayo ni *remote* kabisa ambako tunahitaji nyumba za Walimu. Kwa hiyo idadi hii iwe inachukuliwa kwa idadi ya Walimu na nyumba zilizopo unagawanya pale, kuna baadhi ya maeneo wanajenga nyumba ya Mwalimu, shule nzima hakuna Mwalimu anayekaa hapo. Wanakaa kwenye maeneo yao na siku hizi usafiri bodaboda. Kwa hiyo, mtu anaweza kwenda akarudi jioni na kadhalika, inahitaji kuiangalia kidogo hiyo takwimu.

Mheshimiwa Esther Malleko nilikutaja, utafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia kwenye Wizara ya hii ya TAMISEMI. Moja kwa moja nijikite kuchangia upande wa elimu. Naipongeza sana Serikali yangu sikivu kwa kuweza kusimamia kujenga shule kwenye kila kata. Suala hili la kuwa na shule kwenye kila kata limetupunguzia adha kubwa ya wanafunzi kupata au kwenda mwendo mrefu kwa ajili ya kwenda shule. Pamoja na Serikali kufanya kazi hii kubwa ikatenga shilingi bilioni 23 kila mwezi kwa ajili ya elimu bure, imefanya kazi kubwa sana naipongeza sana Serikali yangu. (*Makofî*)

Mhehimiwa Spika, naomba kutoa ushauri kwa Serikali yangu sikivu, kwamba baada ya kujenga shule hizi kwenye kila kata, tuangalie sasa ni namna gani tunakwenda kujenga *hostel*, mabweni kwenye kila kata sasa ili wale wanafunzi

ambao wanatoka umbali mrefu wasipate shida njiani. Nasema hivyo kwa sababu wanafunzi wa kike wanakutana na vishawishi vingi wakati wanakwenda shule. Wakati mwininge kutokana na umbali wanaokwenda wanaweza kurubunika katikati hapo wakaingia kwenye mitego mingine mingi kwa sababu wanaona muda wa kwenda shuleni na kufika kwa wakati unakuwa ni kidogo. Kwa hiyo naiomba Serikali yangu sikivu iweze kuangalia ni namna gani sasa tumemaliza kujenga shule za kata, tunatoa elimu bure, lakini namna gani tunaweza kujenga mabweni ili wanafunzi hawa waweze kupata elimu sahihi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ule muda wanaotoka shule na kurudi nyumbani wanatumia muda mrefu, lakini wangekuwa shuleni wangeweza kusoma kwa bidii, wakapata muda wa kusaidiana na wenzao, wakapata muda wa kufundishwa zaldi, tofauti na hapa ambapo leo wanatoka shule, wanakwenda nyumbani, wanakuta nyumbani kuna kazi ambazo watasaidia wazazi, kwa hiyo wanakosa muda wa kujifunza kwa muda mrefu. Naomba sana dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu sina mashaka naye, najua yeze pamoja na wasaidizi wake wataliangalia hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema kuhusu wanafunzi, niseme kuhusu Walimu. Walimu hawa wanatusaidia kuangalia watoto wetu, tunaenda makazini na tunafanya kazi zetu kwa sababu tunajua wapo walimu ambao wanatunza watoto wetu, lakini walimu hao hao wamesahaulika, kiwango chao cha malipo kipo chini. Ni lazima sisi kama Bunge Tukufu tuweze kuangaliana kuwapigania Walimu hawa ili waweze kuongezewa mishahara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, Walimu hawa wanakwenda masomoni wakiwa shuleni. Wanapokwenda masomoni wengine wanaobaki shuleni ambao wanaendelea na kazi wanaongezwa mishahara au kupandishwa vyeo, lakini hawa walikwenda kujiendeleza pamoja na kwamba wanajiendeleza kwa pesa zao, tena kwenye kima kile cha mshahara mdogo wanaolipwa,

wanaweza kwenda kujiedelea ili wafanye kazi kwa ufanisi mkubwa, lakini shida inatokea wao wakiwa masomoni wenzao wanapandishwa mishahara, wanapandishwa madaraja, lakini wao hawapandishwi wakiwa masomoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali yangu sikuweze kuwaangalia hao Walimu, imekuwa ni kada ambayo imeachwa nyuma, ni kada ambayo haiangaliwi, wengine wakienda masomoni wakirudi mishahara yao inaongezeka, lakini kwa hao walimu ambao wanatuangalizia watoto wetu, hao walimu wanaotusaidia kufuta ujinga, wamesahaulika. Kwa hiyo naiomba Serikali iangalie pia suala hilo la Walimu. (*Makofi*)

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika. Taarifa

**SPIKA:** Uko wapi?

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, niko hapa!

**SPIKA:** Endelea.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, suala la mishahara na suala la kutokopandishwa vyeo wakiwa shule sio Walimu tu ni watumishi wote Tanzania. Naomba kumpa taarifa hiyo.

**SPIKA:** Unaipokea taarifa hiyo, Mheshimiwa Esther E. Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante naipokea taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kero nyininge kwa Walimu, ni kero kubwa kwa wale Walimu wanaostaifu. Baada ya kustaafu anapotakiwa kubeba mizigo yao na kurudi nyumbani kwao inakuwa wanacheleweshewa kupata yale malipo na hii inaendelea kukatisha tamaa kwa sababu hao watu

wamefanya kazi hiyo kubwa kwa maisha yao yote, lakini wanapofika wakati wa kustaafu bado hata ile hali ya kuangaliwa waweze kurudi nyumbani kwao imekuwa ni shida.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia japokuwa jana jioni nilipewa nafasi ya kuchangia, lakini nashukuru sana kwa kupewa tena mara ya pili.

**SPIKA:** Hapana! kama ulichangia jana basi haupo. (*Kicheko*)

Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kwanza kukushukuru binafsi kwa kuniona. Pili, kushukuru kwa hotuba nzuri ya Wizara ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikiwa ni sambamba...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, huyu anayeongea ndiye aliyechukua Jimbo la yule Mbunge ambaye alikuwa anajita Bwege. Sasa mbadala wake ni Mheshimiwa Kassinge, karibu sana hiyo ndiyo bunduki mpya ya CCM. (*Makofi*)

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, niendelee kupongeza Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa mawasilisho ya hotuba ya bajeti, lakini kwa kuaminiwa na mamlaka katika timu zote kuanzia Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake, lakini pia Katibu Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo langu la kwanza la uchangiaji ni kuishauri Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuja na sera ya ugatuaji ili maeneo ya mgawanyo wa madaraka katika maeneo yote ya siasa, utawala, fedha yabainike baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, katika eneo la mapato ya halmashauri, kuna eneo la mapato ya ushuru wa mazao *produce cess*. Ushuru huu umekuwa ukitofautiana katika ya halmashauri moja na halmashauri nyingine. Niishauri Ofisi ya Rais, TAMISEMI iweze ku-*harmonies* ili ushuru huu uwe sawa na halmashauri zote na kuondoa mgogoro au mgongano ikiwa ni sambamba na kurudisha asilimia tano ya ushuru wa mazao badala ya asilimia tatu ya sasa hivi, kwa sababu utafiti umebainisha kwamba wanaochangia halmashauri katika ushuru huo wa mazao asilimia tatu ni wanunuzi na si wakulima.

Mheshimiwa Spika, pili, kuna eneo hili la *property tax* ambalo baadhi ya Wabunge hapa wamelizungumzia. Kimsingi hili ni eneo la ushuru au mapato ya *Local Authority*, lakini hali ilivyo sasa hivi inakusanya na halmashauri lakini ina hesabika kuwa ni mapato ya Serikali Kuu. Nishauri eneo hili lirudishwe halmashauri na hayo ni mapato ya halmashauri ili zikajenge barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna ushuru wa halmashauri wa kimazoea (*traditional*) wa siku nyingi, ushuru mdogo mdogo wa wajasiriamali, wauza vitumbua, wauza mahindi ya kuchoma na kadhalika.

Lengo la Serikali kutoa vitambulisho kwa wajasiriamali lilikuwa ni lengo zuri na kazi hii inafanywa vizuri na Watendaji wa Halmashauri kukusanya fedha kupitia vitambulisho 20,000 kwa mwaka, lakini mapato yanahesabika si mapato ya halmashari bali ni mapato ya Serikali Kuu, yanakwenda Hazina moja kwa moja. Niishauri Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Serikali kwa ujumla, mapato yanayotokana na wajasiriamali wadogo wadogo yarudi halmashauri yakajenge barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kushauri masuala ya kisera sasa nije katika eneo langu la uongozi na uwakilishi kwa maana ya changamoto zilizopo katika Jimbo la Kilwa Kusini, nikianza na eneo la barabara zinazohudumiwa na TARURA. Naomba hapa nitoe takwimu; kuanzia mwaka 2017/2018 – 2019/2020, Halmashauri ya Kilwa imekuwa ikipata fedha za barabara billioni moja *pluskidogo* hivi, lakini kuanzia 2021 imekuwa ikishuka ni mpaka kufikia Sh.984,000,000 na hali hii imeendelea kushuka mpaka bajeti hii tuliyonayo. Kwa hali halisi ya urefu wa barabara za Kilwa ambazo ni zaidi ya kilomita 1,000, Sh.984,000,000 hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, nashauri tuongeze bajeti hii ili ikahudumie barabara zile. Hapa naomba nizungumze barabara mahsusni na naomba hizi zipewe kipaumbele. Barabara ya kutoka Hoteli Tatoo - Pande, Hoteli Tatoo - Lihimalyao, sisi Wanakilwa hii ni barabara ya kimkakati inaenda kuhudumia wakazi wapatao 30,000 ambao ni wazalishaji wakubwa wa korosho, kwa hiyo itakuwa ni barabara ambayo itajenga uchumi katika eneo hili. Nishauri kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, barabara isiingie katika utaratibu wa *maintenance*, badala yake iingie katika utaratibu wa *development* na itengewe fedha za kutosha ili ipitike kipindi chote cha mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho Sekta ya Afya. Hospitali yetu ya Wilaya ya Kilwa imechakaa vya kutosha...

**SPIKA:** Kengele imeshagonga. Ahsante sana Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Kwa hiyo tunaomba hospitali ikarabatiwe, kama si kujenga hospitali mpya.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah J. Komanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Venant Protas.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika hoja ya TAMISEMI. Nianze moja kwa moja kwa kuiomba Serikali itenge fedha kwa ajili kujenga daraja la Mwamanongu ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati akiomba kura mwaka 2015 kama Mgombea Mwenza. Alitoa ahadi hiyo akiwa katika Kata ya Mwabuzo kwamba daraja la Mto Mwamanongu Ijengwe, lenye urefu wa mita 120 ambalo linaweza likagharimu shilingi billion 1.5. Sisi kama halmashauri tayari tumeliweka katika mpango wa mwaka huu katika fedha za maendeleo. Naomba katika miradi iliyowekwa katika miradi ya maendeleo lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, niungane na maoni ya Kamati ya TAMISEMI kwamba Serikali isimamie na kuhakikisha halmashauri nchini zinatenga na kutoa fedha katika Mfuko wa Barabara. Kabla ya *TARURA* Julai, 2017, halmashauri zilitenga fedha kwa ajili ya miradi kwa ajili ya kuanzisha barabara mpya na fedha hizo zilitengwa katika miradi ya maendeleo. Kwa halmashuari niliyopo fedha hizi zaidi zilitengwa kwenye fedha ya *CBG*. Kazi ya halmashauri ilikuwa ni kuanzisha barabara mpya, baadaye zilikuwa zikichukuliwa wakati huo zilikuwa ni Mfuko wa Barabara (*Road Fund*).

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuanzisha *TARURA*, halmashauri imejitoa katika kuanzisha barabara mpya, kwa hiyo *TARURA* haina barabara za kuzirithi kutoka halmashauri. Niishauri Serikali katika asilimia 40 ya mapato ya ndani, Kamati ya TAMISEMI kila inapoidhinisha bajeti ya halmashauri, ihakikishe kiasi fulani kimetengwa kwa ajili ya kuanzisha barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naunga pia mkono kuhusu fedha za *TARURA*, Serikali iendelee kuziongoeza. Sisi Halmashauri ya Meatu mtandao wa barabara ni kilomita 1,041, lakini tumetengewa shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kilomita 253 na Makalvati 11, sawasawa na asilimia 24. Fedha hii haitoshi kabisa kwa ajili ya mtandao mzima. Kwa hiyo unakuta barabara nydingi zaidi ya miaka 10 hazijafanyiwa ukarabati, ikiwepo barabara ya Mwambegwa - Sapa, barabara ya

Itaba - Mbushi mpaka barabara hizo zimeota miti mikubwa kwa sababu hazifanyiwi ukarabati. Halikadhalika zaidi ya miaka 15 barabara ya Mwamanoni mpaka Mwanzugi haifanyiwi ukarabati kiasi kwamba maji yameosha maboksi kalvati na wananchi wanapitia pembedni na wengine wameng'oa nondo katika makalvati haya.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwepo na utaratibu wa kuzipatia zamu za kufanyiwa ukarabati ili wananchi pia waweze kufaidika na kuweza kupita bila tatizo lolote. Lakini katika utangazaji wa kazi za barabara za *TARURA* naomba *at least* asilimia 50 ya barabara ziwe zinatangazwa mapema kuliko hivi sasa zinasubiri kutangazwa wakati zinaanza. Inakuwa ni masika, fedha yenye we ni kidogo zinashindwa kutekeleza na wananchi wanaendelea kupata shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo nina wasiwasi na mkandarai tuliyepewa katika Jimbo la Meatu. Nina wasiwasi na uwezo wake, mara ya kwanza alikuwa anasingizia mvua lakini sasahivi mvua hakuna na hakuna chochote kinachoendelea kwa ajili ya barabara ya Mwanuzi - Mwabuzo, barabara ya Mwambegwa - Mwamanigwa. Niionbe Serikali wakati wa utoaji tenda ufanyike katika *level* ya wilaya ili waweze kumu-*own* yule mkandarasi tofauti na sasa kazi zinatolewa katika ngazi ya Mkoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Leah Komanya. Nimeshakutaja Mheshimiwa Venant na Mheshimiwa Aida Khenani atafuata.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa hii nafasi. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Igalula nianze kuchangia kwasababu ya ufinyu wa muda, nianze kwa kuchangia suala la barabara, Jimbo la Igalula tumekuwa tukipiga kelele mara kadhaa hapa

kulalamikia barabara zetu, nyingi hazipitiki hasa wakati wa masika.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto ya baadhi ya barabara na baadhi ya kata tangu dunia iumbwe, tangu tumeepata uhuru hawajawahi kuona *caterpillar* la kusafisha barabara limepita katika maeneo yao. Kwa mfano katika kata ya Male toka tumeanzisha hii kata, halijawahi kupitiwa na barabara yoyote kwa bahati mbaya kupitia Serikali. Pia, Kata ya Nsololo haijawahi kupitiwa na *caterpillar* ambalo linasafisha barabara katika kata hiyo. Vile vile kuna barabara za Ipururu – Igalula haijawahi kupitiwa kabisa. Barabara za Kawekapina kuja Igalula hazijawahi kupitiwa. Ziko changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali kwasababu tuna chombo na taasisi ambayo kimeanzishwa na Serikali *TARURA*, tuiombe Serikali iongeze fedha kwasababu yawezekana *caterpillar* haziendi katika maeneo haya kwa sababu ya ufinyu wa bajeti lakini *TARURA* ikiongezewa fedha na halmashauri yetu ikaletewa fedha kupitia mfuko wa *TARURA* nina imani katika maeneo haya na wananchi wataona ma-*caterpillar* yamepita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto ya daraja, jana Naibu Spika amesema katika Jimbo lake kuna watu watano wamepoteza maisha, roho inamuuna sana. Kila mwaka zaidi ya watu 20 wanapoteza maisha katika Kata ya Loya ili mtu aweze kuja kupata matibabu katika Kijiji cha Loya kutoka Mwamabondo lazima avuke mto. Kila mwaka akinamama wajawazito, watoto wanaoenda shule wanapoteza maisha zaidi ya 20 kila mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, imekuwa likipigiwa kelele Daraja hili la Loya tangu mwaka 2013. Nimejaribu kupitia *Hansard* za Wabunge waliopita mwaka 2013 mpaka 2015 Mbunge aliongea, 2020 Mbunge alizungumza na baadaye akaamua kuwa maji yamemfika shingoni akaamua kwenda kuwadanganya wananchi akawaambia kuna fedha imetengwa ya kuja kujenga daraja.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kupita kuwa Mbunge nilikuja kufuatilia fedha hizi sijaona fedha yoyote iliyotengwa. Niiombe Serikali, kwa haya madaraja ambayo ni kiungo ya kijiji na yenye huduma kwa wananchi muda wote niiombe Serikali iwekee kipaumbele, tuna hitaji Daraja la Loya lijengwe kwasababu limeanza kupigiwa kelele zaidi ya miaka 10. Niombe Serikali iweze kusaidia katika hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya TAMISEMI 2021/2022 sijaona wametutengea fedha za kuweka vifaatiba katika kituo chetu cha afya. Tumejenga majengo mazuri, Serikali imewekeza fedha nyngi, tunashindwaje kuweka vifaatiba ili wananchi wetu waanze kutumia yale majengo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, majengo yamekaa kila siku tunapeleka wanafunzi wanakwenda kukalia, yanakuwa machafu nyoka wanaingia kwenye majengo. Niiombe Serikali, kwa hivi vituo ambavyo vimekamilika, wapeleke vifaatiba ili wananchi waanze kupata huduma. Vile vile tuna majengo mengi ya zahanati lakini kwenye bajeti hii wametuwekea kila jimbo angalau watapata zahanati mbili. Nina maboma zaidi ya 10 yapo, wananchi wameweka nguvu zao wanahitaji wapate huduma za afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwananchi anapochangia hela yake ya kwenda kujenga kitu, ana malengo nacho kwasababu amepata shida kwa muda mrefu. Kwa hiyo, yale majengo naomba Serikali itanue wigo wa kuongeza bajeti ya kujenga haya maboma. Sisi kazi yetu tunanyanya maboma lakini Serikali mnapokuja na Mpango wa zahanati mbili mbili, kwa hiyo, nitachukua zaidi ya miaka 20 kumaliza maboma yangu. Niiombe Serikali, kwenye bajeti hii watuongezee ili wananchi wanapotoa nguvu zao basi waone matokeo kwa uharaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru, niachie wigo na wenzangu waendelee kwasababu niliomba tu dakika tano na wewe umenipa. Ahsante, nashukuru sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Venant Protas, tunakushukuru. Mheshimiwa Aida Khenani nilishakutaja atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi kwasababu ya dakika chache nitakwenda moja kwa moja Jimboni na kabla sijakwenda huko kama Wabunge wengine walivyozungumzia kuhusu *TARURA* naomba kushauri mambo machache.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba wahandisi waliochukuliwa kutoka kwenye Halmashauri sasahivi wako kwenye vyeo vya muundo wa *TARURA*. Kuna wengine ambaobado hawajaanza kulipwa kulingana na mamlaka waliyonayo. Sasa tusiweke hizo habari za mamlaka kana *show*. Kama tumeamua kusema kwamba huyu ni Meneja wa *TARURA* ngazi ya Halmashauri, alipwe kulingana na nafasi aliyonayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba kwenye ngazi ya mkoa tuna mratibu wa *TARURA* Mkoa. Yule mtu kuwa peke yake pale kunakuwa na changamoto kadhaa kwa sababu akiwepo pale peke yake yeye ndiyo anayehusika na manunuvi. Huyo huyo mratibu peke yake ndiyo anayehusika na kutangaza *tender*. Kumekuwa na changamoto kwa hawa wakandarasi na changamoto hizo zinaenda kuathiri wananchi moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri, ni vizuri tukaangalia muundo wa *TARURA* upya ili kuweza kutimiza malengo ambayo tulikusudia baada ya kuanzisha chombo hiki.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia maeneo machache, kuna barabara ya Kirando – Korongo na leo nimekushuhudia Mheshimiwa Naibu Waziri ukiwa unajibu hilo swali ambalo kuna daraja la Kavune. Nitambue mchango wa Serikali kwenye jambo hili kwamba wamepeleka fedha kiasi kwa ajili ya ujenzi wa hili daraja lakini uhitaji wa daraja hili na hiyo barabara kwenye lile eneo ni muhimu sana.

Niwaombe TAMISEMI kuna mambo ambayo hayahitaji kufanya siasa, kuna maeneo tunayotoka pembezoni. Tukileta siasa kwenye afya, tukaleta siasa kwenye elimu, tukaleta siasa kwenye miundombinu tutawaumiza wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo kwasababu leo tuna Sera ya Afya ambayo inataka zahanati kwa kila Kijiji, inataka kituo cha afya kwa kila Kata. Wilaya yangu ya Nkasi ina Kata 28, kata zenye vituo vya afya ni kata tatu tu. Tukianza kuzungumzia habari ya llani miaka yote walikuwa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi, kwanini mlishindwa kutekeleza jambo hili. Kwasabbau hiyo, nataka nishauri tu kwa nia njema, basi hizo kata tatu zenye vituo vya afya basi zitoe huduma kulingana na *level* ya Kata kwa maana ya kituo cha afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukija kwa wauguzi bado kuna changamoto, pamoja na kwamba hatujatimiza, hiyo sera haijatekelezeka lakini katika hizo chache tulizonazo basi angalau tupeke huduma zinazoweza kujitosheleza kuwasaidia wananchi wetu. Natambua kwamba wananchi wamehamasika kuweza kuanzisha maboma mbalimbali kwa ajili ya zahanati na vituo vya afya, ni vizuri! Pamoja na kwamba uhitaji ni mkubwa, fedha mnayopata TAMISEMI ni ndogo. Lazima tuwe na kiipaumbele, na kipaumbele ni kuanza kuhestimu nguvu za wananchi ambazo wanakuwa wamezanzisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kata ya Kabwe, Waziri Mkuu amekwenda pale akaahidi kwamba kituo cha afya kitafunguliwa mapema kwasababu ya bandari iliyozanzishwa kule. Mpaka leo ninavyozungumza hakuna fedha yoyote tumeona baada ya tamko lile na haya matamko sio mabaya lakini yamekuwa yanaathiri mambo mengi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naweza nikarudi tu hapo kwenye masuala ya TARURA, unakuta kuna matamko au maagizo au ahadi za viongozi wa Kitaifa. Ahadi sio mbaya lakini ahadi hizo zinavyokuja zinatekelezwa kwa kiasi gani ahadi za viongozi wa Kitaifa na wakati mwингine zinakwenda kuharibu

bajeti za halmashauri, kwa hiyo inakuwa ni ugomvi kati ya wananchi pamoja na viongozi waliopo kwenye kada hizo. Kwa hiyo, ni vizuri hata hizo ahadi zikawa kwenye kumbukumbu maalum. Tunapokuwa tunaandaa bajeti tunakuwa tunajua kuna ahadi ngapi za viongozi wa Kitaifa ili utekelezaji unakuwa unaeleweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine naomba nizungumzie kwenye elimu. Pamoja na kwamba elimu inatolewa Tanzania nzima kuna maeneo ambayo yanahitaji mkakati za ziada, hasa sisi ambao tunatoka pembezoni. Mpaka hivi ninavyozungumza kwenye Wilaya ya Nkasi kuna kata nne ambazo watoto ili wakafanye mtihani wanatakiwa wapite kwenye maji, yaani wavuke maji wakafanye mtihani sehemu nydingine. Leo unazungumziaje matokeo chanya kwa watoto hawa? Anavyopita kwenye maji akafanye mtihani kwanza tumem-*disturb*, arudi tena nyumbani, kesho tena aende apande boti, maboti yenyehe hayapo, Serikali hamjapeleka boti. Lakini na sisi tunataka Marais watoke kwetu yaani mnaamini kwamba Nkasi Rais hawezi kutoka? Lakini kama tunaamini hivyo, lazima tutengeneze mazingira rafiki kwa watu hawa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wanapozungumzia watu wengine kwamba kuna wengine wamekuwa kwa kung'atwa na fisi, Wilaya ya Nkasi watoto wanang'atwa na mamba isivyo kawaida! Leo ni kosa la nani? Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha watoto wanatengenezewa mazingira rafiki kwa ajili ya kupata elimu kwasababu elimu sio fadhila, elimu ni wajibu wa Serikali iliyopo madarakani kutoa elimu kwa watu wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida, unga mkono hoja. (*Kicheko*)

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa. Atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia mchango wangu. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuchaguliwa kuwa katika Wizara hii ya TAMISEMI na Naibu Mawaziri wake, wanaofanya kazi vizuri. Sina wasiwasi na viongozi wetu hawa katika Ofisi hii ya Rais TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu yatokanayo na mgawanyiko wa majukumu yaani *presidential instrument* kwa Wizara hii ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni kuziwezesha Tawala za Mikoa kuendesha majukumu yake ya kisheria. Kwa kuwa moja ya majukumu hayo ya kisheria ya Serikali zetu za Mitaa yanatakiwa yaendeshwe kwa gharama zinazotolewa katika bajeti na Serikali.

Mheshimiwa Spika, sisi katika Mkoa wetu wa Ruvuma Halmashauri zetu kwa ujumla wake nitatolea mfano mwaka 2019/2020 *OC* zilizoidhinishwa ziliikuwa ni bilioni 20 milioni 255 lakini zilizopokelewa ni asilimia 47, bilioni tisa. *OC* ndiyo zinazofanya kazi ya kuendesha shughuli za Serikali za Mitaa Kisheria kwa maana ukiondoa mishahara, kwenda kuangalia shughuli za maendeleo, kusimamia n.k. sasa sisi mkoa wetu una *square kilometers* 67,372. Ukitoka kwa mfano mkoani kwenda mpaka Tunduru ni zaidi ya kilometra 260, kunahitajika magari ya kutosha, kunahitajika fedha za kwenda kugharamia mafuta n.k. ukifika Tunduru kwa mfano kwenda katika eneo la Kusini unatembea zaidi ya kilometra 100 na kidogo. Ukifika Namtumbo kwenda kufika katika Kata ya mwisho unatembea zaidi ya kilometra 200 na kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, fedha za *OC* za miaka hiyo, 2019 zilikujaa asilimia 47. Nasema haya kwa maana ya kwamba ukitazama katika mikoa mingine katika randama kuna wengine sekretarieti ya mkoa imepata zaidi ya asilimia 113. Kwa hiyo, ninachotaka kuiomba Serikali, wanaotoa fedha hizi, wanaofanya *disbursement* asilimia za ugawaji wa fedha uendane sawa na mikoa yote kuliko kufanya

upendeleo mkoa fulani unapata asilimia 47, mkoa mwingine unapata zaidi ya asilimia 100. Kwa hiyo, naomba sana ili twende sambamba *disbursement* za fedha hizi zinatakiwa lazima zitoke sawasawa. Sitaki kutaja mkoa gani lakini tazameni kwenye randama mtaona tofauti zilizopo. Nimetolea mfano wa eneo langu la Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, lakini fedha za maendeleo pia angalau tuliidhinishiwa bilioni 30 lakini tukapata bilioni 21 na milioni 600 sawa na asilimia 72. Lakini mpaka bajeti ya mwaka huu 2020/21 mpaka Februari, tumepata asilimia 31 za *OC na development* asilimia 26.9. Kwa hiyo, bado naamini kabisa sidhani kama tutafikia asilimia 100 mpaka tutakopofika Juni 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kuomba kwanza Serikali ituongezee ukomo wa bajeti, ituongezee pia zile hela ambazo zinapitishwa kwenye bajeti basi tuzipate kwa asilimia 100 katika mikoa kama ya Kusini ambayo ina mipaka miwili ina kazi kubwa sana katika kuhakikisha kwamba wananchi wake wanasimamiwa na wanapata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sisi katika Wilaya yetu ya Namtumbo ina kilometra za mraba 20,375 tuna watu 240,000 lakini jimbo hilo hilo lina jimbo moja na halmashauri moja lakini utakuta katika mkoa wetu nachukulia mfano, una halmashauri zingine zina *square kilometer* 6,000, watu ni wengi lakini kilometra za mraba ni ndogo ukilinganisha na eneo letu. Kwa hiyo, inakuwa ngumu sana katika wilaya na halmashauri yetu kusimamia au kwenda kuleta maendeleo ya wananchi kwasababu kilometra za mraba ni kubwa lakini fedha wanazozipata ni kidogo sana kulinganisha na shughuli zilizopo katika wilaya yetu. Lakini ukitazama malengo tunayowekewa na Serikali tunayatimizia kwa asilimia zaidi ya 100. Sisi tuliwekewa lengo la kukusanya bilioni 1.4, tulikusanya bilioni 1.6.

**SPIKA:** Ahsante, muda tayari. Ahsante sana Mheshimiwa Vita Kawawa. Mheshimiwa Edwin Swalle, nilishakutaja na utafuatiwa na Mheshimiwa Charles Kajege.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wizara ya TAMISEMI, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wake Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Dkt. Dugange kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. Pia kwa upekee kabisa, nimpongeze sana Katibu Mkuu wa Wizara ya TAMISEMI Profesa Silas Shemdoe. Amekuwa na ushirikiano mzuri sana na Wabunge kwa kadri ambavyo tunakwenda kumuona na hata ukimpigia simu usiku anapokea na kujibu changamoto mbalimbali. Nampongeza sana Profesa Shemdoe. Na nimhakikishie wananchi wa Jimbo la Lupembe tuko na yeye, tunamuunga mkono sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitaongea masuala machache, Halmashauri ya Njombe *DC* kwenye Jimbo la Lupembe sisi kama jimbo tunazo changamoto nydingi sana hasa katika eneo zima la kutengewa bajeti ya Serikali Kuu. Kwenye bajeti ya mwaka 2020/2021 Halmashauri ya Njombe *DC* imepokea fedha kwa kiwango cha asilimia sita tu. Maana yake nini? Zaidi ya asilimia 90 halmashauri hii inajientesha kwa mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, ombi la wananchi wa Lupembe pamoja na kwamba Serikali yetu ina majukumu mengi inafanya na inafanya kazi nzuri ya kuhudumia Watanzania mahali pengine, tunajua sungura ni mdogo lakini pia wananchi wa Lupembe wanaiomba Serikali katika bajeti hii mpya ya mwaka 2021/2022 wananchi wa Lupembe waangaliwe kwa jicho la pekee sana hasa katika fedha za Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tuliomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya utawala. Jimbo la Lupembe kwa maana ya Halmashauri ya Njombe *DC* tumehamia kwenye halmashauri yetu kutoka Njombe Mji. Watumishi wa Halmashauri wanakaa kwenye majengo ya shule ya msingi,

hakuna vyoo, hakuna sehemu ya kula na hawana majengo ya utawala. Tunaiomba sana Serikali itoe kipaumbele kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa makao Makuu ya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, liko jambo lingine upande wa *TARURA*, tunaiomba sana Serikali waongeze bajeti zaidi kwenye Mfuko wa *TARURA*. Jimbo langu la Lupembe kwenye maeneo mengi kuna barabara za vijijini halina barabara ya lami hata kilometra moja. Wananchi wa maeneo ya Kata za Kichiwa, Igongolo na Sovi pale Mtwango barabara ni mbaya sana hazipitiki. Ziko barabara kama ya Igongolo – Ninga na barabara ya Nyombo - Ninga – Lima – Itovo - Ikondo wakati wa mvua hazipitiki, wananchi hawana zahanati wanapata shida sana. Naiomba Serikali kwenye bajeti hii watazame kwa jicho la huruma kwa ajili ya kusaidia wananchi wa Jimbo la Lupembe.

Mheshimiwa Spika, Iakini pia niwapongeze sana watumishi wa Halmashauri ya Njombe *DC* wanafanya kazi nzuri sana. Pamoja na kwamba hatupati fedha ya halmashauri kuu sisi kama halmashauri, tumekuwa tukikusanya mapato ya ndani kwa zaidi ya asilimia 100 na tunajiendesha kwa asilimia zaidi ya 90 kwa mapato ya ndani. Naiomba Serikali iwatие moyo watumishi hawa waendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine watumishi hawa wanadai fedha kwa ajili ya uhamisho kutoka Njombe Mji kwenda Njombe *DC*. Tunaomba wapewe fedha....

**SPIKA:** Mna makusanyo ya kiasi gani kwa mwaka? Mapato ya ndani Lupembe ni kiasi gani?

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ni zaidi ya shilingi bilioni moja na milioni mia tisa.

**SPIKA:** Bilioni 1.9?

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Kumbe ni hela ya kawaida tu.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ni hela ndogo sana. Kwa hiyo, naomba sana Serikali waliangalie Jimbo hili ili kusudi waweze kufanya kazi nzuri za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunao uhaba mkubwa wa watumishi wa umma. Jimbo hili kwa maana ya halmashauri tuna upungufu wa watumishi zaidi ya 442, unaweza kupata picha namna ambavyo jimbo hili liliyo na hali mbaya. Tunaiomba sana Serikali kwenye mpango huu wa bajeti mpya ya mwaka huu Jimbo la Lupembe litazamwe kwa upekee na wananchi wamenituma ndani ya Bunge lako kuja kuwanusuru wananchi hawa katika hali hii ambayo wanayo sasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, limesemwa sana humu ndani jambo la watumishi wa Serikali za Mitaa kwa maana ya Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji. Nilipokwenda kwenye kampeni na nilipokwenda kwenye ziara wananchi na viongozi hawa ndiyo wanaofanya kazi kubwa ya kusimamia maendeleo, wanaomba Serikali iwaangalie, iwape posho kwa ajili ya kujikumu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Edwin Swalle. Hivi Jimbo la Lupembe ni halmashauri gani?

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, Njombe DC.

**SPIKA:** Njombe Vijijini.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Yes.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Charles Kajege, atafuatiwa na Mheshimiwa Kirumbe Ng'enda.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami naomba niende moja kwa moja kwenye hoja zangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nilipata bahati ya kuwa katika Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa tukapitia baadhi ya gharama katika baadhi ya mikoa. Kitu cha kwanza nilichogundua ni kuwa kuna ugawaji wa rasilimali ambao hauendani na hali halisi ya wananchi. Kwa mfano, kuna ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kishapu gharama yake itakuwa *1.5 billion*, lakini ukiangalia gharama hizi zinazidi mara tatu ujenzi wa vituo vya afya ambavyo vimekubaliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nataka nijielekeze katika Jimbo langu la Mwibara kwa sababu muda ni mfupi. Naomba katika Jimbo la Mwibara tupate maji kwa sababu licha ya kuzungukwa na robo tatu ya Ziwa Viktoria lakini maeneo mengi bado hayana maji ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, vituo vya afya vilevile ni tatizo kubwa. Katika Kata za Nasimo, Kibara, Chitengule, Igundi, Nampindi, Kwikilamba, Namuhula, Butimba na Nyamiholo bado hakuna huduma nzuri za afya. Katika maeneo hayo wananchi wamejitalidi sana kujenga maboma ya zahanati. Serikali iliahidi kwamba ingemalizia, naomba Serikali itekeleze na yenyewe wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni katika barabara. Barabara nyingi za Mwibara hazipitiki lakini hasa nitazungumzia barabara moja ambayo inatoka katika Kijiji cha Buguma - Chigondo haipitiki kabisa kwa sababu mkondo wa maji umekatisha katikati ya barabara. Kama leo nikiongozana na Waziri wa TAMISEMI akienda kuona jinsi ambavyo wanawake wanavuka pale sidhani kama atafurahi. Kwa hiyo, naomba barabara hii na yenyewe ipewe umuhimu katika kujengwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni elimu. Tuna matatizo ya vyumba vya madarasa, maabara, maktaba na nyumba za

walimu. Vilevile maboma mengine ambayo wananchi wamejenga hajayakamilika, naomba Serikali itusaidie.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni kivuko kati ya Nasimo na Kisiwa cha Nafuba. Naomba Serikali itufikirie kutusaidia katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo lingine ni fidia kwa wananchi ambao walipisha mradi wa barabara ya kutoka Bulamba - Kisorya. Hawa nao bado hawajalipwa, naomba vilevile tufikiriwe.

Mheshimiwa Spika, lingine ni wakulima wa pamba. Hawa ni karibu mwaka wa tatu sasa hivi hawajalipwa pesa zao. Nafikiri Wizara husika inaweza kuangalia namna ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu ajira ziko katika maeneo makubwa mawili, kwanza ni kilimo. Bahati nzuri tunazungukwa na Ziwa Viktoria, naomba tupewe skimu za umwagiliaji maji na vilevile tupate mikopo ya matrekti.

Mheshimiwa Spika, lakini sekta nyingine ni uvuvi. Sasa hivi samaki wamekuwa wajanja huwezi ukawavua kwa kutumia zana za kizamani. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie namna ya kutusaidia kupata zana za kisasa kuliko Maafisa Samaki au Maafisa Uvuvi kuendelea kuwakamata wavuvi wetu kwa kutumia zana za zamani.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine naiomba Serikali kuangalia ulipaji wa madeni kwa wale waliota huduma Serikalini. Kwa mfano, nina kampuni mbili za jimboni kwangu; moja ni *Swahili Ceramics*, hawa wanaidai TBA zaidi ya milioni 139 kuanzia mwaka 2017 hawajalipwa, naomba Serikali ichukue hatua. Kampuni nyingine ni *Wajenzi Enterprises* ambao wanaidai Halmashauri ya Gairo milioni 10.5. Hawa nao wanasumbuliwa, naomba nao waangaliwe.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia halmashauri ya kwetu ambayo ni ya Majimbo mawili ya Mwibara na Bunda Vijijini;

ili uweze kwenda katika Jimbo la Bunda Vijijini inabidi uvuke Jimbo la Bunda Mjini. Ushauri wangu naomba Bunda Vijijini na Bunda Mjini wawe katika halmashauri, moja sisi Mwibara tubaki peke yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa muda huu, naomba na mimi niunge mkono hoja hii. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Kajege. Pendekazo zuri hilo; Bunda Vijijini na Bunda Mjini iwe halmashauri moja, Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Ester Bulaya hapo patawaka moto.

Tunaendelea na Mheshimiwa Kirumbe Ng'enda atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Mahawanga.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nami naungana na Wabunge wenzangu waliotangulia kuonesha imani yetu kubwa sana kwa viongozi wa Wizara hii ya TAMISEMI, Waziri, Naibu Mawaziri pamoja na Makatibu Wakuu na wasaidizi wote. Tuna matumaini makubwa sana katika utendaji wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijazungumza mambo ya kijimbo, nilitaka nizungumze haya ya kisera kidogo na hasa ni utaratibu wa kupeleka fedha za maendeleo katika halmashauri zetu. Tulipokuwa kwenye vikao vya RCC tumekutana na tatizo kubwa sana na tatizo lenyewe ni utaratibu mpya nafikiri uliotolewa na Hazina wa kutaka fedha za maendeleo zitolewe baada ya kuwa kandarasi za kazi zinazotaka kufanyika katika mpango kazi zimetangazwa na wataalamu wameandikia na kwenda Hazina. Sasa utaratibu huu umechelewesha sana miradi mingi ya maendeleo kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha wa 2019/2020 katika Mkoa wa Kigoma ni asilimia 78 tu ya fedha za maendeleo ndiyo zilizopelekwa lakini mwaka huu ndiyo hatari zaidi maana mpaka tunakwenda kumaliza robo ya tatu ya

mwaka ni asilimia 23.3 ya fedha zote za maendeleo ndiyo zimeletwa. Tatizo kubwa limetokea wapi? Ni uhaba wa wataalamu hasa wahandisi ambao wanashughulika na kuchakata miradi hii ili ipelekwe Hazina kwa ajili ya kuombewa fedha.

Kwa hiyo, labda kama tunaona kuna ugumu wa kuwapata hawa wataalamu kwa wakati kwenye halmashauri zetu na kwenye Sekretarieti ya Mkoa basi turudi kwenye utaratibu wa zamani ambapo pesa zilikuwa zinatolewa Hazina kupelekwa mikoani na kwenye halmashauri kwa kuzingatia mpango kazi. Kama mpango umeshatoka na kasma imeshapitishwa na Bunge, pesa zipelekwe mchakato wa miradi ufanyike huko kuliko huu utaratibu wa sasa unachelewesha sana fedha kufika kwenye maeneo yale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda nilizungumze, mimi natoka Manispaa ya Kigoma Ujiji. Sisi ambao tunatoka katika miji tuna maeneo yetu ya mapato na wale wanaotoka katika vijiji wana masuala ya mazao, mifugo na kadhalika, wanakuwa na maeneo mapana ya mapato. Moja ya eneo kubwa tunalolitegemea katika mapato kwenye halmshauri zetu ni masoko. Nimeona Serikali imefanya kazi nzuri katika baadhi ya maeneo ya kujenga masoko ya kisasa lakini Manispaa ya Kigoma Ujiji bado eneo lake la kukusanya mapato hili la masoko halijaboreshwaa.

Mheshimiwa Spika, tungeomba Wizara ya TAMISEMI waone uwezekano wa kusaidia ili tuweze kupata masoko yaliyopangiliwa na yaliyokaa kisasa na ambayo ni rahisi kudhibiti mapato yake. Nasema hili hasa ukizingatia kwamba Manispaa ile iko mpakani, meli zinakuja pale za kutoka Kongo, Burundi, waone hata nchi yetu unajua wengine hawajui Dar-Es-Salaam hawajui Dodoma, akifika pale akiona soko la hovyo anasema hivi Tanzania tunavyowaona walivyo soko lao ndiyo hili? Wenyewe wanasema ndiyo soko la Tanzania. Sasa mnatupa kazi ya kuanza kujieleza aah, kuna Kariakoo, kuna wapi, wenyewe hawajui. Kwa hiyo, tunaomba mtusaidie sana katika suala la kupata soko la kisasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Kigoma Ujiji ni miongoni mwa Halmshauri ambazo hazina hospitali ya wilaya na mpaka sasa tunatumia hospitali ya Shirika la Dini la *Babtist*. Kwa sababu Serikali ni moja nilitaka niseme hili kwamba tumekwishakubaliana kule na sasa hivi tumepata eneo la kujenga hospitali ya rufaa ya mkoa, najua hii iko Wizara ya Afya, lakini ni kwamba hospitali hii ikipatikana hospitali ambayo inatumika sasa kama hospitali ya rufaa ya mkoa inaweza ikawa hospitali ya wilaya ikasimamiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji. Kwa hiyo, niombe tu Wizara hizi zinaweza zikafika mahali zikafanya mashauriano ya kusaidia kuharakisha ujenzi wa hospitali ya rufaa ya mkoa ili hospitali iliyokuwa inatumika kama hospitali ya rufaa ya mkoa ya Maweni iweze sasa kubaki kama Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji.

Mheshimiwa Spika, nimalizie mchango wangu kwa kuzungumzia suala la upandishaji wa vyeo watumishi. Katika Manispaa ya Kigoma Ujiji lipo tatizo kubwa sana, Watendaji wa Kata na Mitaa walioajiriwa Julai 2005 sasa wana takribani miaka 16 hawajapandishwa vyeo. Naomba mltazame suala hili.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Janeth Mahawanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya TAMISEMI. Kwanza niipongeze Wizara kwa wasilisho zuri na vipaumbele vizuri kabisa ambavyo kama vitaenda kutekelezeka nina uhakika tutapata matokeo chanya na changamoto zote kwenye jamii yetu zitakwenda kwisha.

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye mikopo hii ya asilimia 10 ambayo wanufaika ni akinamama, vijana na walemauvu. Lengo la Serikali kwa mikopo hii lilikuwa zuri sana lakini uhitaji ni mkubwa kuliko pesa yenye na hii inatokana

na baadhi ya pesa inayotoka kuwa hairudi. Je, halmashauri zetu zinafanya tathmini ya kuangalia ni kiasi gani kimetoka na kiasi gani kimerudi na kwa nini hakijarudi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, wanufaika wa pesa hii kuna kitu wanakikosa ambacho ni muhimu sana, wanakosa elimu. Akina mama wengi ni wajasiriamali ambao wanafanya shughuli za kijasiriamali kama usindikaji wa vyakula, lakini wanafanya kwa elimu yao binafsi, kwa uzoefu wao wa kufundishana wenyewe kwa wenyewe. Ningezionba halmashauri zishirikiane na taasisi ambazo zinaunga mkono juhudzi za kuwainua wananchi kiuchumi, hasa wajasiriamali wa chini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano unakuta kuna matangazo ya *SIDO* yanayotoa elimu ya ujasiriamali hasa upande wa usindikaji, akina mama wengi wanatamani kwenda kusoma mafunzo haya lakini wanashindwa kutokana na kukosa ada. Halmashauri kama itaandaa utaratibu mzuri ikapata wadau kutoka *SIDO*, kutoka kwenye benki wataalam wa mambo ya fedha, wataalam wa masoko, wataalam wa fursa na wataalam wa kuongeza thamani ya bidhaa za wajasiariamali wadogo wakashirikiana na Maafisa Maendeleo na Madiwani wetu kwenye kata wakapita kwenye vikundi vile vya akina mama, vijana wakatoa elimu hii, nina uhakika itasaidia sana. Tunasema tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda, tunatafuta vyanzo vingine vya mapato, lakini nina uhakika kabisa mikopo hii ni chanzo tosha cha mapato kama tutawaongezea thamani ya ujuzi wanufaika hawa wakaweza kuwa wajasiariamali wakubwa wakalipa kodi, tutapata mapato kwenye Serikali yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kuna kundi lingine la vijana ambao wanamaliza vyuo vikuu wako mtaani hawana kazi. Halmashauri ina uwezo kabisa wa kuangalia mikopo hii ya asilimia 10 ikachukua kundi fulani la vijana *at least* kundi moja kama kikundi kutoka kwenye kila halmashauri wakawapeleka kupata elimu. Kuna taasisi tano zimeungana ambazo ni *SIDO*, *VETA*, *NSSF*, Baraza la Uwezeshaji Uchumi Wananchi na Benki

ya Azania, hawa wanatoa elimu baadaye wanatoa mikopo kwa ajili ya viwanda vidogo kuanzia milioni 50 mpaka milioni 500. Vijana wanaomaliza chuo wakichukuliwa na halmashauri, wakasimamiwa kupata elimu hii kwa kulipiwa huko *SIDO* au *VETA* wakaweza kufungua kiwanda wataweza kuajiri vijana wenzao, watatoka kwenye wimbi la kukosa ajira na mwisho wa siku watakuwa walipa kodi wataongeza mapato kwenye Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niombe halmashauri zetu zishirikiane na benki. Benki nyingi zina bidhaa nzuri sana kwa ajili ya wajasiriamali wadogo, lakini wajasiriamali wengi wanakosa taarifa. Kama halmashauri wataweza kushirikiana na hizi benki ambazo zinainua wajasiriamali wadogo zikapita kwenye kata zetu akina mama, vijana na walemavu wakapata taarifa sahihi wakatumia kile kidogo walichokipata kutoka kwenye ile asilimia 10 hawa watu wanakwenda kuinuka. Ni aibu kuona kijana anakuwa machinga ndani ya miaka kumi. Kijana huyo alitakiwa awe ameshatoka kutoka kwenye ujasiriamali mdogo wa kupita barabarani akaweza kukaa kivulini akawa mlipa kodi mzuri, Serikali itaongeza mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitoe ushauri kwa Wizara ya TAMISEMI. Kuwe na *training* pia za ndani kwa viongozi wetu kuanzia ngazi ya mkoa, wilaya, kata mpaka viji. Viongozi hawa wote wajione wao ni kitu kimoja na wanatembea kwenye safari moja, wanatakiwa wafanye kazi kama timu. Mkuu wa Mkoa ni mteule wa Rais, Mkuu wa Wilaya ni mteule wa Rais, Mkurugenzi ni mteule wa Rais, sasa kama hawa watu hawatakuwa kitu kimoja wakaanza kusigma wenyewe kwa wenyewe misuguano ile waathirika ni wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwananchi anapokuwa na tatizo lake ambalo linatakiwa kuwa solved kwa Mkuu wa Mkoa au kwa Mkurugenzi, lakini...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Janeth.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nimeshakutaja Mheshimiwa Munde Tambwe na Mheshimiwa Innocent Kalogeris ajiandae.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia Wizara ya TAMISEMI. Niungane na wenzangu kumpongeza Waziri wa TAMISEMI na kusema kwamba Wabunge tuna imani naye kubwa kwamba atafanya kazi nzuri kwa sababu tunamfahamu ni mchapa kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kuipongeza Serikali kwa kutuletea pesa nydingi ndani ya Manispaa ya Mkao wa Tabora. Mimi ni Diwani ndani ya Manispaa ya Tabora ndiyo maana naongea sana kuhusu Manispaa, lakini pia ni Mbunge wa Viti Maalum wa mkoa mzima. Tulikuwa tunahangaika sana jengo la utawala kwa muda mrefu lakini bajeti hii imetuonesha kwamba tumepewaa shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi huo, lakini tumeletewa bilioni moja, mia moja hamsini kwa ajili ya hospitali ya wilaya na zahanati tatu; Zahanati ya Igosha, Igombe na Ituru, tunashukuru sana Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kubwa kabisa ambalo tuna shida nalo sisi wananchi wa Mkao wa Tabora, la kwanza nimwambie Mheshimiwa ndugu yangu Mheshimiwa Ummy, tuna shida ya kukata Mkao wa Tabora. Mkao wa Tabora ni mkubwa, ni mkoa wa zamani, una historia kubwa, lakini haujawahi kukatwa. Imekatwa Mikoa midogo na Mkao wa Tabora umeachwa.

Nimwambie Mheshimiwa Waziri, Mkao wa Tabora, Tanga na Morogoro ndiyo mikoa pekee haijifikatwa na inasababisha kutopata huduma sawa sawa kwa wananchi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, mikoa hii mitatu na yenyewe ikatwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Tabora Mjini lina *population* karibia watu 400,000, lakini ni Jimbo moja lenye Kata 29. Namwomba Mheshimiwa Waziri apitie majimbo yote aone kipaumbele gani kilitumika kukata haya majimbo? Kuna majimbo yana Kata sita, yana *population* ya watu 20,000 mpaka 30,000 na kuna jimbo lina watu 400,000. Serikali imetumia mchakato gani kupata haya majimbo? Hiki kitu kinaleta maswali mengi. Unakuta mtu anakata sita... (*Makofii*)

**SPIKA:** Hiyo hoja muhimu sana hiyo, maana Kongwa ina watu 400,000 Jimbo moja, endelea Mheshimiwa. (*Makofii*)

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Hata naongea hapa na Naibu Spika, anasema yeye kwake ana kata 36 zenye *population* zaidi ya watu 500,000. Tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri, hata kwake Tanga Jimbo lile ni kubwa. Sasa yeye labda ataona aibu kujikatia Mheshimiwa Waziri, lakini sisi utukatie. (*Makofii*)

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa jitaje.

## TAARIFA

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, naitwa Stella Ikupa. Naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Munde kwamba hata Dodoma Mjini ina kata 46. (*Makofii*)

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Ikupa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tumwombe Mheshimiwa Waziri apitie majimbo yote na aangalie vigezo. Kama Mheshimiwa Waziri kuna jimbo dogo dogo yaunganishe. Kwa kweli kama nia ni njema na kama mnataka kufuata ukweli, majimbo makubwa myakate.

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye masuala ya watumishi. Tabora Manispaa tuna shida moja; Tabora inaitwa Tabora Manispaa, lakini tuna Kata 12 ziko vijjini. Kwa hiyo, tunapokwenda kwenye mgao wa walimu, tunaambiwa hii ni Manispaa, ina walimu wengi, lakini tuna Kata 12 zina uhaba mkubwa wa walimu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nimeongea na Afisa Utumishi anipe idadi kwamba tulikuwa tunatakiwa kuwa na walimu wangapi kwenye ikama na tunao wangapi; lakini nilikuwa njiani nimechelewa kupata. Pia watumishi wa Afya kwenye zile Kata 12 ambazo zipo vijjini ambazo zipo ndani ya Manispaa pia watumishi ni wachache sana, tunaomba msaada wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imetuletea fedha nydingi za barabara na ujenzi wa majengo chungu nzima, lakini tuna watumishi wachache sana wa ujenzi. Kwa mfano *civil engineer, quantity surveyor* na *ma-technician* wa ujenzi wamekuwa wachache sana kwa sababu tunashindwa kusimamia miradi, hakuna watumishi wengi kama inavyotakiwa kwenye ikama yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pale Tabora tuna Kituo cha Afya kikubwa sana Serikali imetujengea, kina majengo matano, lakini majengo matatu yanafanya kazi. Jengo la *operation halifanyi* kazi kwa sababu hakuna vifaa vya *theatre*. Kila kitu kimekamilika, bado vifaa vya *theatre*. Naiomba sana Serikali ituletee vifaa vya *theatre* kwenye zahanati yetu ya Mailitano. Pia tuna jengo la *Mortuary* ambalo tunashindwa kulitumia kwa sababu hakuna yale *ma-freezer* makubwa ya *mortuary*. Mheshimiwa Waziri nadhani umenisikia, tunakuomba sana, sana, sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunayo Hospitali yetu ya Wilaya, Serikali imetuletea fedha nydingi, lakini bado hatujapata fedha kwa ajili ya vifaa tiba kwa ajili ya hospitali yetu ya Wilaya. Niiombe sana Serikali iweze kutuletea fedha kwa ajili ya vifaa tiba vya hospitali ile ya Wilaya, kwa sababu mpaka sasa wananchi wa Manispaa ya Tabora wanatibiwa

kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora. Wanababisha msongamano mkubwa, wanababisha lawama kubwa kwa madaktari kuonekana hawafanyi kazi ipasavyo, lakini ni kwamba hatuna Vituo vya Afya hatuna Hospitali ya Wilaya; na pale ni mjini *population* ni zaidi ya watu 400,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Munde Tambwe. Mheshimiwa Innocent Kalogeris, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Niendeleze hapo hapo alipozungumza dada yangu Mheshimiwa Munde Tambwe. Mkoa wa Morogoro tunaomba ukatwe ipatikane mikoa miwili. (*Makofi/Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Ugawanywe.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Nimeelekezwa ni ugawanywe.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Morogoro ugawanywe ipatikane mikoa miwili ambapo kutakuwa na Wilaya ya Morogoro, Wilaya ya Mvomero, Wilaya ya Gairo na Wilaya ya Kilosa; na kwingine kutakuwa na Wilaya ya Ulanga, Wilaya ya Malinyi na Wilaya ya Kilombero. Tupate mikoa miwili ili kuweza kurahisisha kupata maendeleo katika Mkoa wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana dada yangu Mheshimiwa Ummy kwa uteuzi ambaao ameupata katika Wizara hii mpya. Ni imani yangu kwamba yeeye na wasaidizi wake; Manaibu wake watafanya kazi kubwa kama ile alioifanya akiwa Wizara ya Afya wakati wa mapambano ya *Corona* na tukashinda, naamini kabisa kwamba TAMISEMI atafanya vizuri zaidi. Hizi changamoto zote

pamoja na mafanikio yote, lakini changamoto hizi tutakwenda kuzimaliza.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la barabara. Mimi ni Mkandarasi. Katika uhalisia, Wilaya ya Morogoro Halmashauri yetu ina eneo la *square* mita 11,731, ina barabara zenye urefu wa kilometra 750, ina madaraja makubwa 29, ina *ma-box culvert* 74, lakini mgao wake tunapata shilingi bilioni 1.1. Ni kwamba kwa namna moja au nyiningine, tunatengeneza kilometra moja tu bila kugusa makalavati wala nini kwa shilingi milioni moja.

Mheshimiwa Spika, kama Mkandarasi, barabara ya changarawe ili iweze kuitika ikiwa na madaraja au *box culvert*, unahitaji kilometra moja kwa shilingi milioni 30. Sasa naomba tu, ndugu yangu Mheshimiwa Zungu amezungumza, Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Miundombinu Mheshimiwa Kakoso amezungumza, tuangalie jinsi gani tunaisaidia *TARURA*. Katika kuisaidia *TARURA*, naomba, hawa wenzetu wamekokotoa, wamechanganua, ni kwamba kutakuwa na uwezekano wa kila mwaka kupata shilingi milioni 500. Katika hilo suala la Mwenyekiti wangu ndugu yangu Mheshimiwa Kakoso, kila mwaka tutakuwa tunapata shilingi triliioni 2,160. Naomba Serikali ichukue mawazo haya na ikayafanyie kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika shilingi triliioni 2,160 ukizigawa kwa Halmashauri zetu, tutakuwa na uhakika wa kila mwaka kupata kila Halmashauri shilingi bilioni 11. Shilingi bilioni 11 ukipeleka kwenye Halmashauri, ndani ya miaka mitano, tatizo la *TARURA* litakuwa halipo tena hapa Bungeni. Kwa hiyo, naiomba Serikali tu, mama yangu Mheshimiwa Ummy, Waziri wa Fedha na wengine wote wanaohusika, lisimamieni hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitakupa kichekesho kimoja, lakini siyo kizuri. Juzi mliona katika mitando, wale watu waliokuwa wanatembea uchi, wametoka jimboni kwangu. Kilicho jitokeza, watu huwa wanavua nguo wanapopita kwenye barabara za umande, wanazihifadhi nguo zao. Kwa

hiyo, naomba tu, tunadhalilika. Jimbo la Morogoro Kusini eneo kubwa ni milima, kwa hiyo, shida yetu kubwa ni barabara. Tunawaomba mtusaidie katika hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna suala la maboma, ndani ya Halmashauri yetu tuna maboma 170 yanashibiri kumaliziwa, tunaiomba Serikali sijui dada yangu Mheshimiwa Ummy katika bajeti ya mwaka huu umetutengea kiasi gani? Tunaomba tufanya jambo hilo ili zile nguvu ambazo wananchi wamezitumia zikakamilike na waone faida yake. Tutaendelea kuwahamasisha kufanya mambo mengine, lakini kama haya hatujawakamilishia wataona kama vile tunawapotezea nguvu zao. Kwa hiyo, katika bajeti hii sijui Halmashauri yetu umetutengea kiasi gani, lakini tunaomba maboma yakamilike.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumza ni kwenye masuala ya madeni ya watumishi. Katika Halmashauri yetu watumishi wanadai karibu shilingi bilioni mbili. Watu hawa wanajitoa kwa hali na mali katika kufanya kazi, inapofika mahali hatuwezi kuwapatia fedha ambayo ni stahiki yao, tunakuwa hatuwatendei haki. Nawaomba katika bajeti hii, fedha zitengwe watu wapate haki zao ili waweze kututumikia vizuri vile inavyopasa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, namwomba dada yangu Mheshimiwa Ummy au wasaidizi wake, tukimaliza bajeti twende wote wakaone uhalisia wa Jimbo la Morogoro kusini na Halmashauri ya Morogoro jinsi gani ilivyo ili wakija katika bajeti ijayo wawe na mpango uliokuwa sahihi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Innocent Kalogeris kwa mchango wako mzuri. Sasa nilimtaja Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, halafu Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo atafuata.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia. Kwanza

naomba nimpongeze Waziri wa TAMISEMI na Manaibu wake, pia Katibu Mkuu na Manaibu wake wa Afya na Elimu. Sisi Wabunge wote humu tunalia na *TARURA*. Tusikilizze ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ili uchumi wa viwanda uendelee tunahitaji barabara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tunazo barabara nyingi ambazo ni muhimu kwa kusafirisha mazao ya wakulima na tunapoangalia uchumi, tunawaangalia hasa wakulima ambao wanaweza kusafirisha mazao yao. Kwa hiyo, naomba sana *TARURA* iongezewe fedha na michango ya Wabunge inayozungumzwa kuongeza tozo kwenye simu, hilo lisikilizwe. Hatuna ubabaishaji kwa sababu hatuhitaji kukaa miaka 40 bila kujenga barabara zetu. Tunahitaji kukaa miaka mitano tumalize barabara zote za wananchi ili uchumi uweze kukua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuongeze tozo kwa sababu wanaosafiri ni hao hao wananchi, wanaotaka maendeleo ni hao hao wananchi. Kwa hiyo, tuongeze tozo kwenye mafuta pamoja na mitandao ili kuhakikisha kwamba barabara zetu zinajengwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninayo barabara muhimu sana ya Isolo, Kabilia Isawida ambayo inahudumia Wilaya ya Itilima pamoja na Magu. Ninayo barabara ya Kisamba - Sayaka ambayo inahudumia barabara ya Wilaya ya Busega pamoja na Magu. Ninayo barabara ya Mwamanga kisasa 'B' ambayo nayo kwa kweli ni barabara muhimu sana katika uchumi wa Wilaya ya Magu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na ahadi ya Mheshimiwa Rais Hayati Dkt. Magufuli ya kuboresha barabara ya Bujora - Kissesa kwenye makumbusho ya Wasukuma, imejengwa kilometra 400 bado kilometra 1.3. Naomba iingizwe kwenye barabara ambazo zitawekewa lami katika miji hii midogo midogo. Pia tunapoboresha miji na majiji tukumbuke pia kwenye Halmashauri zetu, nasi tunahitaji kuwekewa barabara za lami kwenye Wilaya zetu ili angalau wananchi waweze kupata huduma za kutosha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Afya tumefanya kazi kubwa sana, lakini wenyewe umri wa kwangu miaka 47, ni muhimu sasa nikapatiwa fedha ili tuweze kuikarabati hospitali hiyo na yenye ioneokane kwamba ni hospitali ya kisasa. Pia kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kugawa Wilaya ya Magu pamoja na Wilaya ya Misungwi na Nyamagana kidogo kuwa Wilaya mpya ya Kisesa. Hii Wilaya nayo inategemewa ianze ili kusogeza huduma kwa wananchi wetu. Tumejenga vituo vya afya, kinachohitajika sasa ni vifaa; *X-Ray* pamoja na *cold room* katika Kituo cha Afya cha Tangala pamoja na Kabilia na Lugeye ili kuhakikisha kwamba vinatoa huduma iliyo nzuri. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mradi wa *P4R* wa kujenga madarasa umeleta matumaini makubwa sana kwa Watanzania, umepunguza uhaba wa madarasa katika shule zetu. Ushauri wangu ni kwamba, fedha hizi kama itawezekana, kwa sababu kuna maboma ya wananchi, kwa sababu fedha hizi zinapokuja, kwanza zinakwenda kujenga maboma mapya. Kwa sababu tuna maboma ya wananchi ambayo yameshajengwa tayari, fedha hizi ziwe zinamalizia. Sikija shilingi milioni 20 zimalizie maboma mawili, tunakuwa na madarasa mawili badala ya kujenga darasa moja. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ninalo jengo la Halmashauri. Mwaka huu wa fedha tuliomalizia lilitengewa shilingi milioni 750, tumeletewa shilingi milioni 136, ni vizuri fedha ambazo zimebaki ziletwe ili tuweze kuendeleza ujenzi ule. Bajeti ya mwaka huu umetutengea shilingi bilioni moja.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga, muda *washilaga*.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Ahaa!

**SPIKA:** Mmh!

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mhesimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja nikiamini kwamba Wizara hii Waziri na Makatibu Wakuu na Watendaji wadogo wadogo kama akina Ntuli na akina Cheyo wanafanya kazi. Ni Wizara barabara, itakwenda *bam bam*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Huyu mtani wangu Kiswaga huyu! Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote, nampongeza sana Waziri Mheshimiwa Ummy pamoja na timu yake siyo tu kwa kuwasilisha bajeti yao vizuri sana, maana yake kwa kweli wamewasilisha vizuri, lakini pia hata kwa kazi ambazo tumeshawaona wakizifanya ndani ya muda mfupi toka wameingia kwenye nafasi hizo, nikiwatazama hawa naona matumaini kama ninavyoitazama timu yangu ya Simba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naungana na wote waliozungumza juu ya kuongezea nguvu *TARURA*, suala la dawa kwenye Hospitali zetu, watumishi mbalimbali na kuwaongezea uwezo pia Madiwani wetu, hayo yote nayaunga mkono kwa asillimia mia moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye Jimbo langu la Mwanga, naomba kusema kwamba ipo ahadi ya Hospitali ya Wilaya iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni. Kama alivyosema Mheshimiwa Rais, Mama Samia, ye ye na Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli ni kitu kimoja, kwa hiyo, kwa vile Mheshimiwa Dkt. Magufuli alitoa hiyo ahadi, basi ahadi hii ni ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na tunaiomba itekelezwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mwanga walirukaruka sana baada ya kupewa ahadi hiyo kwa sababu ilikuwa ni kilio cha muda mrefu, wakaibana Halmashauri yao, ikatenga ekari 54 za ardhi ambazo zipo tayari kwa ajili ya

mradi huo. Namkaribisha Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu watuletee huo mradi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili juu ya sekta ya afya, ni Kituo cha Afya cha Kigonigoni ambacho ni moja kati ya vituo vya mkakati. Serikali ilileta kwanza shilingi milioni 400 kikajengwa kikafikia hatua iliyofikiwa, lakini tangu hapo kimesimama. Yale majengo na vitu vingine vyote vilivyojengwa vinazidi kuharibika. Tusipomalizia kile kituo cha afya tutazidi kupata hasara na wananchi wa Kata ya Kigonigoni na maeneo yote ya ile Tarafa ya Jipendea watateseka kwa sababu walikuwa na matumaini makubwa ya kituo hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo mawili ya Jimbo langu la Mwanga, yapo mengi, lakini mengine ninaamini Mheshimiwa Waziri na timu yake watakuja kuyaona na mengine tutazungumza, nizungumze moja tu la Kitaifa. Nina imani kabisa hili suala la matumizi ya *force account* yanaweza yakatupeleka mbali, lakini tukitaka mafanikio makubwa kwenye suala hili ni vizuri basi Halmashauri zetu zikawa na jopo zima linalohusika na ujenzi. Lazima Halmashauri ziwe na *ma-architect, ma-quantity surveyors* na *ma-engineer*. Bila hivyo miradi hii itakuja kutupa shida baadaye.

Mheshimiwa Spika, tungependa majengo haya yanayojengwa wajukuu zetu wayakute, lakini kwa mfumo huu wa kumwachia *engineer* peke yake au pengine hata *engineer* hakuna, asimamie mradi ya shilingi bilioni moja, kwa kweli hatuwezi kufika vizuri. Wataalam wa ujenzi walitengeneza mfumo wa jopo linaloweza kusimamia kazi ya ujenzi hata mikataba ambayo inatumika kwa nchi nzima; mikataba ya *FIDIC* na *NCC* yote inazingatia kwamba lazima kuwe na jopo la hao wataalam ili kazi iende vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati tunasubiri kupata wataalam hao, Serikali inaweza kuamua kutumia bodi mbalimbali za wataalam wa hizi fani kama *CRB, AQRB, ERB* hiso zote zinaweza zikaratibu kwa kutumia wataalam waliopo

kwenye zone mbalimbali ili kuhakikisha miradi hii inasimamiwa vizuri ili tuweze kupata *value for money*.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Wizara hii ni moyo wa maendeleo, yapo mengi ambayo tunaweza tukasema, lakini kwa timu hii ambayo Serikali imetupatia, tunaamini watakuja huko kuyaona ili tuweze kufanya mambo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge. Ningekuwa na nusu saa zaidi ningeweza kuwachukua wote. Tumejitahidi sana kwa *marathon* kubwa, lakini haiwezekani kwa wote. Tuvumiliane, wale waliokosa nafasi hapa, tutawapa kipaumbele kwenye bajeti nyingine kuanzia kesho. Tutaendelea jioni ya leo ambapo Mheshimiwa Waziri wa Afya ataanza, halafu Waheshimiwa Manai bu na mtoa hoja pia atahitimisha. TAMISEMI ina mafungu mengi; kuna Mikoa 26, nao wenyewe wana mafungu mawili mengine makubwa.

Kwa hiyo, tuna kazi kidogo ya kuifanya jioni ya leo, huenda hata tusiweze kutumia muda wetu vizuri. Kwa hiyo, tuwahi kurudi tuone nini kinawezekana kwa jioni hii ya leo. Naomba Kamati ya Uongozi tukutane *immediately* baada ya hapa, kwenye ukumbi wa Spika hapa nyuma yangu.

Basi kwa vile shughuli za asubuhi hii ya leo zimekamilika, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni ya leo.

(*Saa 7.02 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 10.00 Jioni*).

(*Saa 10.00 Jioni Bunge Lilitrudia*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa tunaendelea na *session* hii ya jioni, ina mambo mengi lakini tujaribu ku-*coup* hivyo hivyo.

Sasa muda wetu ulivyo hapa tunaanza na Waziri wa Afya, kati ya dakika tano hadi 10 isizidi hapo.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kutoa mchango wangu kwenye kuelekea kuhitimisha mjadala huu wa hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuonyesha utayari na dhamira yake kubwa katika kuboresha sekta ya afya kwa manufaa ya wananchi.

Katika kipindi kifupi cha uongozi wake kama Rais achilia mbali historia yake ya awali ya kuitendea haki sana sekta hii tayari ameshafanya maamuzi makubwa mazito katika kuimarishe Sekta hii ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Spika, Baadhi tu ya maamuzi aliyoafanya ni mtaji na msingi muhimu sana katika maendeleo endelevu ya sekta hii, ambapo kwanza amemteua Naibu Waziri mahsus kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi jambo ambalo litaimarisha sana uwezo wa sekta hii kuwagusa wananchi wa makundi haya ya jamii yaliyo msingi wa maendeleo ya Taifa (Wanawake, Watoto, Wazee na Vijana na masuala yote ya usawa wa kijinsia).

Mheshimiwa Spika, *breaking news* nzuri kabisa, Mheshimiwa Rais ameridhia na ametoa bilioni 80 mwaka huu mwezi huu Aprili 2021 ziende kuimarishe eneo la upatikanaji wa dawa, vipimo na vifaa tiba, eneo ambalo limezungumzwa kuwa kero kubwa sana kwa wananchi wetu sasa hivi. Utaratibu wa kununua dawa hizi haraka sana unaendelea ili tuzifikishe mahali sahihi. Hii ni nyongeza ya fedha iliyotolewa

kipindi cha Julai mpaka Desemba ya bilioni 43, zikaongezwa nyingine kama 18 jumla bilioni 59 ambazo zilishaenda, ziko huko zinaendelea kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Spika, vilevile kama ambavyo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI alitoa taarifa Bungeni hapa Mheshimiwa Rais pia ametoa maelekezo kwamba, ujenzi wa hospitali za Halmashauri kwenye maeneo ambayo zilikuwa hazijajengwa uendelee. Kwa hiyo utaona ni namna gani Mheshimiwa Rais amejitoo kuimarisha sekta hii, nasi tunampongeza. Katika kipindi cha muda huu mfupi ambao amekaa inabidi sasa sisi tumuunge mkono na Wizara yangu itashirikiana sana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhakikisha kwamba hatumwangushi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue sasa fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kuteuliwa kwake kushika nafasi hii nyeti ambayo ni mhimili wa huduma zote nchini ikiwemo huduma za afya, maendeleo ya jamii, jinsia wazee na watoto wanakoishi ambao 70% ya wananchi wote wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa hotuba yake nzuri ambayo imegusa vizuri sana utashi wa kisera tunazozitoa sisi Wizara ya Afya na miongozo ya kisera katika kuendeleza sekta hii ngazi ya afya ya msingi. Wizara yangu itatoa ushirikiano wa kila namna kuhakikisha kwamba maendeleo ya sekta hii ngazi ya halmashauri yanatimia sambamba na sera inavyosema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani kwa Wabunge wote waliochangia mambo mbalimbali ambayo mengine yamekuwa ni michango darasa kwa wataalam wote wa sekta ya afya tulio ngazi zote. Tuwaahidi kwamba tutayafanyia kazi, machache nitayataja hapa kama matano tu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile alichangia kwenye masuala ya rasilimali watu yaani

kuna upungufu wa rasilimali watu ambapo sasa Wizara imepokea hoja hii na inatambua upungufu mkubwa wa watumishi na imewasilisha maombi ya bajeti kwa mwaka huu 2021/2022 tunaouendea takriban bilioni 144 kwa ajili ya kuwaajiri watumishi wasiopungua 2,775 tunaamini kwamba bajeti hii itapitishwa na sisi pia hatutakuwa wachoyo tutakaa na TAMISEMI kuangalia kwamba tunawatumiae hawa watumishi hasa waweze kugusa maeneo yale ambayo tumeyapigia kelele kwamba vituo vimejengwa na havifanyi kazi bado.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ajira hizi Wizara imebaini kuwa kuna haja ya kuimarisha uwajibikaji wa watumishi waliopo katika vituo vyetu. Kwanza kuwapangia maeneo kwa tija na kuwapa motisha waweze kufanya kazi kwa moyo Zaidi. Hivyo, tutashirikiana na Wizara zote za kisekta ikiwepo Utumishi na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kuja na mpango wa jinsi gani watumishi wetu wanaofanya kazi vizuri watambuliwe kokote waliko, maana suala lingine kuwa na watumishi na suala lingine watumishi wale kuwa *productive, efficiency* inakaaje.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya miundombinu ya afya, Wizara imesikia hitaji la kumalizia ujenzi wa miundombinu na kukarabati ile ya zamani pamoja na kuweka vifaa tiba stahiki, mitambo mbalimbali ya huduma za afya na magari ya wagonjwa (*ambulance*). Kwa kuwa Wizara yangu inahusika na kutafuta rasilimali toka vyanzo mbalimbali ikiwemo kuwashawishi wadau wa maendeleo waweze kutoa fedha, tutatekeleza jukumu hilo kwa nguvu zote na rasilimali tutakazopata tutazielekeza katika siyo tu hospitali za rufaa za mikoa kanda na Taifa bali tutalenga kuimarisha vituo hivi vya afya vya ngazi ya msingi kwenye halmashauri ili kupunguza rufaa za kwenda kwenye hospitali kubwa za kibingwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, tutabuni mbinu nyingine mbalimbali za kuwashirikisha wadau wetu hasa sekta binafsi ili pale tunapokuwa na ufinyu wa bajeti kuitipia *PPP* tuweze kuhakikisha tunakaa vizuri, wananchi wetu hawa

tunaowapeleka kwenye bima ya afya kwa wote waweze kunufika na kuona faida ya huduma hizi wakiwa na bima hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu dawa na vifaa tiba na vipimo, kama nilivyosema tumepata hizi fedha na Serikali imekuwa ikijitahidi kuwekeza fedha nyingi, lakini sasa Wizara imeenda mbali kufuutilia nini hasa kinajiri eneo hili. Tumebaini changamoto nyingi huku zikiwa zinaweza kuепukika, kuanzia kwenye mfumo wa manunuzi changamoto za watumiaji, ikiwemo namna wanavyosimamia mtaji wa bidhaa za afya na bidhaa zenyewe zinapofika mikononi mwao kule kwenye vile vituo.

Mheshimiwa Spika, changamoto zingine ni namna gani watumishi wetu wamejiandaa kutoa huduma kwa weledi wenge mvuto *customer care* ili watumiaji wanaofika kwenye vituo vyetu wasiwe tu wale wa msamaha, waje na wale wanaoweza kulipa na wenge bima. Hili eneo tutashirikiana kulifanya kazi ili hawa wanaoajiriwa wakawe na tija.

Mheshimiwa Spika, hivyo tutatendea haki utafiti huu na yatokanayo yake kwa Kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambapo tumeshabaini maeneo yetu ya kufanya kazi hususan uwajibikaji dhidi ya vitendo vya ukosefu wa uzalendo, ubadhirifu na ufujaji na kutojali. Kwa kufanya hivyo tutamtendea haki Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kufanya maamuzi magumu aliyoyafanya kuwa licha ya sekta nyingi ambazo zinahitaji fedha hizi ameona kwamba atupe kipaumbele sekta ya afya kwa billioni hizi 80.

Mheshimiwa Spika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, lakini hujaunga mkono hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nimeunga mkono hoja na bima kwa wote Muswada unakuja Bungeni Juni kabla hatujamaliza Bunge. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, ubarikiwe sana. Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, Naibu Waziri TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango mingi na muhimu sana ambayo wameitoa katika mjadala wa bajeti hii na kwa muktadha huu katika eneo la *TARURA* na afya.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa muhtasari niweze kupita kwenye hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa. Kwanza kwa takriban asilimia 99 ya wachangiaji wamegusa *TARURA*, wametoa ushauri na michango mingi sana muhimu ya kuhakikisha kwamba tunaiwezesha *TARURA* kutenda kazi kwa ufanisi mkubwa unaotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua sana kwamba tuna changamoto kubwa ya barabara zetu zinazohudumiwa na *TARURA*, lakini uhitaji mkubwa wa madaraja na makalvati, lakini inatambua kwamba pia tuna tatizo la changamoto ya bajeti ya *TARURA*. Serikali imeendelea kuweka jitihada za kuhakikisha kwamba tunaboresha sana bajeti ya *TARURA* kuiwezesha kuhudumia mtandao wa barabara ambao inahudumia. Kwa mwaka wa fedha uliopita shilingi bilioni 275 zilitengwa ikilinganishwa na shilingi bilioni 578 za mwaka wa fedha ambao tunaelekea, ongezeko la bajeti ya *TARURA* kwa zaidi ya mara mbili na nusu. Kwa hiyo hii ni dalili kwamba Serikali inatambua sana umuhimu wa kuiwezesha *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, tunapokea mawazo na michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wametoa kuhusiana na kuboresha vyanzo vya mapato kwa maana ya simu, mafuta,

lakini na maeneo mengine. Serikali itaendelea kuyafanya tathmini na kuona njia bora zaidi ya kuongeza bajeti ya *TARURA* ili kuiwezesha kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wameongelea sana suala la kuona namna ambavyo vyanzo vya ndani vya halmashauri vitachangia ujenzi wa barabara kuititia *TARURA* na Serikali itatoa mwongozo kwa Majiji na Manispaa kuanza kutenga fedha kwa ajili ya kuchangia nguvu za *TARURA* kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwa nguvu ni kuhusiana na vigezo vinavyotumika katika mgao wa fedha za *TARURA* katika halmashauri. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali inatambua kwamba halmashauri zetu zinatofautiana kwenye ukubwa wa maeneo na hivyo mtandao wa barabara, lakini hali za kijiografia, milima, tambarare na mvua. Hivyo, katika kuweka vigezo hivi, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali itapitia vigezo hivi, kwa sababu vigezo na mgao uliowekwa awali ulizingatia zile barabara za kilomita elfu 56 na sasa tunakwenda 108,000 na hadi 144,000. Kwa hiyo niwahakikishie kwamba hii itapitiwa vizuri na itakwenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya kuthibitisha Mameneja wa *TARURA* na ni kweli kama tunavyofahamu *TARURA* haina muda mrefu tangu imeanza na taratibu hizi za uteuzi wa viongozi wa Serikali kuna hatua mbalimbali zikiwemo za upekuzi kwa maana ya *vetting*. Niwape taarifa Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imeendelea kufanya kazi hiyo na sasa imeshawafanyia *vetting* kwa maana ya upekuzi watendaji 111 kati ya 126, sawa na 88% na hawa hatua za kiutumishi za kuwathibitisha zitaendelea na zoezi hili ni endelevu.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni suala la miradi hii kuchelewa kuanza na barabara mara nyingine kujengwa wakati wa msimu wa mvua. Serikali imeboresha sana

utaratibu wa kupata zabuni kwa njia ya kielektroniki kwa maana *TANePS*. Katika mwaka wa fedha ujao tunatarajia miradi hii yote itatangazwa mapema, wazabuni watapatikana kwa wakati na barabara zitaanza kujengwa na kukarabatiwa kwa wakati na si wakati wa mvua.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili, maeneo ya madaraja na makalvati yamesisitizwa sana na Serikali imekwishatambua jumla ya madaraja 3,182 nchini kote, lakini pia makalvati 62,817 na imeweka mkakati ambao tutahakikisha labda kila baada ya mwaka wa fedha tunakwenda kutengeneza madaraja robo na makalvati pamoja na barabara za udongo kwenda changarawe.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la *TARURA* kwa ujumla wake Serikali itaendelea kuimarisha sana uwezo wa *TARURA* lakini pia kuuboresha sana mfumo wa utendaji wa *TARURA* ili kuhakikisha kwamba barabara zetu zinaboreshwani.

Mheshimiwa Spika, niende eneo la afya katika eneo hili Waheshimiwa Wabunge wamepongeza sana kazi kubwa ya Serikali ya kujenga na kukarabati miundombinu, hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati. Sisi kama Serikali tunaendelea na tunatambua kweli pamoja na kazi kubwa bado tuna mahitaji makubwa ya vituo vya afya na ndiyo maana katika mwaka wa fedha ujao, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Afya ametangulia kusema hospitali mpya 28 zimetengewa shilingi bilioni 14 zitaanza ujenzi, lakini hospitali za awamu ya kwanza 68 zitaendelea na ujenzi kwa bilioni 55.7, lakini pia hospitali 27 za awamu ya pili nazo zimetengewa bilioni 11.4.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la hospitali tunafahamu hospitali chakavu na kongwe tunakwenda kufanya tathmini na kuona njia bora zaidi kama ni kuzikarabati ama kuanza ujenzi ili ziweze kuwa na viwango bora. Vituo vya afya katika mwaka ujao tunatarajia kuendelea na ujenzi na ukamilishaji wa vituo vile vya afya 52, zimetengewa bilioni 15.6. Pia ujenzi wa vituo vipyta 121, kuna

shilingi bilioni 60.51. Jumla vituo vya afya 173 nchini kote kwa gharama ya shilingi bilioni 76.1, utaona ni kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, eneo la zahanati, tumetambua kwanza maboma Waheshimiwa Wabunge wameongelea suala la maboma ya zahanati ambayo wananchi wamechangia, tumekwisha yatambua maboma yote, mpaka Februari tulikuwa na maboma 2,350 na tayari katika mwaka huu wa fedha maboma 555 yametengewa shilingi bilioni 27.75 na tayari bilioni 20 zimekwishapelekwa, kazi za ujenzi zinaendelea, bilioni 7.75 zinaendelea na hatua za upelekaji kukamilisha maboma hayo.

Mheshimiwa Spika, mwaka ujao wa fedha maboma 758 yametengewa fedha kiasi cha shilingi bilioni 38.15 na hivyo tutakuwa tuna jumla ya maboma 1,313 ambayo tayari yatakuwa yanaendelea na ujenzi na ukamilishajili, tutabaki na maboma 1,037 ambayo tutaendelea kuyakamilisha kwenye mwaka mwingine wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la vifaa tiba dawa na vitendanishi, Mheshimiwa Waziri wa Afya ameелеza vizuri, lakini Serikali imeendelea kutenga fedha kwenye hospitali za Halmashauri. Hospitali 67 tayari zimeshapata bilioni 32.5, vituo vya afya tayari bilioni 26 mwaka huu, bilioni 15 tayari vifaa vimeshanunuliwa vinapelekwa, bilioni 11 hatua za manunuvi zinaendelea. Kwa mwaka ujao wa fedha bilioni 12.3 tunatarajia pia zitakwenda kununua vifaa tiba. Kwa hivyo tutahakikisha tunaendelea kuboresha vifaa tiba katika maeneo hayo. Dawa imeongelewa na Mheshimiwa Waziri wa Afya, tayari hatua za manunuvi ya dawa hizo zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kuongelea eneo la CHF, Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboresha na eneo hilo ni kipaumbele cha Serikali, tumeponga kuwa na ajenda ya kudumu kwenye vikao vyote vya kisheria kuanzia ngazi za mitaa, vijiji, kata hadi ngazi za mkoa. Tumekwishahamasisha wananchi na utaratibu huu unaendelea wananchi 3,300,000 wameshajiunga na shilingi bilioni 19 tayari zimekwishakusanya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt Festo Dungange. Sasa naomba nimkaribishe Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa David Silinde, una dakika 10 pia.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ambayo ni uwasilishaji wa hotuba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ningependa kutolea uafafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo zilijitokeza wakati Waheshimiwa Wabunge wanachangia katika hotuba ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi walichangia kuhusu miundombinu katika shule zetu na mionganoni mwa mambo ambayo walikuwa wamechangia; moja walipendekeza kwamba kwenye hizi shule kongwe za msingi ambazo nyingi ni mbovu, walikuwa wanaomba Serikali izingatie na izifanyie ukarabati. Mpaka ninavyozungumza sasa hivi Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeshazitambua shule 722 nchi nzima, shule kongwe na shule hizi ni zile ambazo zilijengwa kabla ya uhuru na nyingine zilijengwa mara baada ya kupata uhuru. Tumekubaliana kwamba wanafanya tathmini na baada ya kumaliza tathmini tutatumia hii miradi ambayo tuko nayo; tuna Mradi wa *GPE-LANES II*, Mradi wa Shule Bora, Mradi wa *Boost* na Mradi wa *EP4R* kuhakikisha hizi shule zinakarabatiwa kama Bunge linavyohitaji.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kuonyesha kwamba Serikali bado inahangaika na miundombinu na kuhakikisha watoto wetu wanasoma katika mazingira bora. Mwaka huu

wa fedha ambao tunakwenda kuupitisha kama Bunge lako litaidhinisha, tumedhamiria kujenga shule 300 kati ya shule 1,000 *complete school* na shule hizi zitajengwa katika zile kata ambazo hazina sekondari. Shule hizi zitakuwa za kidato cha kwanza mpaka cha nne, madarasa yatakuwa nane mpaka 12 na shule hizi shule moja itagharimu shule milioni 650 mpaka 700 mpaka inakamilika.

Mheshimiwa Spika, na zoezi hili ni endelevu tutalifanya Mwaka huu wa fedha, tutalifanya mwakani, tutalifanya mwaka kesho kutwa. Baada ya kukamilika kwa shule zote hizi maana yake tunatarajia kuwasaidia watoto wa masikini 400,000 kwa kujenga shule 1,000 katika safari hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, Serikali kwenye kuhakikisha kwamba tunaboresha miundombinu na tunamsaidia mtoto wa kike, tumekuballana kwamba tutajenga shule 26 maalumu za kimkoa na mwaka huu tunaanza shule 10 kati 26 na mwakani tutafanya 16 kuhakikisha kwamba kila mkoa unakuwa na shule ya wasichana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, shule hii ya wasichana itakua inachukua watoto 1,000 mpaka 1,200 nchi nzima, shule itakuwa *complete* itakuwa na kila kitu na tunajenga shule ya kisasa kweli kweli, kwasababu ghamrama ya shule moja hizi ni bilioni nne, ni kitu ambacho nafikiri kwa mara ya kwanza katika Serikali yetu tunafanya kitu kikubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, walijaribu kuzungumzia kuhusu ujenzi wa mahabara, ninafikiri kama kuna kazi kubwa Serikali imefanya ni kujenga mahabara za kisasa kwenye shule zote nchini. Na kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu Mwaka 2020, hakuna mwanafunzi hata mmoja aliyefanya mtihani wa *alternative to practical*, kwa hiyo, haya ni mapinduzi makubwa kabisa katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana utaona kabisa kwamba kwenye bajeti yetu tumetenga pale, mwaka huu wa fedha tunakwenda kufanya ukamilishaji wa mahabara

1,043, tunakwenda kumalizia maboma yale ambayo wananchi wameanzisha na kila boma litagharimu milioni 12.5 na mahabara moja tumepeleka kwa ajili ya kwenda kuzikamilisha milioni 30 na shule sekondari 1,841 na kwenye bajeti yetu, tumetenga bilioni 89.9 kuhakikisha zoezi hili linakamilika. kwa hiyo, tumedhimiria kabisa kuibadilisha sekta ya elimu katika ngazi ya elimu msingi ambayo tunaisimamia.

Mheshimiwa Spika, kwenye uhaba wa nyumba za walimu ni hoja ambayo hata Mheshimiwa Spika ulizungumza hapa na sisi tumeipokea kwakweli kuna changamoto kubwa. Tulikuwa tunazungumza na wataalam pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, tumekubaliana kuangalia namna bora ambayo tunaweza kuwasaidia walimu hasa walioko katika mazingira magumu kuhakikisha kwamba, sasa hii adha tunawaondolea. Kwa hiyo, tumedhamiria na tumekubaliana baada ya bajeti yetu tutakwenda kuanda mpango maalumu ili tuwasaidie walimu ambaao zaidi wanakaa katika mazingira magumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ajira za walimu ni kweli kabisa kwamba bado tunachangamoto ya walimu katika maeneo mengi, lakini tukiri wazi kwamba Serikali itaendelea kuwaajiri walimu kila mwaka kulingana na mahitaji na hali alisi ya kibajeti. Kwa hiyo, hilo ni kwamba kwa sasa hivi na ndiyo mpango wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, kwamba kila mwaka tutaajiri moja kwa kufanya *replacement* ya wale walimu ambaao wanastaifu, wanafariki, wanaacha kazi, au wanafukuzwa kwa mambo mengi yaani hatutakua tunaacha kwamba wanastaifu halifu atuaajiri, sisi tunesema kila mwaka tutaajiri kwa kufuatia hivyo.

Mheshimiwa Spika, jingine bajeti na mahitaji tutaongeza namba kulingana na mahitaji yaliyopo kuhakikisha kwamba tunaongeza ajira za walimu nchini. Katika kuondoa urasimu, tumeanzisha mfumo wa ajira ya mambo ya kazi unaitwa *Online teacher application system* na lengo la mfumo huu, moja ni kuondoa urasimu, pili ni mfumo ambaao unawapangia walimu vituo moja kwa moja yaani unakwenda pale unapo- *apply* unaona mpaka shule

unayotaka kuchagua. Kwa hiyo, kama kuna halmashauri zimeja maana yake ule mfumo utakuwa unakuonyesha huku kumejaa Kongwa au maeneo mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, na lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunawasaidia watu wote. Tumekubaliana kwamba tutaendelea kuzingatia walimu wanaojitolea mashulenii kwa muda mrefu, tutazingatia mwaka wa masomo wa wa wale wanafunzi kwa maana walimu wanafunzi waliohitimu, kuna walimu wameitimii 2012,2013,2014, hawajaajiriwa. Kwa hiyo, tumesema sasa hivi tutakwenda kuwazingatia hao kwanza, lakini wote tunahakikisha tuna wa-*accommodate* katika mfumo wetu na watu wote wanapata hiyo ajira. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwenye issue ya uhamisho ni moja ya ajenda ambayo ilizungumzwa sana na Wabunge, nieleze tu kweli kuna changamoto kubwa sana ya uhamisho hususani wa walimu na ndiyo moja ambayo imekua kero kubwa sana. Kwa hiyo, tumekubaliana Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Utumishi, tumeandaa mfumo unaitwa *Human Capital Management Information System*. Mfumo huu ni kwamba mtumishi atakuwa na uwezo wa kujiamisha *online* yani *straight* bila kuja huku chini uonge, fedha sijuwi ufanye kitu gani ndiyo upate uhamisho. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, na huu mfumo uko katika hatua za mwisho na sasa hivi tunachokifanya, tumemaliza kutoa mafunzo katika ngazi za halmashauri sasa tunakuja katika ngazi ya juu ili watu wote waanze ku-*applykupitia* huu mfumo. Kwa hiyo, lengo moja mtumishi atahama kupitia online; lakini pili taarifa mara yule mtumishi atakapokua amedhibitishwa kuhamza zitaamishwa mara moja ikiwemo na mshahara wake yaani tukimuamisha tunamuhamisha moja kwa moja. Kwa hiyo, tunaamini kwa hili tutaondoa changamoto ya watumishi kuchelewa kupata majibu yao ya kuomba utumishi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, tutoe rai tumesema kabisa katika huu mfumo ni lazima tuweke masharti vile vile, moja ya sharti tukalo liweka sasa hivi tumekua tukiajiri walimu, mwalimu akishafika kwenye kituo kwa mfano amepangia Kasulu, akishapata *check number* kesho yake anataka

kuhama, tumewecka *condition* kwamba mtumishi hatahama kituo mpaka amalize miaka tatu kwenye kituo chake cha kazi. Kwa hiyo, na mfumo uta *detect* hili jambo kwamba huyu mtumishi bado muda wake wa kuhama, kwa hiyo ataendelea kukaa kwa hiyo mfumo utamkataa direct, tumekubaliana tutafanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika bajeti yetu ya mwaka 2021/2022 tumetenga bilioni 50 kwa ajili ya kununua vitabu vya kujifunzia na kujifundishia kwasababu kumekua na changamoto kubwa sana na Wabunge wamezungumza, shule zetu nyingi hazina vitabu katika maeneo husika na mawili ya mwisho ni kwamba kumekua na madeni ya wastaafu ambayo yamezungumziwa. Na ninavyozungumza sasa hivi kuna baadhi ya halmashauri zimeanza kuwalipa watumishi baada ya kusikia mjadala unavyoendelea Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, na Waziri husika tumesha pitia yale madeni tuna wastaafu walimu 2,822 ambaao wanadai Serikali bilioni 3.9 kwa hiyo tunamalizia hatua za mwisho ili kuhakikisha watumishi wote waliofanya kazi kwa Amani kulitumikia Taifa letu nawenyewe wote wanalipwa kuhakikisha kwamba hatuendelei kuwasumbua kama ambavyo imekua ikitokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho mwaka huu Serikali inatarajia kupandisha madaraja, watumishi zaidi ya 90,000 nchi nzima, lakini kwenye hao watumishi wako na walimu kuna *fivey-three, percent* asilimia 53 ya hao watumishi ni walimu, kwa hiyo tuseme tu jamani Serikali imesikia mambo ya Wabunge, Serikali inafanya kazi, Serikali inajiamini kwa kitu ambacho tunajipanga na sisi tunawaomba Waheshimiwa Wabunge mtupitishie hii bajeti yetu ili twende tukatekeleze tumejipanga na tuko tayari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru naunga mkono moja ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Sana, nakushuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri David Silinde kwa maneno ya kutupa matumaini sana ahsante sana. Jamani hizi lakini wasichana ni nzuri lakini wavulana nao wanaachwa? (*Makof!*)

Kila wakati lazima nikumbushe hili jambo *seriously* wavulana wanaachwa *it is not a joke*, maana tumeimba kutoka ubelgiji mpaka leo watu tumeelewa masuala ya kinamama, kweli serious wavulana wanaachwa nyuma sana. Kwa hiyo, ni vizuri hizo shule hata kama inawanafunzi 1,000 ikawa na wavulana mia nne na wasichana mia sita kweli tutakua na Taifa la ajabu sana lenye wanawake waliosoma vizuri waelewa na wanaume waajabu ajabu, Serikali ijaribu kuangalia kidogo upande huo pia. Sasa dakika zilizobaki hizi mpaka saa kumi na moja kamili tumpe Mheshimiwa Waziri kama dakika thelathini thelathini na tatu hivi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Waziri karibu utumie mic ya mbele, karibu sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kule Tanga wanamwita Odo! (*Makof!*)

**WAZIRI NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nianze Mwenyezi Mungu kwa kunipa kipalicha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuhitimisha hoja yangu kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu pamoja na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kwa kutoa ufanuzi kuhusu michango ya Waheshimiwa Wabunge ambao wametoa katika mjadala wetu wa siku tatu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wameweza kupata fursa ya kuchangia hoja yangu, hoja yangu imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 103 ambapo Wabunge 89 wamechangia kwa kuongea na Wabunge 14 wamechangia kwa maandishi, lakini pia Wabunge 46 wamechangia kuitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kipekee ninawashukuru sana, Waheshimiwa Wabunge kwa maoni na ushauri wenu na katika hatua hii, niseme kwamba tumepokea maoni na ushauri wenu na tutaufanyia kazi. Kipekee nitambue mchango mkubwa wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ambao uliwasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Humphrey Polepole. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tumepitia mchango wa Kamati umesheheni madini, mazito ya kwenda kuimarisha utendaji kazi wa Mikoa na Tawala za Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, tunajibu tu kwa kifupi, lakini naomba niwahakikishie Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Pamoja na wajumbe wa Kamati yetu yote ambayo mmetushauri tutayafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunapokea pia pongezi ambazo mmetupatia mimi pamoja na Manaibu Mawaziri, tunawashukuru sana na niseme pongezi hizi hazitatuufanya tukapandisha mabega juu, bali litakua ni deni kwetu la kuhakikisha changamoto zilizopo katika mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa, tunakwenda kuzitatu. Tunaweza tusizimalize zote, lakini nataka kuwadhibitishia Waheshimiwa Wabunge, pia kuilinda imani kubwa na heshima kubwa ambayo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amenipa pamoja na Manaibu Mawaziri tutakwenda kufanya kazi na Waheshimiwa Wabunge mtaona matokeo ya kazi zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba wizara hii ikifanya vizuri basi tutakua tumeboresha maisha ya watanzania kwa sababu tunagusa maisha ya Watanzania katika ngazi zote, kwenye vitongoji takribani 64,384, vijiji 1,2319, mitaa 4,263, kata 3,956, tarafa 570, halmashauri 184, wilaya 139, pamoja na mikao 26. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge tunatambua jukumu ambalo tunalo la kuhakikisha kwamba tunaenda kuboresha shughuli za utawala na maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hususani katika masuala

ya elimu, Afya ya msingi, barabara, pamoja na Utawala Bora ikiwemo usimamizi wa rasilimali fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge zililhusu mambo mengi, lakini makubwa ambayo tumeyabaini ni matano, la kwanza ni miundombinu ya barabara chini ya wakala wa barabara vijijini na mijini *TARURA*; la pili ni masuala ya afya katika upande wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika zahanati, vituo vya afya, na hospitali zetu, za hal mashauri kuna masuala ya watumishi upatikanaji wa dawa vifaa, na vifaa tiba, bima ya afya ya jamii iliyoboreshwa, pamoja na matumizi ya *force account* katika ujenzi wa miundombinu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini hoja ya tatu ni elimu ikiwemo pia miundombinu, mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia ikiwemo uhaba wa watumishi; eneo la nne ni Utawala Bora na Ukusanyaki na usimamizi wa mapato kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa, lakini kubwa ambalo limejitokeza pia ni posho za Waheshimiwa Madiwani, madeni ya Madiwani kutokana na dhamana na mifumo ya ukusanyaji mapato. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo la tano ni masuala ya kuwawezesha wananchi kiuchumi hususani wanawake, vijana na watu wenyeulemavu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge zile hoja binafsi tutazjibu kwa maandishi kuhusu majimbo yenu moja moja. Lakini hapa nitatoa ufanuzi wa jumla katika masuala haya makubwa matano na nimshukuru sana Waheshimiwa Manaibu Mawaziri kwa kujibu baadhi ya hoja za waheshimiwa Wabunge na Waziri wa Afya kwa kujibu baadhi ya hoja. Kwa hiyo, nitajikita kwenye mambo makubwa mawili Utawala Bora na Usimamizi wa Rasilimali za Umma na pili ni suala la kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, labda tu kwa ufupi nitowe msisitizo kuhusu miundombinu ya barabara kama alivyosema Naibu Waziri Dkt. Festo Dugange karibu asilimia 90 ya michango imegusa *TARURA*. Waheshimiwa Wabunge tumelipokea ili na kama alivyosema Naibu Waziri kwenye hotuba yangu

tulisema mtandao wa barabara ambao umepitishwa ni kilometra laki moja na nane, habari njema tunamshukuru Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi wiki hii wameongeza mtandao wa barabara ambao utasimamiwa na TARURA kufikia kilometra 144,427, maana yake dada yangu Anne Kilango Malecela hata lile suala la vigezo vyta kugawa, fedha za TARURA linaenda pia kupatiwa ufumbuzi kupitia suala hili. (Makof)

Mheshimiwa Spika, hatutaangalia tu ukubwa wa barabara, tutaaangalia na masuala ya geografia ya eneo husika, kwasababu tukisema Tanga unipe kwa sababu ninakilometra labda 30 na mama Kilango ana kilometra 10 utupe fedha sawa siyo sahihi kwasababu yeche anamilima na mabonde na kuna mambo mengi ambayo tutazingatia. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge naomba niwaahidi tutatenda haki kwa kila jimbo, tutatenda haki kwa kila halmashauri. Lakini jambo la pili ambalo mmeliongea ni kuhusu kuongeza fedha kwa ajili ya TARURA, Serikali imelipokea, Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa amewasikia, Waziri wa Fedha amewasikia tutaendelea kulifanyia kazi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, suala la tatu kuhusu TARURA, Waheshimiwa Wabunge tumesikia maoni na ushauri wenu kwamba hakuna ushiriki mzuri wa Waheshimiwa Madiwani katika kupanga vipaumbele vyta ujenzi, matengenezo pamoja na maboresho ya barabara. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tumelitafakari ili na tumeamua kuanzia mwaka huu wa fedha vipaumbele vyote vyta ujenzi, kuboresha na matengenezo ya barabara vitapitishwa na baraza la Madiwani. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika zile siku tatu za Madiwani kukutana kwa ajili ya kujadili bajeti tunaongeza siku moja kabla itakuwa ni madiwani kujadili vipaumbele vyta matengenezo, maboresho, pamoja na ujenzi wa barabara.

Kwa hiyo, badala ya kikao cha siku tatu kitakuwa ni kikao cha siku nne na ikiwezekana waende *site* wakaone hizo barabara ambazo zinapendekezwa kujengwa na kufanyiwa maboresho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwasababu na sisi tunakaa katika Mabaraza ya madiwani, tuzingatie pia ushauri wa wawataalamu wetu tusije tukarudi nyuma kila diwani anataka apewe mita 200 au 300 za barabara. Kwa hiyo, pale ambapo labda tutashindwa kupata *consensus*, barabara ipi, kwa hiyo, tutaomba baraza la madiwani watuandikie wizara alafu tutafanya maamuzi, lakini tumewasikia, kwakweli ni haki yao madiwani zile ni barabara zao ziko katika maeneo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwasababu ya muda mradi wa *TAKTIK* na tumewasikia Wabunge kutoka Manispaa, Majiji na Miji upo kwenye maandalizi na tunaamini kwamba tutaukamilisha kwa wakati. Kwa hiyo, niwatowe hofu Wabunge hususani kutoka majiji, Mheshimiwa Naibu Spika ulisema, Mheshimiwa Mabula Mwanza, lakini na mimi pia Tanga ni mnufaika kwa hiyo kupata kwa Mbeya kutakua kupata kwa Tanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, siyo tu majiji sita ni majiji, manispaa na miji 45 tumeona manufaa ya mradi huu. Kuhusu *DMDP II*, watu wa Dar es Salaam tumewasikia na pia tuko katika maandalizi ya mwisho. Kwa hiyo, tunaamini pia kwamba mradi huu tutaukamilisha kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa nijikite katika hoja nyingine mbili; ya kwanza ni suala la utawala na usimamizi wa rasilimali fedha za umma. Tumepokea ushauri wa kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba tuzisimamie kikamilifu halmashauri nchini ili kuhakikisha kuongeza makusanyo kwa kuweka malengo halisia. Hili tumelipokea na nikweli halmashauri nyingi zina *under* bajet hazipangi malengo mahususi ya makusanyo,

lakini hata yale makusanyo katika taarifa yangu nimeonyesha hadi mwezi wa pili mwishoni makusanyo ni asilima 58 tu.

Mheshimiwa Spika, na makusanyo hayo kadri tutakavyoyapata ndipo tunaenda kuboresha huduma za jamii katika halmashauri zetu. Kwa hiyo, tumeandaa mwongozo wa usimamizi wa mapato ya ndani *revenue administration manual* ambayo umeainisha namna bora ya kuandaa mipango na bajeti ukusanyaji na usimamizi wa mapato haya.

Mheshimiwa Spika, pia Ofisi ya TAMISEMI tutaendelea kuwajengea uwezo wataalam wa ngazi za mikoa na halmashauri jinsi ya kuandaa mipango na kufanya makisio ya mapato ya ndani yenye kuakisi uhalisia. Pia sasa hivi ndani ya Wizara tunakamilisha Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (*Five Years Revenue Enhancement Strategic*) ambapo lengo pia ni kufanya maoteo ya makusanyo kwa kila halmashauri kwa miaka mitano. Kwa hiyo, suala hili tumelipokea na tutaenda kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, Serikali itizame mwenendo wa ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya ndani ya halmashauri kwa kutumia *machine* za kielektroniki (*POS*). Hili pia tumelipokea na sasa hivi tumeongeza matumizi ya *machine* za kielektroniki kwa ajili ya kukusanya mapato, tuna takribani *machine* za *POS* 26,873. Ndani ya kipindi kifupi tutaongeza *machine* 2,129 ambazo tutazisambaza katika halmashauri 49.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri tunalo pia tatizo la uadilifu wa baadhi ya watendaji wetu hususani wanaohusika na ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo, hatutasita kuchukua hatua za nidhamu pamoja na kuboresha sheria ndogondogo za halmashauri katika kuhakikisha kwamba mapato yanakusanywa na yanaenda katika njia sahihi na iliyokusudiwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tunaboresha mfumo wa makusanyo unaotumika

sasa hivi ili kuondoa kabisa mapokezi ya pesa taslimu kama Waheshimiwa Wabunge mlivyotushauri hapa lakini pia kutowasilishwa benki fedha zinazokusanywa na matumizi ya fedha mbichi kabla ya kuwasilishwa benki. Tunaamini kwamba mfumo huu utawawezesha pia walipa tozo, ushuru na kodi kujua wanachodaiwa, kupata *control number* na kufanya malipo kwa mtandao kwa wakati na tunategemea utaanza tarehe 01 Julai 2021.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuhusu kuibua vyanzo vipyta ya mapato ili kuziwezesha halmashauri kutoa huduma bora. Nalo hili tumelipokea na ndiyo maana pia katika bajeti yetu moja ya kipaumbele tumeeleza pia tunaenda kuongeza nguvu ya kuhakikisha kwamba tunawekeza au tunaziwezesha halmashauri katika kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara pamoja na uwekezaji. Lengo letu ni kuhakikisha tozo, kero kwa wananchi zinaondoka, tujike kwenye vile vyanzo ambavyo tunajua kwa hakika kwamba vitawenza kutuletea mapato.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya CAG imeonyesha kwamba halmashauri zimeshindwa kukusanya takribani shilingi bilioni 31 katika mwaka wa fedha 2020/2021 wakati wenyewe wamesema hiki ni chanzo lakini wameshindwa kukusanya. Kwa hiyo, tumelipokea na hili tutalifanyia kazi ikiwemo pia kuweka miradi ya kimkakati katika halmashauri nyingi kwa sababu pia tumeona ni vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni katika utawala bora, Kamati na Waheshimiwa Wabunge wameshauri Ofisi ya Rais-TAMISEMI isimamie Sekretarieti za Mikoa kuandaa taarifa za mipago na bajeti za mafungu. Tunakubaliana na ushauri na mimi mwenyewe nataka nikiri nimeona tunalo tatizo. Juzi nilienda kwenye Sekretarieti ya Dodoma, kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa imeanzishwa Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa. Huyu Katibu Tawala wa Mkoa ana wataalam wote wa fedha, wahasibu, miundombinu *including* wahandisi, wanasheria, madaktari na watu wa elimu lakini nikawauliza katika huu mwaka wa fedha wa 2021 mlishakaa na halmashauri yoyote ya Dodoma

mkachambua mipango yao ya maendeleo na makusanyo yao; *internal auditors* mlisshawahi kuwaita mkawauliza mnafanya kitu gani hawajawahi kufanya. Kwa hiyo, tunakwenda kuzifumua Sekretarieti za Mikoa, tunakwenda kujenga uwezo wa Sekretarieti za Mikoa kwa sababu sheria inasema wao wana wajibu wa kuzisimamia, kuzishauri na kuzijengea uwezo halmashauri katika masuala mazima ya mapato na maendeleo katika halmashuri zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika ofisi ya *RAS* kuna watu wanaitwa Katibu Tawala Msaidizi wapo kama sita, nane au kumi, wale watu ni wakubwa kuliko Wakurugenzi wa Halmashauri kwa sababu ni *Assistant Directors; DEDyuko* chini ya *RAS* lakini sasa tumegundua kuna baadhi ya Wakurugenzi hawawaheshimu hawa ambao ni Makatibu Tawala Wasaidizi. Kwa hiyo, pia natuma salama kwa Wakurugenzi wa Halmashauri unapofuatwa na Katibu Tawala Msaidizi kumbuka ni bosi wako unatakiwa kumsikiliza, kumheshimu na kutekeleza maelekezo yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini tumeona upande wa pili wa shilingi, kuna baadhi ya hawa Makatibu Tawala Wasaidizi wenyewe hawajiamini na hawana uzoefu. Sasa unaenda vipi kukaa na Mkurugenzi wakati wewe mwenyewe hujiamini na huna uzoefu, ndiyo maana nasema tunaenda kuzifumua Sekretarieti za Mikoa kwa sababu sitegemei Waziri wa TAMISEMI ndiyo azunguke nchi nzima wakati kuna Katibu Tawala wa Mkoa na wataalam zaidi ya tisa katika ofisi yako ambao wana jukumu la kisheria kusimamia halmashauri zetu. Kwa hiyo, hili tunaenda kulifanya kazi na tutasaini *performance contract*na Wakuu wa Mikoa kwa sababu wao ndiyo wanasmamia hizi Sekretarieti za Mikoa. Kwa hiyo, ushauri huu tumeupokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la posho za Madiwani kuna hoja mbili; hoja ya kwanza ilikuwa ni kuongeza posho za Madiwani. Tumewasikia Serikali iko hapa itafanya kazi suala hili. Hoja ya pili ni kwamba posho hizi zilipwe moja kwa moja kupitia ruzuku ya Serikali. Tumelipokea pia na tunakubaliana na maoni ya Waheshimiwa Wabunge kwamba Madiwani

wamekuwa wakifanya kazi kubwa na nzuri ya kusimamia shughuli za maendeleo katika majimbo yetu. Mimi nataka kukiri hata mimi nikienda Tanga Mjini namtafuta Diwani yule ndiye mpambanaji wangu, ndiye askari wangu.

Mheshimiwa Spika, tumefanya tathmini ya haraka haraka ya miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2019/2020 halmashauri 97 zimekusanya wastani wa mapato ya ndani chini ya shilingi bilioni mbili, halmashauri 71 zimekusanya wastani wa chini ya shilingi bilioni tano, ni halmashauri 17 tu ndizo zilizokusanya wastani ya mapato ya ndani ya shilingi bilioni tano kwa mwaka. Kwa hiyo, ni kweli kwamba halmashauri nyingi zinashindwa kulipa posho za Madiwani kikamilifu hali ambayo inasababisha kama alivyosema mtani wangu Mheshimiwa Kasalali kwamba Diwani anajiona ni dhaifu mbele ya Mkurugenzi kwa sababu ni Mkurugenzi atakavyoamua na kulipa posho anasema sina mapato. Kwa hiyo, hata ule usimamizi wa halmashauri maana mtu wa kwanza wa kusimamia fedha za Serikali kwenye halmashauri ni Baraza la Madiwani sio mtu mwingine ndiyo inakuja *Regional Secretariat. (Makof)*

Mheshimiwa Spika, hili naomba niseme tumelipokea na kwa kweli tunakubaliana na nyie kwamba ni sehemu ya kero, bugudha lakini pia kutoheshimisha kada ile ya Madiwani. Serikali imewasikia na tunaendelea kufanya uchambuzi. Tumeangalia tuna Madiwani takribani 5,275 inayojumuisha Madiwani 3,956 wa Kata na Madiwani 1,319 wa Viti Maalum. Niwaombe sana tulibebe hili twende tukafanye uchambuzi zaidi, ikiwemo posho ya Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la kuboresha mahusiano ya viongozi wa mikoa, wilaya ya halmashauri. Tunalipokea, tutaendelea kutoa elimu na mafunzo kwa viongozi wetu Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, ma-DAS, kuhusu kila mtu kutambua wajibu na mipaka katika kazi zake na majukumu yake na umuhimu wa kufanya kazi kama timu. Niseme tu tumekuwa pia tukishirikiana na Taasisi ya Uongozi

kwa ajili ya kutoa mafunzo lakini pale ambapo kumekuwa na mgogoro pia tumekuwa wepesi wa kwenda kulifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika suala la utawala bora, kuna suala la matumizi ya *force account*, Wabunge wengi mmekubali kwamba ni utaratibu mzuri lakini pia ni kichaka cha upotevu wa fedha. Tunakuliana nanyi, tutaenda kuongeza nguvu ya kusimamia eneo hili lakini tukubaliane kwamba *force account* imetusaidia sana kwa sababu kuna maeneo Ofisi ya Jengo la Mkuu wa Mkoa tunaletewa bili ya bilioni 1.5 wakati sehemu nyingine inajengwa kwa shilingi milioni 300 au400. Kwa hiyo, tunakubali kwamba ipo haja ya kuimarisha ubora hususani kuwa na Wahandisi na watu wa QS katika halmashauri zetu. Habari njema kwa sababu tuna uhaba wa Wahandisi katika halmashauri zetu, tunao kama 80 katika halmashauri zote 184, tumeongea na Mkuu wa Majeshi ana Wahandisi katika Jeshi, kwa hiyo, tunamuomba ikiwezekana tuwashikize katika halmashauri zetu ili pia waweze kufanya kazi hii ya kutoa ushauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la TAMISEMI isimamie na kuhakikisha fedha za uendeshaji katika ngazi za chini za kata na vijiji zinakwenda, hili totalisimamia. Pia kuna masuala ya halmashauri zinazodaiwa na benki, mikopo ya Waheshimiwa Madiwani iliyotokana na dhamana ya posho za kila mwezi ikamilishwe, hili pia tumelipokea na madeni yameanza kulipwa, hadi Juni 30 madeni ya mikopo ya Madiwani yalikuwa shilingi bilioni 5.5 kati ya shilingi bilioni 10.9 ambazo zimelipwa.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la migogoro na kero za wananchi kwamba tuongeze jitihada za kuhakikisha kwamba tunatatua migogoro ya ardhi, wananchi kunyang'anywa mali zao lakini pia kuna mambo mengine ya mirathi. Nafurahi sana nimeongea na Waziri wa Katiba na Sheria simuoni hapa pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali tumeamua kuchukua hatua ya mpito tunakwenda kuwatumia Wanasheria katika Ofisi za Makatibu Tawala wa Wilaya ambao wapo tutawaongezea jukumu pia la kutoa

huduma kwa wananchi katika halmashauri zao ambao wana matatizo ya kisheria hususani migogoro ya ardhi, mirathi pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, masuala ya kiutawala yapo mengi Waheshimiwa Wabunge tumeyapokea, lakini kubwa ni kwenda kudhibiti makusanyo ya halmashauri pamoja na matumizi ya Serikali. Ukingalia bajeti hii shilingi trillioni tatu tunazipeleka kwenye halmashauri, maana yake ni lazima tuongeze nguvu ili fedha hizi ziweze kuleta matokeo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvezeshaji wa wananchi kiuchumi, tumepokea maoni au ushauri wa Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba tuongeze umakini katika kusimamia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali. Hili wala sihitaji kuchukua muda mrefu, tunakubaliana na ushauri na hususani kwanza kuhakikisha badala ya mikopo ile kuwa inatolewa kiduchukiduchu itolewe kwenye miradi mikubwa ambayo itaweza ku-*generate* ajira lakini pia itaweza kuleta mapato na faida kwenye halmashauri. Kwa hiyo, tutaweka mgao maana pia tusiwasahau hawa akina mama wangu wanaopika maandazi, wanaochoma mishikaki na vijana hawa wanaouza karanga, kwa hiyo, tunaweza tukasema katika kila hela ile inayotolewa kwa mikopo basi asilimia fulani iende kwa hawa wajasi lamali wadogowadogo. (*Makof!*)

